**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Sita – Tarehe 7 Septemba, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tumekutana tena kwa Mkutano wa Nne, Kikao cha Sita. Nadhani Waheshimiwa Wabunge mnazidi kuona jinsi ambavyo Bunge likianza mchana lilivyo na raha zake kuliko kurupukurupu ya asubuhi. Hata Waheshimiwa Mawaziri wanapata nafasi ya kuona ofisi zao zinafananaje, vilevile wanakutana na wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Waziri Mkuu

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 14 la tarehe 02 Aprili, 2021;
2. Toleo Na. 15 la tarehe 09 Aprili, 2021;
3. Toleo Na. 16 la tarehe 16 Aprili, 2021
4. Toleo Na. 17 la tarehe 23 Aprili, 2021;
5. Toleo Na. 18 la tarehe 30 Aprili, 2021;
6. Toleo Na. 19 la tarehe 07 Mei, 2021;
7. Toleo Na. 20 la tarehe 14 Mei, 2021;
8. Toleo Na. 21 la tarehe 21 Mei, 2021;
9. Toleo Na. 22 la tarehe 28 Mei, 2021;
10. Toleo Na. 23 la tarehe 04 Juni, 2021;
11. Toleo Na. 24 la tarehe 11 Juni, 2021;
12. Toleo Na. 25 la tarehe 18 Juni, 2021;
13. Toleo Na. 26 la tarehe 25 Juni, 2021;
14. Toleo Na. 27 la tarehe 02 Julai, 2021;
15. Toleo Na. 28 la tarehe 09 Julai, 2021;
16. Toleo Na. 29 la tarehe 16 Julai, 2021;
17. Toleo Na. 30 la tarehe 23 Julai, 2021;
18. Toleo Na. 31 la tarehe 30 Julai, 2021;
19. Toleo Na. 32 la tarehe 06 Agosti, 2021;
20. Toleo Na. 33 la tarehe 13 Agosti, 2021;
21. Toleo Na. 34 la tarehe 20 Agosti, 2021;
22. Toleo Na. 35 la tarehe 27 Agosti, 2021.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tunakushukuru. Sasa nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Prof. Kilangi. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kwa niaba yake anakuja Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Olelekaita Kisau. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete.

Na. 66

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Makete Mjini**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Stendi ya Mabasi Makete Mjini?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Festo Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Makete katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 ilitenga eneo lenye ukubwa wa ekari 3.1 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Halmashauri ilianza ujenzi kwa gharama ya shilingi milioni 40; na katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Halmashauri imepanga kutenga fedha kwenye mapato ya ndani ili kuendelea na ujenzi wa kituo hicho

Mheshimiwa Spika, Serikali inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Makete kufanya tathimini ya ujenzi wa kituo cha mabasi na kuandaa andiko ili kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Festo nimekuona, uliza swali lako.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini nilikuwa napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Makete ya mwaka 2014 na Makete ya sasa ni ya tofauti sana. Kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imejengwa lami ambayo imefika hadi Makete, na kwa hiyo mabasi kutoka Dar es salaam na mikoa mingine tayari yameshaanza kuingia Makete.

Je, Serikali ipo tayari kutupatia fedha kutoka kwenye mpango wa miradi ya kimkakati ili Makete ipate kituo cha mabasi kizuri ambacho kinaendana na uhitaji mkubwa wa sasa ambao tunao?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili kama utakuwa tayari twende Makete kwa ajili ya kuangalia ukubwa wa uhitaji wa kituo cha mabasi pale ndani ya Wilaya ya Makete. Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kutoka kwa Mbunge wa Makete Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuwatetea wananchi wa Jimbo la Makete katika miradi mbalimbali ya kiuchumi pamoja na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, pili, nimhakikishie kwamba Serikali inatambua kwamba baada ya utekelezaji mzuri wa Ilani na barabara ya lami kutoka Njombe kwenda Makete, ambayo pia itatoka Makete kwenda Mbeya Mji wa Makete utafunguka na una kila sababu ya kupata stendi ya kisasa ya mabasi. Ndiyo maana katika katika jibu la msingi, na ninaomba niendelee kusisitiza, kwamba tunawashauri Halmashauri ya Makete, waandae andiko la kimkakati la ujenzi wa stendi ya mabasi ya kisasa ambalo litaonesha *business plan* yake na uwezo wa kulipa fedha zile ili tuweze kutafuta vyanzo vya fedha, iwe Serikalini au kwa wadau mbalimbali, lakini pia na mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tatu; nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili. Naomba tukae ili tupange ratiba yetu tufike pale; pamoja na mambo mengine tuangalie ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi. Ahsante.

**SPIKA:** Kule Msekwa nimemuona Mheshimiwa Neema Lugangira, uliza swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uhitaji wa stendi kuu ya mabasi uliopo kule Makete unafanana kabisa na uhitaji wa Stendi ya Mabasi ya Bukoba Mjini. Ningependa kupata kauli ya Serikali; je, sisi Bukoba Mjini tutapata lini stendi mpya

ya mabasi hususan ukizingatia kwamba Wilaya ya Bukoba Mjini ndiyo *reception* ya Mkoa wetu wa Kagera na inaunganisha Kagera na nchi ambazo tunapakana nazo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Stendi ya Mabasi ya Mji wa Bukoba ni miongoni mwa stendi ambazo Serikali imeziwekea kipaumbele cha kutosha kwa kuhakikisha kwamba kinatafutiwa fedha; lakini pia nitaangalia kwenye miradi ile ya kimkakati ya *TACTIC* kama Halmashauri ya Mji wa Bukoba imo ili tuweze kujiridhisha kwamba stendi ile itakuwa sehemu ya ule mradi ambao utakwenda kuhudumiwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Lugangira, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Steven Byabato, Naibu Waziri wa Nishati na Mbunge wa Bukoba Mjini kwa kazi kubwa ya kufuatilia stendi hii na mambo mengine; na kwamba nimhakikishie, sisi kama Serikali tutashirikiana nao Waheshimiwa Wabunge wote kutekeleza miradi hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee nilikuona, uliza swali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri kabla haujawa Mbunge na hatimaye Naibu Waziri tulikuwa wote Manispaa ya Kinondoni; na unafahamu kwamba tulikuwa

tuna mpango wa kujenga stendi Kata mashuhuri ya Kawe yenye wananchi wengi sana. Sasa, sasa hivi umeshakuwa Naibu Waziri upo huko kwenyewe huko. Sasa naomba uniambie, kwa sababu mkakati wa Kinondoni unaujua, ni lini tutajenga Stendi ya Kawe? Kwa sababu tuna eneo la iliyokuwa Wizara ya Mifugo na eneo la *Tanganyika Packers.* Ni lini tutajenga stendi Kata ya Kawe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Ummy Mwalimu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Dugange kwa majibu mazuri, lakini nimshukuru Mheshimiwa Halima Mdee kwa swali lake, kwamba lini tutajenga stendi katika Kata ya Kawe.

Mheshimiwa Spika, nimesimama, tulipata maelekezo kutoka kwa Kamati yako ya Bajeti lakini pia Kamati ya Utawala na TAMISEMI kwamba tufanye mapitio ya mwongozo wa kutekeleza miradi ya kimkakati nchini, kwa sababu inavyoonekana mwongozo ule unazipendelea Halmashauri zenye mapato makubwa na kuzifanya Halmashauri zenye mapato madogo kutopata rasilimali fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu fedha hizi ni *grant*, ukipewa hazirudi; kwa hiyo tulijadili, na sisi tumekubaliana na ushauri wa Kamati. Unamuacha Makete, unampa Kawe, Kinondoni ambaye ana mapato ya zaidi ya bilioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunapitia mwongozo ili halafu sasa tuweke vigezo vya jinsi ya ku-*finance* miradi ya kimkakati ili hata Halmashauri zisizo na fedha na mapato ya kutosha waweze kupata fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa stendi, masoko na vitega uchumi vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Kawe itasubiri kwa kuwa kipaumbele chetu tutaangalia uhitaji wa Halmashauri maskini au zenye mapato madogo Zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa makofi hayo madogo, kwa hiyo Kawe *mjiju* kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Bado tupo TAMISEMI Waheshimiwa, swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi.

Na. 67

**Wanafunzi Waliochaguliwa Kwenda Kusomea Kozi ambazo Hawakuzichagua Katika Matokeo ya Kidato cha Nne**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia Wanafunzi ambao wamechaguliwa kwenda kusomea kozi ambazo hawakuzichagua katika Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha nne yaliyotoka mwaka 2021.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais_TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali hutumia fomu maalum itwayo *Student Selection Form (Sel-Form)* ambayo humuwezesha mwanafunzi kuchagua tahasusi na kozi anazopenda kusomea endapo atachaguliwa kujiunga na kidato cha tano au vyuo vya ulimu wa ufundi, ambapo

hujazwa na wahitimu wote wanaotarajia kuhitimu kidato cha nne mara baada ya kumaliza mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, mwanafunzi anaweza kuchagua wapi anahitaji kwenda kusoma, kama ni kuendelea na masomo ya elimu ya Sekondari (kidato cha tano), vyuo vya elimu ya ufundi, vyuo vya ualimu au vyuo vya afya. Kwa kila chaguo mwanafunzi hupewa machaguo matano ya kuchagua tahasusi na shule anayohitaji kusoma au kozi na chuo anachohitaji kusoma. Endapo mwanafunzi ataridhia atapewa machaguo matano ya kozi na vyuo vya kati anavyohitaji kusoma. Wanafunzi huchaguliwa kujiunga na vyuo vya elimu ya ufundi, vyuo vya afya au ualimu endapo wamechagua kama chaguo la kwanza kwa sababu wanataka kupata ujuzi badala ya kujiunga na kidato cha tano au wamekosa nafasi ya kujiunga na kidato cha tano.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuwagharamia wanafunzi wanaochaguliwa kusomea kozi mbalimbali katika vyuo vya kati isipokuwa wanafunzi wanaochaguliwa moja kwa moja kujiunga na vyuo vya ufundi vitatu ambavyo ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam *(DIT),* Chuo cha Ufundi Arusha *(ATC)* na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imejikita kuongeza nafasi za kudahili wanafunzi wa kidato cha tano, hivyo idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2021 ni wanafunzi 87,663 ikilinganishwa na wanafunzi 73,113 waliochaguliwa mwaka 2020.

**SPIKA:** Tutakubaliana kwamba jibu hilo lilikuwa refu sana. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kusema ukweli katika hili Serikali lazima ikubali kwamba imefanya makosa. Mwanafunzi amefaulu, ana ndoto ya kuwa daktari, *combination* ya *PCB* imekubali wewe

unampangia aende Dar es salaam akasome *IT,* chuo ambacho hajakichagua, hana *interest* na masomo hayo? Na hii imetokea maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni hili, kwa nini Serikali isiwahurumie hawa wanafunzi ambao kwanza wana *passion* na masomo yao waliyoyachagua na wamefaulu masomo hayo, mkawaruhusu wakaenda *form five* au kusomea hizo *course* walizofaulu na walizochagua kuliko kumlazimisha mwanafunzi ambaye amefaulu kwenda kusomea kitu ambacho hajapanga wala hakihitaji kwenye maisha yake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Samahani Mwenisongole, hili si ndio lililokuwa swali lako la msingi?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hajajibu swali. Mimi nilitaka wawaruhusu hawa wanafunzi warudi waende wakafanye.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa George. Tunaendelea na Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, bado tupo TAMISEMI.

Na. 68

**Migogoro ya Wakulima na Wafugaji – Mkoa Wa Lindi**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatafuta mkakati wa kudumu wa kutatua tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo ya Mkoa wa Lindi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi kumekuwa na ongezeko la migogoro ya wakulima na wafugaji, hususan katika Wilaya za Kilwa, Nachingwea na Liwale. Migogoro hii imetokana na ongezeko la mifugo ambapo kumeongeza uhitaji wa nyanda za malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi pamoja na Halmashauri ya Wilaya za Kilwa, Nachingwea na Liwale imefanya uhakiki na kubaini jumla ya migogoro 19, ambapo jumla ya migogoro 12 imetatuliwa na migogoro saba iko katika hatua mbalimbali za utatuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sekretariati ya Mkoa wa Lindi imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 81, na kuunda kamati ya utatuzi wa migogoro kwa kila halmashauri ili kuwahamasisha wafugaji kufuga kibiashara kwa kuendeleza *ranch* ndogondogo, na kila halmashauri kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji vitano kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Halmashuri za Mkoa wa Lindi na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kutumia kiasi cha shilingi milioni 279.22 kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 15, ikiwa ni hatua za utatuzi wa migogoro hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali pia napongeza kazi kubwa inayofanywa na Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi na Halmashauri zake kupambana na migogoro hii ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni lini Serikali itakuwa na mkakati wa kujenga mabwawa ama marambo kwa ajili ya kunywesha mifugo hiyo? Nasema hivyo kwa sababu katika jibu la msingi tumeona kuwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla unasoma swali lako.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Hapana, halipo.

**SPIKA:** Nakuona. *(Kicheko)*

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hivyo basi, naomba...

**SPIKA:** Ninao mtambo hapa, inabidi uniangalie mimi huku.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Kama hivi.

**SPIKA:** Hapo sawa. *(Kicheko)*

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni u-*form one* huo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali pia napongeza kazi inayofanywa na Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi na Halmashauri zake katika kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni lini itajenga mabwawa kwa ajili ya kunywesha mifugo hiyo? Hapa tumeona katika jibu la msingi shida kubwa ni kugombania maji pamoja na malisho.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaomba kazi hii ya kutatua migogoro katika Mkoa wa Lindi iharakishwe maana Sekretarieti ya Mkoa imeelemewa na migogoro hiyo. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na suala hili?

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tecla. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tecla, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kutambua umuhimu na katika mkakati wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan wa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji, katika bajeti ya mwaka huu 2021/2022 tumetenga jumla ya shilingi milioni 900 kwa ajili ya kujenga mabwawa katika Mkoa wa Lindi. Bwawa moja litajengwa katika Wilaya ya Liwale na lingine katika Wilaya ya Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Lindi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejipanga vyema kwa kutumia Kamati inayoshughulikia migogoro ya ufugaji na wakulima kwenda kuweka kambi kuzungumza nao na kushirikiana katika kutafuta mbinu za kusuluhisha migogoro hii, ikiwa ni pamoja na kutatua lile tatizo la nyanda za malisho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi.

Na. 69

**Utunzaji wa Bahari**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari ili kurejesha mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuweka matumbawe bandia katika maeneo kadhaa ya mwambao wa Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Katika eneo la Sinda Pwani ya Dar es Salaam eneo la mita za mraba 2000 limepandikizwa matumbawe bandia. Vilevile, kwa upande wa Unguja na Pemba jumla ya matumbawe bandia 90 aina ya *reef ball* yalipandikizwa katika Kijiji cha Jambiani; na matumbawe bandia 46 na mapande maalum 6 katika Kijiji cha Kukuu. Matumbawe hayo yalifuatiliwa ukuaji wake kitaalam na matokeo yameonyesha mafanikio makubwa kwa kuimarika kwa mazalia ya samaki na hivyo kuongezeka kwa kiwango cha samaki katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na upandaji wa mikoko, Serikali imekuwa ikiongeza jitihada zaidi katika upandaji wa mikoko katika fukwe mbalimbali nchi nzima kwa kushirikiana na asasi binafsi na washirika wa maendeleo. Takribani hekta 7 za mikoko zilipandwa Unguja na hekta 10 zilipandwa Pemba kwa mwaka 2020/2021. Upandaji wa hekta 13.5 unaendelea mpaka sasa na matarajio ni kupanda hekta 15 kwa mwaka huu. Aidha, kwa upande wa Tanzania Bara, hekta 105 zimepandwa katika Delta ya Rufiji na matarajio ni kupanda hekta 2000 kwa pwani yote ya Tanzania Bara ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sote kuhakikisha tunatunza, tunahifadhi na kusimamia matumbawe na mikoko pamoja na mifumo ya ikolojia inayopatikana ndani ya bahari zetu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo nimekuona umesimama.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri bado nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeona jitihada mbalimbali za wananchi wakizichukua kwa makusudi katika kupanda mikoko kwa lengo na madhumuni ya kuhifadhi mazingira, kuongeza mazalia ya samaki lakini kuzuia maji ya bahari kupanda nchi kavu. Mfano mzuri ni wananchi wa Kijiji cha Mjini Wingwi na Sizini Wilaya ya Micheweni. Swali la kwanza, je, Serikali inawapa matumaini gani wananchi hawa wa Mjini Wingwi na Sizini kwa kuwapatia misaada ya kifedha na vifaa kama boti kwa ajili ya *patrol* kama sehemu ya kuhamasisha na kuwapa moyo kuendelea na jitihada hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufuatana nami baada ya Bunge hili mpaka kwenye Kijiji cha Mjini Wingwi na Sizini kwa lengo la kwenda kuona jitihada za wananchi hawa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali haya, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Omar Issa kwa juhudi yake ya kutunza mazingira katika maeneo yake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anauliza Serikali itawapa matumaini gani wananchi? Serikali kwa sababu inasikiliza na inathamini juhudi za wananchi, naomba hili tulichukue na baadaye tutakaa pamoja naye na

wataalamu wetu tuone namna gani tunawapatia motisha wananchi ambao wanajitahidi kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili mimi niko tayari kabisa kufuatana naye baada ya Bunge hili kwenda kuona na kutafuta njia sahihi ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Nishati na swali la Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma.

**MHE. SAMWELI H. XADAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla ya kuuliza swali, naomba nifanye marekebisho kidogo kwenye jina langu, mimi naitwa Samweli Hhayuma Xaday badala ya Samweli Xaday Hhayuma.

Na. 70

**Kujenga Kituo cha Kupoza Umeme – Katesh**

**MHE. SAMWELI H. XADAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha kupooza umeme Mjini Katesh kwani kuna *line* ndefu ya Km 780 hivyo kusababisha umeme kukatika mara kwa mara Wilayani Hanang?

**SPIKA:** Lile jina la mwisho linatamkwaje hebu rudia tena matamshi tu.

**MHE. SAMWEL H. XADAY:** Mheshimiwa Spika, Xaday *(Hadai). (Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kuwasaidia muweze kujua namna linavyotamkwa ni Xaday *(Hadai).* Majibu ya swali la Mheshimiwa Xaday tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** aljibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samwel Hhayuma Xaday, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* limeanza taratibu za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na kituo kidogo *(switching yard)* cha kilovoti 33 kutoka njia kuu ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 inayoendelea kujengwa kutoka Singida hadi Namanga katika Kijiji cha Mogitu Wilayani Hanang.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo hicho utaboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Wilaya ya Hanang na maeneo jirani utaanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika Juni, 2023. Gharama ya mradi ni takribani shilingi bilioni 2.6. Utekelezaji wa mradi huu utagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100.

**SPIKA:** Mheshimiwa Xaday.

**MHE. SAMWELI H. XADAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kufuata mipaka ya kiutawala katika kutoa huduma za umeme, kwa mfano, Kata ya Masakta iko kwenye Wilaya ya Hanang kiutawala lakini inahudumiwa na *TANESCO* Babati na hii imekuwa ikisababisha usumbufu kwa wananchi kufuatilia huduma. Je, Serikali ina mkakati gani kurekebisha tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imefanya kazi kubwa kwenye mradi wa *REA* kupeleka umeme vijijini lakini kwenye vijiji husika maeneo yanayofikiwa au watu wanaopata umeme ni wachache. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanapata umeme na kufika kwenye hatua ya vitongoji hasa kwenye Jimbo langu la Hanang? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato majibu ya maswali hayo, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Samweli Xaday, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo ambapo mikoa au wilaya za ki-*TANESCO* haziendani na mikoa au wilaya za kiserikali na nia kuu ya Shirika la *TANESCO* chini ya Serikali ilikuwa ni kuhakikisha kwamba huduma zinawafikia wananchi katika maeneo ambayo yanafikika kirahisi. Kwa kutoa mfano katika Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Kiteto inahudumiwa na Mkoa wa Dodoma lakini tunayo wilaya ya ki-*TANESCO* inaitwa Simanjiro na wilaya nyingine inaitwa Mererani. Wilaya ya Simanjro ki-*TANESCO* inahudumiwa na Mkoa wa Kilimanjaro lakini wilaya ya ki-*TANESCO* ya Mererani inahudumiwa na Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa wanaofahamu ni rahisi sana kutoka Simanjiro kwenda Kilimanjaro, ni rahisi sana kutoka Mererani kwenda Arusha kuliko kurudi Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara ambapo ni Babati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nia ya Serikali ilikuwa ni kuhakikisha kwamba huduma zinawafikia wananchi kirahisi wanapohitaji kwenda ofisini kupata huduma lakini pale ambapo *TANESCO* inatakiwa iende kuwafuata wananchi kuwahudumia au kwenda kufuata vifaa katika bohari.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga hatua kubwa sana ya kuhakikisha miundombinu inafika karibia kila sehemu na hivyo ni rahisi sana kufikisha huduma kwa wananchi mbalimbali kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, kila inapowezekana Serikali imeamua sasa ipeleke utawala wa ki-*TANESCO* sawasawa na utawala wa kiserikali ili kuhakikisha mtu anapata huduma kutoka kule ambako anategemea kuipata na maendeleo hayo ataendelea kuyaona kadri muda unavyozidi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili ni kweli na kama tunavyofahamu maendeleo ni hatua. Kwa harakaharaka tu mwaka 2007 wakati *REA* inaanza ilipita vijiji 506 ndio vilikuwa na umeme lakini taarifa zinaonyesha kufikia 2015 tulikuwa tuna vijiji 2018 vyenye umeme na kufikia mwaka huu 2021 taarifa zetu zinaonyesha tuna vijiji 1950 kati ya 12,268 ambavyo viko Tanzania kwa ujumla wake. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba maendeleo ya kupeleka umeme ni endelevu na kadri Serikali inavyoendelea kupata pesa kwa kujibana na kwa kujihamasisha yenyewe inaendelea kuepeleka huduma hii na tutahakikisha inamfikia kila mwananchi anayehitaji kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto.

Na. 71

**Serikali Kujenga Minara ya Simu Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano ya simu katika Jimbo la Lushoto?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi Andrea Mathew Kundo, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetekeleza miradi ya ujenzi wa

minara ya mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali Wilaya ya Lushoto. Mpaka sasa kuna miradi 16 ya ujenzi wa minara katika Wilaya ya Lushoto katika kata 15 ambapo tayari miradi 8 imekamilika na miradi mingine 8 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo iko katika Kata za Baga, Kwai, Kwekanga, Malibwi, Malindi, Manolo, Mayo, Mbaramo, Mgwashi, Mlola, Mponde, Rangwi, Shume, Ubiri na Vuga. Miradi ya ujenzi wa minara katika Kata za Kwekanga, Kwai, Malindi, Manolo, Mbaramo, Mayo, Mponde na Mlola imekamilika na tayari inatoa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa minara ya mawasiliano unaendelea katika Kata za Shume, Ubiri, Rangwi, Mgwashi, Vuga, Baga, Kwai na Malibwi. Ujenzi wa minara hii utakamilika mwezi Disemba 2021. Aidha, Kata zilizobaki Mfuko utazifanyia tathmini na zitaingizwa katika zabuni zijazo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shikilindi, una swali la nyongeza nakuruhusu.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri, kwa kweli nimehakikisha mwenyewe kwamba kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama unavyojua jiografia ya Wilaya ya Lushoto ni ya milima na mabonde ambayo husababisha kutopata huduma katika maeneo mbalimbali hasa Makanya, Mavului, Mbwei na maeneo mengine ya Mazumbai. Je, ni lini sasa Serikali itaenda kujenga minara ile ili kuondoa kadhia wanayoipata wananchi wa Wilaya ya Lushoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Wilaya ya Lushoto ina changamoto ya usikivu wa Radio ya Taifa yaani *TBC* na hili suala nilikuwa naliongelea mara kwa mara lakini mpaka leo hii hakuna majibu yoyote wala hakuna mnara wowote uliojengwa. Je, ni lini Serikali itaenda kujenga minara ya habari ndani ya Wilaya ya Lushoto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ile dozi ya Shekilindi bado inaendelea, kwa hiyo, tusisahau hasa kipindi hiki. *(Kicheko)*

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Andrea Mathew Kundo, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo Serikali inazichukua kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwanza kabisa ni kujiridhisha na ukubwa wa tatizo wa eneo husika. Ukubwa huo unaweza ukategemea na tatizo lenyewe, inawezekana katika maeneo fulani mawasiliano hakuna kabisa; maeneo mengine mawasiliano ni hafifu; lakini kuna maeneo mengine ambapo unakuta kwamba mawasiliano yako hapa hayako hapa; kunakuwa na *dark sport* za kutosha. Sasa Serikali inapofanya tathmini ni kujiridhisha pia na ukubwa wa tatizo ili kujua teknolojia gani ambayo tunaweza kwenda kuitumia pale ili kutatua tatizo la eneo husika kulingana na tathmini iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri tumekuwa na mawasiliano mazuri na amekuwa akiwapambania kweli wananchi wa Jimbo lake na sisi kama Serikali kwa sababu ndio jukumu letu na kupitia Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ibara ya 61(f) na (g) inaeleza kabisa kwamba ni jukumu la Serikali kwenda kufikisha mawasiliano kwa wananchi wote, kwa hiyo, suala lake litaangaliwa baada ya tathmini kufanyika.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la usikivu ni jambo lilelile ambalo pia kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA)* wanaendelea na kufanya tathmini katika maeneo yote pamoja na maeneo ya mipakani kuhakikisha kwamba palipo na changamoto ya usikivu basi Serikali inafikisha mawasiliano katika maeneo husika.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendela na Viwanda na Biashara na swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Na. 72

**Wananchi Rungwe Kulazimishwa Kuuza Chai na Maziwa kwa Mnunuzi Mmoja**

**MHE. SOPHIA H. MWAKANGENDA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini wananchi wa Wilaya ya Rungwe wanalazimishwa kuuza chai na maziwa kwa mnunuzi mmoja hali inayosababisha mnunuzi kupanga bei kitu ambacho ni kinyume na Sera ya Ushindani wa Biashara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakangenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003, uwepo wa mnunuzi mmoja katika soko siyo kosa, kosa ni endapo mnunuzi huyo atatumia nguvu ya hodhi ya soko aliyonayo katika kufupisha ushindani kwa kuzuia washindani wengine waliopo sokoni kufanya biashara. Kufifisha ushindani kwa kuwaondoa washindani wengine waliopo sokoni na kufifisha ushindani

kwa kuzuia makampuni au watu wengine kuingia kwenye soko husika.

Mheshimiwa Spika, iwapo itathibitika kuwa kuna kosa la kupanga bei ya huduma au bidhaa Tume ya Ushindani kwa maana ya *FCC* kuchukua hatua kwa kutumia Kifungu Namba 9 cha Sheria ya Ushindani. Kwa mujibu wa Kifungu hiki ili kosa husika lifanyike ni lazima kuwe na washindani katika soko, ambapo washindani hawa hukutana na kupanga bei ya bidhaa au huduma wanayotoa au kupanga kiasi cha kuzalisha au kugoma kusambaza bidhaa na huduma husika au kupanga zabuni.

Mheshimiwa Spika, hivyo Wizara kupitia *FCC* inafanya uchunguzi wa suala hili ili kubaini uwezekano wa kuwepo kwa uvunjifu wa Sheria ya Ushindani. Katika hatua za awali za uchunguzi *FCC* imeshawasiliana na Bodi ya Chai Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania na Ofisi ya Katibu Tawala, Mkoa wa Mbeya ili kupata taarifa muhimu kwa ajili ya kujiridhisha kuhusu changamoto hii katika soko la chai na maziwa Wilayani Rungwe. Ikiwa itabainika kuwa kuna uvunjifu wa sheria ya ushindani, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, nipende kutumia fursa hii kuwajulisha wafanyabiashara wote nchini kuzingatia sheria zilizowekwa ili kuwa na ushindani wa haki katika soko.

**SPIKA:** Hili nalo jibu refu sana.

Mheshimiwa Suma Fyandomo upo, yaani huko Rungwe chai na maziwa anakunywa mtu mmoja tu. Swali lake Mheshimiwa Sophia linasema; je, ni kwa nini wananchi wa Wilaya ya Rungwe wanalazimishwa kuuza chai na maziwa kwa mnunuzi mmoja tu. Nikasema sasa si mnywe wengi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hebron Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kipekee nimshukuru Mkuu wa Wilaya mpya aliyekuja katika Wilaya ya Rungwe, jana ameweza kuwaita wadau wanaonunua zao la maziwa na kuhakikisha wanapatikana wengi na wala siyo mmoja tena.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; Serikali haioni kuna haja ya kuleta Sheria Namba 3 ya mwaka 1977 ambayo ilikuwa inataka wakulima wote wanakaa katika mfumo wa kijiji. Sasa inawafanya Bodi ya Chai ambao ndiyo watoaji wa leseni hawawapi wakulima mmoja, mmoja kwa maana mkulima wa chai aweze kwenda kukopa benki, aweze kujua ni chai yake amuuzie nani na amkatae nani, sheria hii inawabana. Sasa kwa nini Serikali isilete marekebisho ya Sheria hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mrajisi wa Ushirika Wilaya ya Rungwe na sijui wilaya zingine alianzisha ushirika mpya na kuondoa ushirika wa kwanza bila kuwahusisha wakulima. Serikali inasemaje kwa hilo japokuwa jibu la msingi amesema ameweka, anasimamia na anafuatilia. Serikali ifuatilie kwa kina juu ya wakulima hawa ambao wao wanajua wapo *RSTGA*, lakini leo kuna kitu kinaitwa RUBUTUKOJE, wakulima wameachwa njia panda. Naomba Serikali ifuatilie kwa ukaribu suala hili. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuwa bado nawaza RUBUTUKOJE ni lugha ya Kibunge au ni...

Mheshimiwa Silaoneka natumaini umemwelewa Mheshimiwa Mbunge. Majibu ya maswali hayo mawili. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana dada yangu kwa ufuatiliaji wa karibu kuhusiana na maendeleo ya wakulima wa chai na maziwa katika Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kama kuna maendeleo ambayo anayaona kupitia Mkuu wa Wilaya kama tulivyosema tayari tumeshaanza kulishughulikia hili, ili kupata taarifa maalum kama nivyosema kwenye jibu la msingi kupitia Tume yetu ya Ushindani *(FCC).* Kwa hiyo hilo analolisema kuhusiana na Sheria Na.3 ya mwaka 1977, basi tutaangalia hilo pia, lakini tukipata taarifa maalum kulingana na ambavyo tumeomba kwa maana ya utaratibu wa ununuzi, namna bei zinavyopangwa katika soko, lakini pia na majina ya wanunuzi ambao wanashiriki katika ununuzi wa chai na maziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mrajisi katika Vyama vya Ushirika, naomba nalo tulichukue kama Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, tutafuatilia ili tuone ni namna gani tutatatua changamoto ambayo inawakabili wakulima wa chai na maziwa katika Wilaya ya Rungwe. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Kwa sababu ya muda tuendelee na swali la Mheshimiwa Ali Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini kuelekea kwenye Wizara hii hii. Mheshimiwa Kassinge.

Na. 73

**Kuanza Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea – Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea katika Mji wa Kilwa Masoko kitakachotumia malighafi inayotokana na gesi asilia ya Songosongo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Matumizi ya Gesi Asilia kwa maana *Gas Utilization Master Plan* imepanga kutumia kiasi cha futi za ujazo trilioni 0.7 za gesi asilia kwa uzalishaji wa Mbolea. Utafiti unaonesha kuwa Tanzania ina kiasi cha akiba ya gesi asilia kilichogunduliwa na kuthibitishwa takribani futi za ujazo trilioni 57. Hazina hii ya gesi tuliyonayo kwa sasa katika visima vyetu vya gesi asilia inatosha kwa matumizi ya viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na kiwanda cha mbolea kwa kutumia malighafi ya Gesi Asilia. Hivyo, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* na *TPDC,* Tume imeendelea na juhudi za kupata wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea. Hapo awali Serikali iliwahi kufanya majadiliano na kampuni ya *Ferrostaal* na *Helm* kutoka Ujerumani. Serikali imeendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wengine akiwemo Dangote, Elsewedy kutoka Misri na Minjingu *Mines Limited* ambao wameonesha nia ya kufanya uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC), TPDC*, *PURA*, *EWURA* na Wizara inaharakisha kukamilisha majadiliano hayo na hatimaye kupata wawekezaji wenye uwezo wa kujenga viwanda vya mbolea kwa lengo la kumaliza tatizo kubwa la uagizaji mbolea nje ya nchi. Pindi majadiliano hayo yatakapokamilika ni imani ya Serikali kuwa ujenzi wa kiwanda hicho utaanza mara moja. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge nimekuona.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, gesi asilia ninayozungumzia kwenye swali langu la msingi ni ile gesi ya Songosongo na eneo mahsusi ambalo nimeulizia ujenzi wa

kiwanda ni katika Mji wa Kilwa Masoko, ambapo kimsingi tayari eneo la kutosha lipatalo ekari 400 lilishatengwa tangu mwaka 1989, lakini pia *TPDC* ilishalipa fidia ya eneo hili na ni eneo ambalo lipo huru na lina hati. Je, Serikali inathibitisha kupitia Bunge lako Tukufu kwamba kiwanda hiki cha mbolea kitajengwa mahsusi Kilwa Masoko na si kwingineko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kwa ridhaa yako kuambatana nami baada ya Bunge hili kwenda Kilwa ili akajionee maendeleo na maandalizi ya eneo la kutosha la kiwanda hiki? Ikiwa ni pamoja na uwepo wa bandari, uwepo wa eneo la kutosha kwa ajili ya upanuzi wa bandari, lakini pia uwepo wa eneo la kutosha kwa ajili ya kutolewa malighafi hii, lakini pia atapata fursa ya kujionea Kiwanda cha Maji cha Swahili *Water* pale Nangurukuru. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge nitamruhusu Naibu Waziri baada ya kupata uhakika wako kwamba atarudi salama Kilwa, vinginevyo itakuwa vigumu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali, upo tayari kwenda Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nipo tayari.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba tunataka kuona tunatumia malighafi iliyopo ya gesi asilia na kimsingi kama alivyosema *TPDC* tayari walishakuwa na eneo na hata wawekezaji hawa tunaojadiliana nao wengi tunataka waeleke kujenga katika Mji huu wa Kilwa Masoko ambapo ndipo malighafi inatoka.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana kwa juhudi zake za kufuatilia suala hili na kama nilivyosema mwanzoni

nitaambatana naye katika maombi yake ili tuweze kupitia kuona namna gani tunajionea, lakini pia kuona na viwanda vingine ambavyo vimewekeza katika Mkoa wa Lindi hususani Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Ndulane, swali fupi la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na suala la Kiwanda cha Mbolea katika Wilaya ya Kilwa. Ningependa kwa sababu kuna sehemu tayari ameshanifilisi mzungumzaji wa kwanza wa swali, ningeomba tu labda atakapokuja Mheshimiwa Waziri katika Wilaya yetu ya Kilwa kwa ajili ya kuzungumzia suala la kiwanda hiki, aje na majibu ya kwa nini mradi huu umechelewa kwa sababu mradi huu ni wa mwaka 1996. Kwa hiyo, ningeomba aje na majibu ya kuwaeleza wananchi ni kwa nini umechelewa, sasa ni miaka 15 tangu ulipobuniwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hilo Mheshimiwa Naibu Waziri utakapoenda basi uende na majibu, ndiyo umetakiwa kufanya hivyo.

Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo.

Na. 74

**Kuwakinga Akinamama Wanaochenjua Dhahabu kwa Kutumia Zebaki**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda Akinamama wanaochenjua dhahabu dhidi ya sumu ya zebaki ambayo ina madhara makubwa kiafya?

**SPIKA:** Nilikuwa naruka swali, Mheshimiwa Ester Bulaya ameniwahi, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali katika kuwakinga akinamama wanaochenjua dhahabu kwa kutumia kemikali ya zebaki ni kuendelea kutoa elimu ya uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini pamoja na madhara ya kemikali hiyo kwa wachimbaji wadogo. Elimu hiyo inatolewa na Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(GST)*, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango huu, Serikali kupitia Wizara ya Madini imejenga Vituo vitatu (3) vya Mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Itumbi (Chunya), Lwamgasa (Geita) na Katente (Bukombe) ambayo yameonekana kuwa na wachimbaji wadogo wengi zaidi. Teknolojia ya uchenjuaji inayotumika katika vituo hivyo ni *Carbon–in–Pulp (CIP)* ambayo ni mbadala wa matumizi ya kemikali ya zebaki.

Mheshimiwa Spika, zipo kampuni tayari za uchimbaji mdogo ambazo zimeanza kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia ya *shaking table,* meza inakuwa itatikiswa kufuatia *gravity* ambayo haitumi zebaki wala kemikali yoyote. Teknolojia hii Wizara inaendelea kuifanyia majaribio ili kuona tija yake kabla ya kuanza kuitumia kwa wachimbaji wote hasa wale wachimbaji wadogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester, nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Mbali tu na tatizo la kemikali ya zebaki, lakini wachimbaji wadogo wamekuwa na tatizo kubwa sana la mitaji wakiwemo wachimbaji la Nyamongo Mkoa wa Mara. Ni lini sasa Serikali watawawezesha wachimbaji wadogo wa Nyamongo hasa vijana na akinamama ili waweze kuchimba vizuri dhahabu zao.

Mheshimiwa Spika**,** swali langu la pili kuhusiana na kemikali zinazodhuru wananchi, si tu kwa wachimbaji wadogo mbali na kwa wananchi wanaozunguka migodi. Sasa wananchi wa Nyamongo wameathirika sana na mara nyingi Serikali imesema italipa fidia, ni lini sasa itawafidia wananchi ambao wameathirika na kemikali zinazotoka migodini?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Profesa Shukrani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mitaji Serikali kupitia Wizara ya Madini imefanya lile linalowezekana kuhusisha benki zetu za ndani ambazo zimehiari kutoa mitaji kwa ajili ya wachimbaji wetu wadogo na kwa taarifa mwezi wa Sita Mheshimiwa Waziri wa Madini alizindua *NMB Mining Club* ambapo wateja wachimbaji wadogo wanaweza wakaenda pale na wakakopeshwa.

Mheshimiwa Spika, pia benki zetu zingine za ndani zimehiari tayari na tayari tumeona kwamba wanashiriki katika shughuli za kuwakopesha wachimbaji wadogo. Ambacho tumewaasa wachimbaji wadogo ni kwamba kabla ya kwenda benki awe na leseni halali, inayotambulika na Tume ya Madini, lakini pia awe basi na takwimu za kazi anazozifanya ionekane kwamba unaonekana ukizalisha, ukiuza unapata faida benki wamehiari kutoa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo limefanyiwa kazi kwa namna hiyo na wachimbaji wadogo wameanza kupata matunda. Pia kwa taarifa benki zetu za ndani zimekwenda mbali zaidi hadi kutoa fedha kwa ajili ya miradi mikubwa. Kwa hiyo tunadhani kwamba, hiyo ni hatua na suala la mitaji limeendelea kushughulikiwa halimradi wachimbaji wetu wadogo waweze kutoa ushirikiano kwa jinsi hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira yanayozunguka migodi. Ni kweli kwamba inapokuja kwenye mgodi ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja, Serikali imeendelea kufanya hatua, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba hakuna tena maji yanayotiririshwa katika maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, limeendelea kushughulikiwa na timu yetu ya Wizara ya Madini pamoja na *NEMC* pamoja na watu wa Wizara ya Maji, wamekuwa wakishirikiana katika kufanya ukaguzi kuhakikisha kwamba hakuna uchafu tena unaoendelea kutiririshwa kutoka katika migodi.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia pia limeendelea kufanyiwa kazi na yule Mthaminishaji Mkuu wa Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Tunahamia Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga.

Na. 75

**Sera ya Uvumbuzi**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuleta Sera ya Ubunifu *(Innovation Policy)* ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Juma Omary Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jidith Salvio Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa ubunifu na teknolojia kama nyenzo muhimu katika kurahisisha maisha yetu kwa kuokoa muda katika utendaji kazi, kuongeza tija na ubora katika uzalishaji wa bidhaa na hata utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa ubunifu, mwaka 2012 hadi 2014 Serikali ilifanya mapitio ya Mfumo wa Ubunifu nchini ili kuutambua na kuainisha upungufu uliopo. Mapitio hayo yalitoa mapendekezo ya namna ya kuboresha mfumo huo ili kuleta tija katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Aidha, moja ya mapendekezo hayo ni kuwa na sera yenye kuchochea ukuaji wa ubunifu nchini kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hatukuwa na Sera maalum ya Ubunifu nchini na kwa kuwa, masuala ya ubunifu yanaenda sambamba na sayansi na teknolojia, kwa sasa Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 kwa lengo la kuiboresha ili ijumuishe masuala ya ubunifu. Aidha, maboresho hayo yanalenga kuifanya sera iendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia nchini, kikanda na kimataifa. Hivyo, katika mapitio hayo sehemu ya ubunifu itapewa uzito unaostahili. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith nimekuona.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba Sera yetu ya Sayansi na Teknolojia ni ya muda mrefu, ya miaka 25

nyuma, lakini vilevile kutokana na suala kwamba mapitio ya sera hii ili yaweze kuleta tija kwenye ubunifu yamekuwa yakichukua muda mrefu, tangu 2012, jambo linalosababisha programu za ubunifu chini ya *COSTECH* kutokutengewa fungu na kutegemea zaidi ufadhili na hivyo kukosesha vijana fursa nyingi zinazotokana na ubunifu: Je, Serikali haiwezi kutuambia ukomo wa muda wa mapitio haya ya sera ya kwamba yatakamilika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu tumeambiwa maboresho yamekuwa yanafanyika toka 2012 lakini hadi leo hayajafanyiwa kazi. Tunaomba Wizara ituambie ukomo wa muda wa kufanyia maboresho ili programu za ubunifu ziweze kuwa na tija kwa vijana wa Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Wizara imekuwa ikitenga fedha katika kila bajeti kwa lengo la kuhakikisha kwamba eneo hili la ubunifu linafanyiwa kazi sawa sawa. Nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara imetengeneza mwongozo wa mwaka 2018. Vilevile mwongozo huu tunaendelea kuuboresha mwaka huu, tena tunaendelea kuupitia upya ili kuweka mwongozo huu sawa sawa, nimtoe wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, pia anataka kujua kwamba ni lini Serikali itakamilisha utungaji huu au mapitio haya ya sera? Ndani ya mwaka huu wa fedha tutalifanya hilo na kuhakikisha jambo hili linakaa sawa sawa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa

Norah Mzeru uliza swali lako. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Londo.

Na. 76

**Uhaba wa Mashine za *Incubator* Nchini**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mashine za *incubator* za kutosha nchini ili kuzuia vifo vya watoto?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Afya mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru kwa kuwa na utashi wa kuangalia afya za watoto wachanga katika Taifa letu kama sehemu ya changamoto tuliyonayo sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali lake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kifaa cha *incubator* hutumika kuwasaidia watoto wachanga waliozaliwa kabla ya wakati au wenye uzito pungufu ili kuwapatia joto na kuzuia wasipoteze maisha. Hadi sasa tuna *incubators* 214 nchi nzima kwenye hospitali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tafiti zimeonesha kuna changamoto nyingi sana za kutumia *incubators* kuliko faida

zenyewe. *Incubators* zimesababisha kusambaa kwa magonjwa kutoka mtoto mmoja kwenda kwa mwingine atakayefuatia kulazwa hapo. Aidha, hakuna ukaribu wa mama aliyejifungua na mtoto aliyewekwa kwenye *incubator.*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya *incubator* katika mazingira ambayo umeme siyo wa uhakika nayo inakuwa changamoto. Hivyo, katika mazingira hayo, *incubator* inaweza kuwa chanzo cha uambukizo na vifo badala ya kusaidia. Hata hivyo *incubators* chache zilizopo zinatumika kwa ajili ya watoto waliozaliwa na uzito pungufu sana *(extreme low birth weight)* kwa kuzingatia kanuni za usafi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Wizara inasisitiza kuwa kila hospitali ianzishe vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga ili kuendana na mwongozo wa Kitaifa wa Matibabu ya Watoto Wachanga. Vyumba hivyo ni chumba cha huduma ya *Mama Kangaroo,* yaani mtoto anakaa na mama kifuani kwake muda mwingi kwa watoto waliozaliwa na uzito pungufu, lakini pia na chumba cha matibabu ya mtoto mchanga mgonjwa. Kufikia Julai, 2021, jumla ya hospitali 159 zilishaanzisha vyumba hivyo na kazi inaendelea kwenye hospitali nyingine. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Londo, nimekuona umesimama.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna uchache ama upungufu mkubwa wa hizi mashine za *incubator;* na anasema kwamba hakuna utafiti wa kisayansi ambao unaonesha kwamba zinaweza kusaidia maisha ya Watoto; je, yuko tayari kuleta utafiti wa kisayansi kuelezea mahusiano ya vifo vya watoto njiti kwa kukosa huduma hasa kwa kutokuwepo kwa hizi *incubators?*

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kama wametambua kwamba *Kangaroo Mother Care* imekuwa ni njia mujarabu

katika kuokoa maisha ya watoto, ni juhudi gani za Serikali zimechukuliwa kuhakikisha elimu hii inafika vijijini ili kuokoa maisha ya watoto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Afya, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Londo kwa maswali yako mawili mazuri kabisa. Napenda kujibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *scientific data* au *scientific evidence* kuhusu eneo hili zipo na sayansi huwa inaendelea kufuatilia mambo mbalimbali kadri muda unavyokwenda na ku-*adapt* marekebisho ili kuboresha. Hivyo, kwa ridhaa yako, kama tutapata fursa tunaweza tukawasilisha kupitia Kamati ya Huduma za Jamii baadaye ikafika Bungeni, hizi tafiti mbalimbali zilizofikia, tukafanya *adjustment* siyo tu Tanzania, dunia nzima, kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu kufika vijijini, tayari tulishatoa mwongozo wa maboresho eneo hili, upo; na kupitia Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya tutahakikisha tunasogeza elimu hii kwenye jamii ili waweze kuona umuhimu wa kukaa na mtoto kifuani kwao, hasa anapokuwa amezaliwa na uzito pungufu sana tuendelee kuokoa maisha. Hii imeonesha kwenye *data* zetu za mwaka 2018 mpaka 2020 vifo vimeendelea kupungua kutoka 11,524 mpaka 8,190. Ni katika mikakati hii ambayo tumeichukua ya kuhakikisha kwamba tunaokoa maisha ya watoto.

**SPIKA:** Kule Msekwa nimekuona sijui kama ni Mheshimiwa Mwanaisha au nani? Endelea kuuliza swali lako.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya swali la nyongeza; na nitauliza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mashine ya kupima kiwango cha usikivu kwa watoto mara wanapozaliwa *(auditory brainstem response test)* ipo Muhimbili peke yake hapa nchini. Hospitali zote za rufaa nchini hazina kifaa hiki, sasa ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kuhudumia wanafunzi wenye ububu na uziwi na kuendesha kwa gharama kubwa shule hizo: Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba mashine hizo zinapatikana na inakuwa ni lazima kwa kila mtoto anayezaliwa kupimwa kiwango chake cha usikivu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa Mheshimiwa Daktari kutoka kwa Mhandisi tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa swali zuri la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha, Mbunge, kuhusu masuala ya kuwapima watoto kiwango cha usikivu pale wanapozaliwa, kwamba ni gharama sana kwa sababu ni hadi uende Muhimbili. Nakubaliana kabisa na ninampongeza kwa kuliona hili.

Mheshimiwa Spika, niweze tu kusema haja ipo na ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha miundombinu ya hospitali za kibingwa, hasa za kanda ili kusogeza siyo tu vifaa, pamoja na hawa wataalam wanaotakiwa kupima. Tuna hospitali yetu ya Mtwara imeshafikia asilimia 95, tuna ya Chato inakamilika, pia tuna Meta Mbeya inakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni pendekezo la msingi na ni hoja ya msingi sana. Katika bajeti inayokuja tutaanza kuona kadri tunavyozindua, hata hawa wataalam wanaoshughulika na masuala ya usikivu, tuendelee kuwapa *training* tuwasogeze kwenye hospitali hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Nashukuru sana. Bado tuko Wizara ya Afya, swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, tafadhali.

Na. 77

**Kuwapatia Wazee Wasiojiweza Vitambulisho kwa Ajili ya Matibabu**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani suala la kuwapatia wazee wasiojiweza vitambulisho kwa ajili ya kupata matibabu bure limetekelezwa kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko na wewe Mheshimiwa Waziri wa Afya, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge, kwa swali lake zuri na kwa mapenzi yake kwa wazee wetu ambapo nasi ni wazee watarajiwa; kwamba wanaendeleaje hawa wazee wasiojiweza kupata vitambulisho vya kupata matibabu bure, limetekelezwaje.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwatambua wazee na kuwapatia vitambulisho linaendeshwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote hapa nchini. Hadi kufikia Desemba, 2020 jumla ya wazee 2,344,747 wametambuliwa sawa na asilimia 87 ya makadirio ya wazee wote nchini. Kati yao wanaume ni 1,092,310 na wanawake ni 1,252,437. Aidha, wazee wasio na uwezo 1,087,008 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bure na wazee 856,052 wamepatiwa kadi za matibabu za Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa *(iCHF).*

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kuhakikisha kuwa makundi yote ikiwemo wazee wanapata huduma bila kuwa na kikwazo cha ugharamiaji, Serikali ipo kwenye hatua ya

kuandaa Muswada wa Bima kwa wote utakaowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu ili kuundiwa sheria. Tunatarajia kwa hapa tulipofikia ni Novemba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia nimekuona.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na kutokana na hayo basi swali langu la kwanza litakuwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zake na kwa jinsi hali halisi ilivyo, zipo Halmashauri ambazo hazijakamilisha zoezi hili na ni kwa madai kwamba hazina mapato ya kutosha. Sasa je, Serikali inatoa tamko gani kwa zile Halmashauri ambazo hazina fedha za kutosha kukamilisha zoezi la utambuzi na la utoaji vitambulisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba lipo tatizo wazee wanapofika hospitalini wanaandikiwa dawa na kuambiwa waende kununua katika maduka ya dawa kwa madai kwamba katika kituo husika hakuna dawa: Je, Serikali inatoa maelezo gani pale ambapo wazee wanakuwa wakiambiwa wakanunue dawa ilhali wanastahili kupata matibabu ya bure? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge Anastazia kwa kuendelea kuwatetea na kuwapambania wazee. Naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kweli zipo Halmashauri ambazo zinashindwa kutimiza hili, kati yake zipo ambazo hawatimizi tu mpaka uwafuatilie sana na wapo wengine ambao kwa kweli uwezo wao unakuwa mdogo sana. Niseme kwenye

bajeti yetu hii iliyopita, nilishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kupitisha ile bajeti yetu ya shilingi bilioni 149 ambazo tunatarajia kwenye muswada huu wa sheria zitakwenda kuhudumia zile nyumba zote wakiwemo wazee ambao watakuwa wamebainika kwamba hawana uwezo kabisa. Kwa hiyo, tunatarajia kumaliza kabisa hili suala la wazee hawa wasio na uwezo kabisa ili wawe *covered* kupitia Mpango wetu wa Bima ya Afya Kwa Wote tunaotarajia kwenda kuuchukua.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tumekuwa na vikao vya kwenye mtandao pamoja na Mtandao wa Wazee nchi nzima, kila Jumamosi; tumeanza hiyo sera, “Jumamosi Zungumza na Wazee.” Tunafanya hivi vikao kujadili hizi changamoto. Wiki iliyopita tumekubaliana kwamba; awali iliagizwa asilimia sita ya bajeti tunayopanga lazima dawa zake ziende kwa wazee. Kwa hiyo, hata sasa hivi Serikali imefanya uamuzi wa kurudisha kupitia Hazina ile fedha ya Hospitali kwa mfano za Mikoa iliyokuwa inaenda moja kwa moja *MSD,* ili dawa zinapokosekana, zinunuliwe huko kwenye hospitali. Asilimia sita ya ile fedha ndiyo itumike kununua hizo dawa za wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kamati za Maamuzi kwenye Vikao vya Bodi za hizi hospitali zetu, tumeona kwamba tuweke hata mwakilishi wa wazee awe anahakikisha kwamba anatetea ile hoja yake pale. Hii ni mikakati ya kufanya kwamba wazee wawe na sauti katika vikao vya maamuzi vya *management* za hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeanza mkakati wa kila hospitali; mnawaona wale wamevaa nguo za *“Mpishe Mzee Apate Huduma Kwanza.”* Hawa nao wanachukua takwimu za kujua mzee gani amekwenda kituoni, ameondoka bila dawa ili *Medical Officer in Charge* ahusike kuhakikisha mzee huyu anapata dawa kwa taratibu hizi za kuweka bajeti ya dawa pembeni yao. Ahsante.

**SPIKA:** Hii sera ina taabu. Msisitizo wa Sera hi ya Chama cha Mapinduzi ni wazee wasiojiweza, siyo mzee ambaye

ameoa kigori miezi sita iliyopita, naye anahusika na hili, hapana. Ni wazee wasiojiweza. Hili swali Waheshimiwa Wabunge mtaulizwa sana huko, kwa hiyo, ni vizuri kulielewa vizuri. Ni wazee wasiojiweza. Kwa hiyo, hata hizo kamati ziwe na wazee wasiojiweza. Maana kila unapoenda unaulizwa, sisi wazee mbona imesemekana dawa bure? Haihusishi wazee wote.

Kuna wale wazee wengine nao wamo katika ma...; kama yule mzee wa Yanga yule, sasa yule si lazima alipe tu nanii! Juzi kakimbia uwanjani kule ana nguvu kabisa. Simtaji jina. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka.

Na. 78

**Hitaji la Gari Kituo cha Polisi Chwaka**

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE** aliuliza: -

Je, ni lini Kituo cha Polisi cha Chwaka kitapatiwa gari ili kutimiza majukumu yake kwa ufanisi zaidi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Simbachawene, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linatambua uhitaji wa magari katika Kituo cha Polisi cha Chwaka kama nyenzo ya kutendea kazi. Kupitia mkataba wake na Kampuni ya Ashok Leyland Jeshi la Polisi linategemea kupokea magari 369 toka Serikalini. Pindi magari hayo yatakapofika, kipaumbele kitatolewa kwa maeneo yote ya vituo vya polisi

ambavyo havina magari kikiwemo pia Kituo cha Polisi Chwaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, swali la nyongeza.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Chwaka lina kituo kingine kidogo cha Polisi kilichopo Jozani: Je, Serikali haioni kwamba kuna sababu ya kukipelekea usafiri angalau wa ma-*ring* mawili? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunayo changamoto kubwa sana katika vituo vingi vya Polisi, shida kubwa ikiwa usafiri. Yapo maeneo hata ya wilaya nzima kabisa ikiwemo Wilaya ya Kongwa, gari pale ni mbovu na iko moja.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar kule vituo hivi viko karibu karibu sana. Katika kugawa magari haya tutaangalia sana hata ukubwa wa jiografia, tutaangalia pia maeneo yenye changamoto kubwa zaidi hasa ya mipakani. Vile vile niseme tu, kwa maeneo ambayo vituo viko karibu karibu, huduma ile wanaweza kuipata katika wilaya, kwa sababu *setup* yetu katika vituo vya Polisi, bado ni ya kiwilaya zaidi, siyo vituo vile vidogo vidogo. Kwa hiyo, niseme tu tutakwenda kuangalia tuone umbali kati ya kituo hiki anachokisema na kituo cha wilaya halafu tuone kama hilo analolisema litawezekana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Msekwa kule, Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa changamoto ya wananchi wa Chwaka inafanana kabisa na ya wananchi wa Jimbo la Mlimba, kwenye Kituo cha Polisi cha Mlimba: Je, Mheshimiwa Waziri haoni hayo magari yatakapofika katika mpango wake, basi aweze kukumbuka pia na Kituo hiki cha Polisi Mlimba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu kwamba changamoto hii, kama nilivyosema, iko katika vituo vingi. Naamini hata Kituo cha Polisi cha Mlimba ambacho kina hadhi ya Kituo cha Wilaya kina changamoto kubwa sana ya gari. Kwa kawaida hata angalau magari yakipungua sanakwenye Kituo cha Wilaya, yanapaswa kuwa angalau matatu au manne, lakini pale kuna gari moja na lingine bovu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yenye changamoto za miundombinu, changamoto za shughuli za uzalishaji ndiyo zitapewa kipaumbele magari haya yatakapofika.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Maliasili na Utalii, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, tafadhali.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa niamba ya wananchi wa Vijiji 11 vinavyozunguka Pori la Akiba, Mkungunero, swali lao Na. 79 lipate majibu ya Serikali.

Na. 79

**Tatizo la Mapori ya Hifadhi na Vijiji Vinavyozunguka Mapori Hayo**

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI** aliuliza: -

(a) Je, ni lini Serikali itaelekeza kwa wananchi maamuzi ya Timu ya Mawaziri iliyozunguka kwenye maeneo yenye migogoro kati ya wananchi na mapori ya hifadhi?

(b) Je, ni lini Serikali kwa kushirikiana na wananchi itaweka mipaka kati ya mapori ya hifadhi na vijiji vinavyoyazunguka ili kupunguza migogoro iliyopo na kuwezesha wananchi kufanya shughuli za kiuchumi bila usumbufu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondoa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maamuzi ya Baraza la Mawaziri, Serikali imeandaa mpango kazi kwa ajili ya kuwaeleza wananchi juu ya uamuzi wa Serikali kuhusu migogoro kati ya wananchi na hifadhi. Katika kutekeleza mpango kazi huo, timu ya Mawaziri wa Kisekta itapita katika mikoa husika kwa lengo la kutoa elimu na ufafanuzi kwa viongozi wa mikoa pamoja na wilaya.

Zoezi hilo litaenda sambamba na timu ya watalaam itakayojumuisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Uongozi wa Mikoa, Wilaya na Vijiji.

(b) Mheshimiwa Spika, zoezi la uwekaji wa mipaka kwenye maeneo yote yenye migogoro litafanywa na timu ya wataalam kutoka katika sekta za Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Timu hii, itapita katika maeneo yote ili kufanya tathmini, uhakiki na kuweka mipaka kulingana na uamuzi wa Serikali. Aidha, katika zoezi hilo wananchi watashirikishwa ili kuondoa uwezekano wa kujitokeza migogoro mingine. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Naomba niulize swali moja tu la nyongeza nalo ni hili lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utekelezaji wa maamuzi wa maelekezo na kazi nzuri iliyofanywa na mawaziri hawa nane bado hayajafanyika, na kwa kuwa bado maelekezo yaliyotolewa wakati timu hiyo inaundwa kwamba wananchi waachwe maeneo yao wakiendelea na shughuli za maendeleo bado halijavunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa je, ni kwa nini wananchi wa vijiji 11 wanavyozunguka pori la Akiba Mkungunero bado mifugo yao inakamatwa? Na wananchi bado wanapigwa na maaskari hawa wakiwa kwenye maeneo yao hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi nimekuona, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ashantu na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Kaimu Naibu Waziri wa Maliasili nilitaka nimpe maelezo Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepata maelekezo

maalum ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu, kwamba sasa tuunde timu kwenda kufanya uhakiki wa maeneo hayo kama Mkungunero ambalo anahangaika nalo na mimi nalijua sana. Na ilikuwa lazima Mheshimiwa Rais mwenyewe atoe idhini na maelekezo hayo na ametoa maelekezo ya huruma kabisa kwamba pamoja na maelekezo yale ya awali, lakini nendeni mkafanye uhakiki kabisa ili tuone namna ya kumaliza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kumhakikishia timu ya watalaam itakuja Mkungunero mwezi wa kumi na maeneo mengine yenye migogoro kama hii kwa sababu inajulikana. Tumeagizwa tufanye kazi hiyo ya uhakiki ili kukomesha kabisa migogoro hii kwa kadri itakavyowezekana. Uamuzi umetolewa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutakuja kushirikiana pamoja na wewe na viongozi wengine na viongozi wa mkoa katika kuhakikisha mambo haya yanakwisha.

Mheshimiwa Spika, tunajua yapo mengi huyu ameuliza katika mengi mengine na wewe hata leo uliunda kamati fulani niende kule nimewaambia kidogo, lakini nataka kukuhakikishia kwamba haya maneno Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo maalumu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa maelezo haya mazuri, lakini sasa wakati wananchi wanaendelea kusubiri hii kauli ya njema sana ya Mheshimiwa Rais. Nini kauli ya Serikali kwa maafisa hawa wanyamapori ambao wanaendelea kunyanyasa wananchi na kukamata mifugo yao kwa kipindi hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, tafadhali majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, narudia tena kwamba Mheshimiwa Rais amesema kazi iendelee. Anatambua

uamuzi uliotolewa na Awamu ya Tano na yeye amesisitiza kwamba wananchi wote waliopo kwenye maeneo yao wasiondolewe katika vile vijiji 920, uamuzi huo upo vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ametupa kazi ya ziada kwenda kufanya uhakiki wa hali halisi iliopo. Kwa hiyo, ningeomba na wananchi nao wasitumie vibaya uamuzi huu wa Serikali wakafiri kwamba basi wasiondolewe maana yake ni kujipanua wanavyotaka. Tafadhali wakae kama walivyokuwa ili kazi hii ya uhakiki ije iwatendee haki kwa sababu hii pande mbili kuna upande huo wa wananchi, lakini upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wengine tulivyotoka na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kule Katavi, baada ya kutoa tamko lile pale watu waliingia kwenye Msitu wa Mbuga ya Katavi. Kwa hiyo, na wananchi nao wasubiri nia njema ya Rais wa Awamu ya Sita ni kutenda haki. Tufanye uhakiki kama alivyoagiza halafu uamuzi utatolewa.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, jambo hilo litatekelezwa, lakini wakati huo huo kazi iendelee maana yake uamuzi ule, ule uliotolewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita amerudia maagizo yale yale kwamba nataka wananchi wote waliopo kwenye vile vijiji 920 wasiondolewe. Kwa hiyo, nadhani hakuna mtu wa Serikali anayewaondoa watu katika maeneo yale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa muda mrefu Wabunge walikuwa wakisubiri taarifa ile ya mawaziri nane, tunajua ni taarifa ya Serikali sijui kama imefikia kiwango cha Wabunge kuweza kujua angalau kilichomo au bado ni...Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana leo asubuhi uliunda kamati mbili twende tukawasilishe ile taarifa, lakini nimewaomba rasmi kwamba jambo hilo ndilo ambalo

Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo mwezi huu uliopita. Kwa hiyo, nikawaomba radhi kwamba kwa sasa hatuna jipya watusubiri kidogo kazi hii ya kwenda kufanya uhakiki wa kina wa leo kwa sababu maamuzi haya yametolewa miaka mitatu, lakini hali ya leo ni tofauti na yeye ni Rais wa Awamu wa Sita amemetutuma mwezi uliopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimewaomba radhi kwamba kwa leo hatutatoa hiyo taarifa, lakini itakapokamilika huu uhakiki wa uandani ambao kwa vyovyote vile tukipita mikoani tutawakuta na Waheshimiwa Wabunge huko baada ya kukamilika hiyo kazi na Mheshimiwa Rais akitolea maamuzi tutakuja kuileta taarifa hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Jamani nilidhani inatosha, basi kwa sababu ya muda tu maswali hayo mawili yawe ya mwisho. Nimekuona Mheshimiwa Mwalimu na Mheshimiwa Musukuma atamalizia.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nataka kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miaka mitatu, minne iliyopita mawaziri nane hawa walipewa kazi ya kupita huko wilayani na vijijini kwa ajili ya kuhakiki mipaka na matatizo mengine kama hayo. Lakini baadhi ya wilaya kama Wilaya ya Songwe ilikuwa bado wakati huo ni wilaya mpya hatukufikiwa na timu ile na wale watalaamu na sasa hivi ukimuambia Mheshimiwa Waziri anasema kwamba tena wameambiwa waende wakahakiki, lakini najua tunaweza tukasahaulika tena na anasema watapita huko na wataona na Wabunge, lakini Wabunge wanaweza wasiwepo wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini siku nne ambazo zimebaki hapa tusipewe kazi Wabunge tuorodheshe vile vijiji ambavyo vina matatizo ya mipaka na mambo mengine ili angalau tumpe Waziri atakapokuwa anakwenda huko awe tayari na *feedback* ya Wabunge? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tulipoanza Bunge hili, nilileta maombi kwa Katibu wa Bunge kuuliza swali hili kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye anakero yake atuandikie, walioandika, wameandika. Nakupa ruksa Mheshimiwa Mulugo kama unayo nikabidhi tu, sisi tunapenda kuwa na hiyo *directory* ya migogoro hii ili itusaidie.

Mheshimiwa Spika, lakini hata utaratibu utakaokwenda tukienda mikoani tutakutana na viongozi wote kwa ujumla ili watuambie haya kwa sababu siyo kweli kwamba kamati hii ya watu nane ilipita kila mahali hapana. Tulienda maeneo machache, lakini tuli-*take stop* taarifa mbalimbali ya kamati mbalimbali ikiwemo Kamati ya Bunge mbalimbali zilizoundwa humu. Zilikuwa na taarifa nyingi sana ndiyo tumetumia zile taarifa kuchambua juu ya migogoro mbalimbali iliyopo, siyo kwamba sisi ndiyo tumegundua migogoro ilikuwepo katika nyaraka na tume mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanafikiri wanazo taarifa za ziada, ambazo wanafikiri tungependa kuzijua, ruksa tupo hapa tupatieni tu sisi tutaweka kwenye rekodi yetu siyo lazima iwe sisi kuna taarifa nyingine kama hizo za mipaka ya vijiji na vijiji siyo lazima sisi. Mamlaka zipo kule tutawaelekeza watafanya tu. Kwa hiyo, ni fursa kwa Waheshimiwa Wabunge wakati wowote kutupa hiyo kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Habari za vijiji na vijiji hizo tukazitatue kule, hapa tulete ile migogoro ile yenyewe kabisa. Mheshimiwa Musukuma nilikutaja wewe swali la mwisho kabisa kwa siku ya leo.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la mwisho.

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita ni kweli iliundwa timu ya mawaziri wanane na walizunguka kwenye wilaya baadhi ya wilaya na wilaya nyingi. Lakini, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ziara ile ya mawaziri imekuwa kama ni ya kificho ficho, yaani tunawasikia tu, walipita, walipita, yaani sehemu hata ambazo hazina umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa na sisi ndiyo tunaolalamikiwa kila siku tunakuja kuuliza haya maswali. Kwa nini Serikali au Waziri asiweke mpango mzuri, timu inapoenda kwa mfano Wilaya ya Geita tujulishwe Wabunge na sisi tushiriki kwenye kuonyesha ile mipaka ili kuondoa ile sintofahamu. Ni hayo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Japo Mheshimiwa Waziri alijibu, lakini ajibu tena swali hilo kwa kuweka msisitizo ili tuelewane. Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musukuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, timu yetu ilikuwa na hadidu za rejea, haikuwa kutembea tu, na kuchunguza kila kitu, tulikuwa tumepewa hadidu za rejea na mambo fulani za kushughulikia, ilikuwa ni migogoro maalumu yenye mwiingiliano kati ya hifadhi na wananchi na vijiji, kulikuwa na migogoro hiyo maalumu.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kufanya kazi hii nimesema hatukupita kila mahali kwa sababu tulikuwa tayari tuna taarifa, moja ya taarifa kubwa tuliyokuwa nayo ilikuwa migogoro ya wafugaji na wakulima ambayo ilikuwa ni Tume ya Bunge iliundwa hapa na Bunge lako Tukufu nayo tulitumia na tume nyingi nyingi na taarifa mbalimbali. Lakini tukawa tunataka kujiridhisha juu ya yale yaliyoandikwa kwa hiyo tulienda sehemu chache sana.

Mheshimiwa Spika, tunajua nchi hii kuna migogoro ya mipaka kati ya vijiji na vijiji ambayo si ngumu sana kusuluhisha.

Tumeagiza sana viongozi wa mikoa na wilaya kwa sababu mwenye mamlaka ya kuunda maeneo ya utawala ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuna kijiji kilichoanzishwa wala wilaya wala mkoa ambayo mipaka yake haikuandikwa kwenye *GN* ni suala la kwenda kusoma *GN* kwenye uwanda na kuamua mpaka upo wapi kwa sababu hawatakiwi kuunda mipaka ya utawala, mipaka ya utawala imeshaandikwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ipo migogoro mingi inayoendelea vijiji na vijiji kata kwa kata, sijui tarafa kwa tarafa ni uzembe tu. Tukishirikiana migogoro hii itaisha kwa sababu ina maandishi yake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma nataka kukuomba kama kuna mgogoro wa mpaka wa wilaya usisubiri ile tume, tuambie hizo ndiyo kazi zetu za kila siku.

Mheshimiwa Spika. kwa hiyo, tutenganishe kati ya ile kazi ya Tume na shughuli zetu za migogoro kila siku, shughuli kama kuna migogoro mingine mliyonayo Waheshimiwa Wabunge tupeni hizo ndiyo kazi zetu, wizara yangu inatatua migogoro kila siku, kama kuna mtu unamgogoro usisubiri Kamati ya Mawaziri msife na hiyo migogoro tupeni tuifanyie kazi hata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatuma wataalamu, tunavyo vifaa vya kutosha na wizara yangu hivi sasa imeanzisha Ofisi za Ardhi kila mkoa, kuna ma-*surveyor* kuna kila mtu, tutakuja kuainisha mipaka. Na katika kuahinisha mipaka Mheshimiwa Musukuma ndiyo tunavyofanya tunachukua viongozi wa pande mbili zote wanaobishania mipaka tunaamua kwa pamoja hatuendi sisi peke yetu, na ndiyo maana hata hii ya uhakiki wa Maliasili ipo mipaka iliyowekwa kwenye Hifadhi na Maliasili.

Mheshimiwa Spika, lakini tunataka tuunde timu maalumu ambayo wananchi na majirani pale na viongozi watahusika katika kuhakiki mipaka ya hifadhi ili waridhike kwamba mipaka hiyo inafanana kabisa na ile mipaka iliyoandikwa kwenye *GN* za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi hiyo tupeni tuifanye msisubiri kamati ya watu wa nane ni kazi yetu ya kila siku.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu mazuri sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, yanayotia moyo kwa kweli tunawatakia kila kheri kwa kazi hiyo. Kwa migogoro kama hii ya Mpungunero sijui kule Tarangire kwa kweli ni upande tu wa Serikali, Mpungunero ni kubwa. Hivi vijiji, vijiji ambavyo ni *periphery* ni kukata tu chukueni hiyo, wakina Tarangire, Tarangire *National Park* peke yake ni nusu ya Mkoa mzima wa Dodoma. Kwa hiyo, kimpaka cha kijiji hapo ni upande wa Serikali kuwa tu, kata rudisha, labda vihifadhi vidogo kama Manyara *National Park* kwa sababu ni kadogo sana unaweza ukaelewa.

Lakini mahifadhi mengi haya ma-*game reserved* nani makubwa mno kiasi kwamba ni Serikali tu, na maeneo haya yasingepatikana kama siyo wanakijiji hawa kuyatoa, ila sasa waweka mipaka ndiyo wakaweka vibaya. Kwa hiyo yanarekebishika tunawatakia kila kheri, Mheshimiwa Waziri.

Kama hakuna, tumeshamaliza maswali *unless* kuna mwongozo tunaendelea na shughuli.

Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI- KATIBU MEZANI:**

**MISWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Samahani kabla hatujaendelea sijamuita Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Simbachawene ambao ni pamoja na

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nchi Ndugu Christopher Kadio, ahsante Karibu sana Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Pia, tunaye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ndugu Ramadhani Kailima, karibu sana. *(Makofi)*

Pia, tunaye Kamishna Generali wa Uhamiaji ndugu Dkt. Anna Makakala. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wanawake, Makofi hayo hayatoshi hayo. *(Makofi/ Vigelegele)*

Pia, tunaye Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar ndugu Johari Sululu, ahsante sana. *(Makofi)*

Hili tangazo lingine nitawatangazia mwishoni. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu sana uwasilishe hoja yako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2020. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali Namba 5 ya Mwaka 2021 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Na.* 5 *Bill* 2021 kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Rehema na Neema zake na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge hili, ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu pia kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha Muswada wa Sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali Namba 5 ya Mwaka 2021 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Number 5 Bill 2021.*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano wanayoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, nina wapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uweledi na ufanisi ikiwemo kuandaa Muswada huu uliowasilishwa katika bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali Namba 5 wa mwaka 2021 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Number 5 Bill 2021* ambao upo mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu na kuishauri Serikali kwa malengo ya kuboresha Muswada huu. Na Serikali imezingatia ushauri wa kamati na imeleta jedwali la marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo umuhimu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Namba 5 ya mwaka 2021 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Number 5 Bill 2021*unapendekezwa kufanya marekebisho katika sheria

9 kwa lengo la kuboresha baadhi ya masharti katika sheria hizo na kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali katika sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432;

(ii) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95;

(iii) Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366;

(iv) Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sura ya 180;

(v) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54;

(vi) Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;

(vii) Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241;

(viii) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 298;

(ix) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260.

Mheshimiwa Spika, Mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi, ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya utangulizi. Ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Usafirishaji

Haramu wa Binadamu, Sura ya 432, ambapo katika Kifungu cha 3 tafsiri ya baadhi ya misamiati inapendekezwa kufutwa na badala yake, kuweka tafsiri mpya na tafsiri za misamiati mingine zinapendekezwa kuboreshwa. Kwa lengo la kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika matumizi ya misamiati hiyo. Kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kuweka masharti kwa kesi zinazohusisha makosa makubwa ya usafirishaji haramu wa binadamu kusikilizwa katika Mahakama Kuu. Kifungu kipya cha 8A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yatakayozuia majaribio ya kutenda makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa majaribio ya kutenda makosa chini ya Sheria hii yanawekewa adhabu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha kosa la kutoa taarifa binafsi za wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuzuia utoaji wa taarifa za wahanga kinyume na sheria na kuhakikisha kuwa maisha binafsi na utambulisho wa wahanga unalindwa. Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kupanua wigo wa watu wanaoweza kutoa taarifa, kuhusu makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu badala ya taarifa kutolewa na mhanga pekee kama ilivyo sasa katika Sheria. Marekebisho haya yana lengo la kutoa kwa kila mtu jukumu la kutoa taarifa za utendaji wa makosa kwa mamlaka husika. Kifungu cha 12 kinarekebishwa ili kumpa mtu yeyote anayemkamata mshukiwa wa usafirishaji haramu wa binadamu jukumu la kumfikisha mtu huyo katika Kituo cha Polisi kilicho karibu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 pia kinarekebishwa ili kutoa nafasi kwa mapato yanayotokana na mali zilizokamatwa au kutaifishwa katika utendaji wa makosa chini ya Sheria hii, kuweza kuwekwa katika Mfuko wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Hatua hii inapendekezwa kufanyika kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha. Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa idadi ya watu wanaoweza kuteuliwa kuhudumu katika Sekretarieti ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Marekebisho haya yanalenga

kumuwezesha Waziri kuamua na kuteua idadi ya watu watakaohudumu katika Sekretarieti kulingana na wajibu na majukumu ya Sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuongeza mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, katika Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu na kuainisha muda wa kushika madaraka kwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Awali, muda wa Wajumbe kuhudumu katika Kamati hiyo haukubainishwa katika Sheria. Kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla, kwa makosa ambayo adhabu mahsusi haijaainishwa na lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa makosa yote yanayotendwa dhidi ya masharti ya Sheria yanawekewa adhabu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95. Kifungu cha 2 kinarekebishwa ili kuweka tafsiri ya msamiati "*substance with drug related effect*", ambao umetumika katika masharti mbalimbali lakini haujapewa tafsiri katika Sheria na lengo ni kuondoa uwezekano wa msamiati huo kutafsiriwa vinginevyo wakati wa utekelezaji wa Sheria. Kifungu cha 4 cha Sheria hiyo kinapendekezwa kurekebishwa ili kuvitaka vyombo vingine vyovyote vyenye mamlaka ya kutoa vibali au leseni katika shughuli za dawa kuitaarifu Mamlaka kabla ya kutoa vibali au leseni. Marekebisho haya yana lengo la kuondoa ukiritimba katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kifungu cha 14 kinarekebishwa ili kujumuisha katika masharti yake dawa ambazo zimezuiliwa chini ya sheria nyingine yoyote na marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa dawa zote za kulevya zinadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 15 na 15A vya Sheria hiyo vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza uzito wa bangi na mirungi, anayoweza kukutwa nayo mtu katika makosa yanayosikilizwa katika Mahakama Kuu au Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya na

lengo la marekebisho haya ni kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama Kuu ambazo zingeweza kusikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya. Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kufanya kuwa kosa la jinai kitendo cha kukutwa na au kutumia kiwango kidogo cha dawa za kulevya. Kwa sasa, Sheria inazuia kitendo hicho bila kutamka kuwa ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366. Ambapo Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo kinachohusiana na matumizi ya Sheria kinarekebishwa ili kuiondoa Idara ya Uhamiaji katika wigo wa Sheria hiyo. Marekebisho haya yanatokana na mapendekezo ya kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura ya 180. Ambapo Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo kinarekebishwa ili kumuwezesha Mkurugenzi kutoa miongozo kwa ajili ya ukuaji na usimamizi wa masuala mbalimbali yanayohusu nyanda za malisho na vyakula vya wanyama. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuweka sifa sahihi za kitaaluma za mtu kuteuliwa kama Mkaguzi wa Vyakula vya Wanyama au Mkaguzi wa Nyanda za Malisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Ambapo Kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa lengo la kuongeza tafsiri ya neno "Wizara" ambalo limetumika katika masharti mbalimbali ya Sheria lakini halijatafsiriwa kwa sasa. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi na kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza Kanuni zitakazoainisha haki na stahili mbalimbali kwa Maafisa Uhamiaji kama za Majeshi mengine chini ya Wizara. Aidha, inapendekezwa kubaki na dhana ya "Idara" katika Sheria badala ya kubadili jina lote kuwa "Jeshi la Uhamiaji" ili kuendeleza taswira ya kidiplomasia ya Idara katika Jumuiya za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Nyama Sura ya 421. Kifungu kipya cha 10A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Bodi ya Nyama kukasimu utekelezaji wa baadhi ya majukumu yake kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa majukumu ya Bodi yanatekelezwa pia katika ngazi za Serikali za Mitaa. Vifungu vipya vvya 13A na 13B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa ofisi za Kanda na uteuzi wa Wakaguzi. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuhakikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Bodi na kumuwezesha Waziri, kuteua wakaguzi wa tasnia ya nyama watakaotekeleza majukumu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo pia kinarekebishwa ili kujumuisha miongoni mwa majukumu ya Msajili, jukumu la kutunza rejesta ya wadau wengine wa tasnia ya nyama ambao hawajatajwa katika kifungu hicho. Vilevile, Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuwataka wadau wote wa nyama kusajiliwa na Bodi kabla ya kufanya shughuli yoyote ya biashara katika tasnia ya nyama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa shughuli zote za kibiashara katika tasnia ya nyama zinasimamiwa na Bodi na wadau wote wanasajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241. Ambapo Kifungu cha 19A kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha mafao anayostahili kulipwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma Sura ya 371. Ambapo Kifungu cha 40 kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho na marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa Kamishna Jenerali wa

Uhamiaji, anapokea stahili sawa na Wakuu wa Majeshi mengine yaliyo chini ya Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Sura ya 260. Ambapo Kifungu cha 3 kinafanyiwa marekebisho ili kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria. Kifungu cha 4 kinarekebishwa ili kuitambua *TAWIRI* kama Taasisi kiongozi katika masuala ya utafiti wa wanyamapori na lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa, utafiti wowote kuhusiana na wanyamapori unafanywa kwa usimamizi wa *TAWIRI*. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa majukumu ya *TAWIRI* kwa kujumuisha miongoni mwa mambo mengine, utoaji wa ushauri wa kisayansi kuhusu wanyamapori walio katika hatari ya kupotea na kufanya sensa ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 10 na 11 vinarekebishwa kwa kuongeza adhabu iliyoainishwa kwa vitendo vya ukiukaji wa masharti ya vifungu hivyo. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa adhabu inayowekwa inazuia vitendo vya uvunjifu wa Sheria. Aidha, baada ya majadiliano na Kamati, Serikali imekubali kuongeza adhabu ya faini na kuweka adhabu ya kifungo. Pamoja na kufutiwa kibali cha kufanya utafiti kwa yeyote atakayekiuka masharti ya vifungu hivyo. Maboresho haya yanaonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Serikali. Aidha, vifungu vipya vya 11A na 11B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu hakimiliki za ugunduzi katika tafiti za wanyamapori na zuio la uchapishaji wa tafiti. Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa, haki zote zinazotokana na ugunduzi katika tafiti za wanyamapori zinalindwa na tafiti za wanyamapori zinachapishwa kwa idhini ya *TAWIRI*.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza Kanuni ili kujumuisha maeneo

mengine ambayo yanaweza kuhitaji kufafanuliwa zaidi katika Kanuni. Kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa pia ili kuweka utaratibu wa rufaa kwa mtu asiyeridhika na maamuzi ya Taasisi. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha sifa za mtu kuteuliwa kama Mkurugenzi Mkuu wa *TAWIRI* pamoja na majukumu yake. Kwa sasa, Sheria haijabainisha sifa hizo na majukumu mahsusi yanayopaswa kutekelezwa na Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha 21 cha Sheria kinarekebishwa ili kutambua fedha na michango inayotoka katika Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato ya *TAWIRI*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill,* 2021) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. ADELARDUS L. KILANGI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 5) WA MWAKA 2021 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 5) BILL, 2021) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA - KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

---

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, naomba kutoa Hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 **(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021')** kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa

usomwe Mara ya Pili; na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema zake na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa nne wa Bunge. Ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 **(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021).**

**Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa weledi na ufanisi, ikiwemo kuandaa Muswada huu uliowasilishwa katika Bunge hili.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 **(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021** ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali

imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021, **(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021)** unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa (9) kwa lengo la kuboresha baadhi ya masharti katika Sheria hizo na kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali katika Sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

1. Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432;
2. Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95;
3. Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366;
4. Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sura ya 180;
5. Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54;
6. Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;
7. Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241;
8. Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 298; na
9. Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260.

## MPANGILIO WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya utangulizi, ikiwa ni pamoja na, jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Usafirishaji

Haramu wa Binadamu, Sura ya 432, ambapo katika kifungu cha 3 tafsiri ya baadhi ya misamiati inapendekezwa kufutwa na badala yake kuweka tafsiri mpya na tafsiri za misamiati mingine zinapendekezwa kuboreshwa kwa lengo la kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika matumizi ya misamiati hiyo. Kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kuweka masharti kwa kesi zinazohusisha makosa makubwa ya usafirishaji haramu wa binadamu kusikilizwa katika Mahakama Kuu. Kifungu kipya cha 8A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yatakayozuia majaribio ya kutenda makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa majaribio ya kutenda makosa chini ya Sheria hii yanawekewa adhabu.

Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha kosa la kutoa taarifa binafsi za wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuzuia utoaji wa taarifa za wahanga kinyume na sheria na kuhakikisha kuwa maisha binafsi na utambulisho wa wahanga unalindwa. Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kupanua wigo wa watu wanaoweza kutoa taarifa kuhusu makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu badala ya taarifa kutolewa na mhanga pekee kama ilivyo sasa katika Sheria. Marekebisho haya yana lengo la kutoa kwa kila mtu jukumu la kutoa taarifa za utendaji wa makosa kwa mamlaka husika. Kifungu cha 12 kinarekebishwa ili kumpa mtu yeyote anayemkamata mshukiwa wa usafirishaji haramu wa binadamu jukumu la kumfikisha mtu huyo katika kituo cha polisi kilicho karibu.

Kifungu cha 26 kinarekebishwa ili kutoa nafasi kwa mapato yanayotokana na mali zilizokamatwa au kutaifishwa katika utendaji wa makosa chini ya Sheria hii kuweza kuwekwa katika Mfuko wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Hatua hii inapendekezwa kufanyika kwa idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha. Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa idadi ya watu wanaoweza kuteuliwa kuhudumu katika Sekretarieti ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Marekebisho haya yanalenga kumuwezesha

Waziri kuamua na kuteua idadi ya watu watakaohudumu katika Sekretarieti kulingana na wajibu na majukumu ya Sekretarieti.

Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuongeza mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu na kuainisha muda wa kushika madaraka kwa wajumbe wa Kamati hiyo. Awali, muda wa wajumbe kuhudumu katika Kamati hiyo haukubainishwa katika Sheria. Kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahsusi haijaainishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa makosa yote yanayotendwa dhidi ya masharti ya Sheria yanawekewa adhabu.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95. Kifungu cha 2 kinarekebishwa ili kuweka tafsiri ya msamiati "*substance with drug related effect*" ambao umetumika katika masharti mbalimbali lakini haujapewa tafsiri katika Sheria. Lengo ni kuondoa uwezekano wa msamiati huo kutafsiriwa vinginevyo wakati wa utekelezaji wa Sheria. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuvitaka vyombo vingine vyovyote vyenye mamlaka ya kutoa vibali au leseni katika shughuli ya dawa kuitaarifu Mamlaka kabla ya kutoa vibali au leseni. Marekebisho haya yana lengo la kuondoa ukiritimba katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya udhibiti wa dawa za kulevya. Kifungu cha 14 kinarekebishwa ili kujumuisha katika masharti yake dawa ambazo zimezuiliwa chini ya sheria nyingine yoyote. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa dawa zote za kulevya zinadhibitiwa.

Vifungu vya 15 na 15A vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza uzito wa bangi na mirungi anayoweza kukutwa nayo mtu katika makosa yanayosikilizwa katika Mahakama Kuu au Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama Kuu

ambazo zingeweza kusikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya. Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kufanya kuwa kosa la jinai kitendo cha kukutwa na au kutumia kiwango kidogo cha dawa za kulevya. Kwa sasa, Sheria inazuia kitendo hicho bila kutamka kuwa ni kosa la jinai.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366, ambapo kifungu cha 2 kinachohusiana na matumizi ya Sheria kinarekebishwa ili kuiondoa Idara ya Uhamiaji katika wigo wa Sheria hiyo. Marekebisho haya yanatokana na mapendekezo ya kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sura ya 180, ambapo kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kumuwezesha Mkurugenzi kutoa miongozo kwa ajili ya ukuaji na usimamizi wa masuala mbalimbali yanayohusu nyanda za malisho na vyakula vya wanyama. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuweka sifa sahihi za kitaaluma za mtu kuteuliwa kama mkaguzi wa vyakula vya wanyama au mkaguzi wa nyanda za malisho.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54, ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa lengo la kuongeza tafsiri ya neno "Wizara" ambalo limetumika katika masharti mbalimbali ya Sheria lakini halijatafsiriwa kwa sasa. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi na kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazoainisha haki na stahili mbalimbali kwa maafisa uhamiaji kama za majeshi mengine chini ya Wizara. Aidha, inapendekezwa kubaki na dhana ya "Idara" katika Sheria badala ya kubadili jina kuwa "Jeshi la Uhamiaji" ili kuendeleza taswira ya kidiplomasia ya Idara katika jumuiya ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421. Kifungu kipya cha 10A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Bodi ya Nyama kukasimu utekelezaji wa baadhi ya majukumu yake kwa mamlaka za serikali za mitaa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa majukumu ya Bodi yanatekelezwa pia katika ngazi za serikali za mitaa. Vifungu vipya vvya 13A na 13B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa ofisi za kanda na uteuzi wa wakaguzi. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuhakikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Bodi na kumuwezesha Waziri kuteua wakaguzi wa tasnia ya nyama watakaotekeleza majukumu katika maeneo husika.

Kifungu cha 16 kinarekebishwa ili kujumuisha miongoni mwa majukumu ya Msajili, jukumu la kutunza rejesta ya wadau wengine wa tasnia ya nyama ambao hawajatajwa katika kifungu hicho. Vilevile, kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuwataka wadau wote wa nyama kusajiliwa na Bodi kabla ya kufanya shughuli yoyote ya kibiashara katika tasnia ya nyama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa shughuli zote za kibiashara katika tasnia ya nyama zinasimamiwa na Bodi na wadau wote wanasajiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241, ambapo kifungu cha 19A kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha mafao anayostahili kulipwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371, ambapo kifungu cha 40 kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho. Marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha kuwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anapokea stahili sawa na wakuu wa majeshi

mengine yaliyo chini ya Wizara yenye dhamana na mambo ya ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260, ambapo kifungu cha 3 kinafanyiwa marekebisho ili kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria. Kifungu cha 4 kinarekebishwa ili kuitambua TAWIRI kama taasisi kiongozi katika masuala ya utafiti wa wanyamapori. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa utafiti wowote kuhusiana na wanyamapori unafanywa kwa usimamizi wa TAWIRI. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa majukumu ya TAWIRI kwa kujumuisha, miongoni mwa mambo mengine, utoaji wa ushauri wa kisayansi kuhusu wanyamapori walio katika hatari ya kupotea na kufanya sensa ya wanyamapori.

Vifungu vya 10 na 11 vinarekebishwa kwa kuongeza adhabu iliyoainishwa kwa vitendo vya ukiukaji wa masharti ya vifungu hivyo. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa adhabu inayowekwa inazuia vitendo vya uvunjifu wa sheria. Aidha, baada ya majadiliano na Kamati, Serikali imekubali kuongeza adhabu ya faini na kuweka adhabu ya kifungo pamoja na kufutiwa kibali cha kufanya utafiti kwa yeyote atakayekiuka masharti ya vifungu hivyo. Maboresho haya yanaonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Serikali. Aidha, vifungu vipya vya 11A na 11B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu hakimiliki ya ugunduzi katika tafiti za wanyamapori na zuio la uchapishaji wa tafiti. Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa haki zote zinazotokana na ugunduzi katika tafiti za wanyamapori zinalindwa na tafiti za wanyamapori zinachapishwa kwa idhini ya TAWIRI.

Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza kanuni ili kujumuisha maeneo mengine ambayo yanaweza kuhitaji kufafanuliwa zaidi katika Kanuni. Kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka utaratibu wa

rufaa kwa mtu asiyeridhika na maamuzi ya Taasisi. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha sifa za mtu kuteuliwa kama Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI pamoja na majukumu yake. Kwa sasa, Sheria haijabainisha sifa hizo na majukumu mahsusi yanayopaswa kutekelezwa na Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha 21 cha Sheria kinarekebishwa ili kutambua fedha na michango inayotoka katika Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato ya TAWIRI.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 **(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021)** na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA.

Prof. Adelardus L. Kilangi
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

.
ISSN 0856 - 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 10*** ***25th August, 2021***

# *SPECIAL BILL SUPPLEMENT*

*To the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.10. Vol.101 dated 25th August, 2021*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

## THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 5) ACT, 2021

### PART I
### PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

### PART II
### AMENDMENT OF THE ANTI-TRAFFICKING IN PERSONS ACT, (CAP.432)

3. Construction.
4. Amendment of section 3.
5. Amendment of section 6.
6. Addition of section 8A.
7. Amendment of section 9.
8. Repeal and replacement of section 10.
9. Amendment of section 12.
10. Amendment of section 26.
11. Amendment of section 30.
12. Amendment of section 31.
13. Addition of section 34A.

### PART III
### AMENDMENT OF THE DRUG CONTROL AND ENFORCEMENT ACT, (CAP. 95)

14. Construction.
15. Amendment of section 2.
16. Amendment of section 4.
17. Amendment of section 14.
18. Amendment of section 15.
19. Amendment of section 15A.
20. Amendment of section 17.

PART IV
AMENDMENT OF THE EMPLOYMENT AND LABOUR RELATIONS ACT,
(CAP. 366)

21. Construction.
22. Amendment of section 2.

PART V
AMENDMENT OF THE GRAZING LAND AND ANIMAL FEED RESOURCES ACT,
(CAP. 180)

23. Construction.
24. Amendment of section 6.
25. Amendment of section 7.

PART VI
AMENDMENT OF THE IMMIGRATION ACT,
(CAP. 54)

26. Construction.
27. Amendment of section 3.
28. Amendment of section 4.

PART VII
AMENDMENT OF THE MEAT INDUSTRY ACT,
(CAP. 421)

29. Construction.
30. Addition of section 10A.
31. Addition of sections 13A and 13B.
32. Amendment of section 16.
33. Amendment of section 17
34. Amendment of section 33A

PART VIII
AMENDMENT OF THE POLICE FORCE, TANZANIA IMMIGRATION SERVICES DEPARTMENT AND PRISONS SERVICE COMMISSION ACT,
(CAP. 241)

35. Construction.
36. Amendment of section 19A.

PART IX
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND ACT,
(CAP. 371)

37. Construction.
38. Amendment of section 40.

## PART X
## AMENDMENT OF THE TANZANIA WILDLIFE RESEARCH INSTITUTE ACT,
## (CAP. 260)

39. Construction.
40. Amendment of section 3.
41. Amendment of section 4.
42. Amendment of section 5.
43. Amendment of section 10.
44. Amendment of section 11.
45. Addition of sections 11A and 11B.
46. Amendment of section 13.
47. Addition of section 13A.
48. Repeal and replacement of section 14.
49. Amendment of section 21.

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
21st August, 2021

HUSSEIN A. KATTANGA
*Secretary to the Cabinet*

## A BILL
*for*

**An Act to amend certain written laws.**

**ENACTED** by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

**1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Act, 2021.

Amendment of certain written laws

**2.** The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE ANTI-TRAFFICKING IN PERSONS ACT, (CAP. 432)

Construction Cap. 432

**3**. This Part shall be read as one with the Anti-Trafficking in Persons Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 3

**4**. The principal Act is amended in section 3, by-

(a) adding the words "in the case of Mainland Tanzania or the Regional Court in the case of Tanzania Zanzibar" immediately after the words "District Court" appearing in the definition of the term "court";

(b) deleting the definition of the terms “exploitation”, “security services” and “social welfare officer” and substituting for them the following:

““exploitation” includes-

(a) keeping a person in a state of slavery;
(b) subjecting a person to practices similar to slavery;
(c) involuntary servitude;
(d) forcible or fraudulent use of any human being for removal of organs or body parts;
(e) forcible or fraudulent use of any human being to take part in armed conflict;
(f) forced labour;
(g) sexual exploitation;
(h) forced marriage; or
(i) forced begging;

“security services” includes the police, Tanzania Revenue Authority, immigration, Anti-Trafficking in Persons Secretariat, Ministry responsible for social welfare, Ministry responsible for labour and employment, local government authority and the Tanzania Intelligence and Security Services;”;

“social welfare officer” means a social welfare officer in the service of the Government;”; and

(c) adding in the appropriate alphabetical order the following definition:

““victim of trafficking in persons” means a person against whom an act of trafficking under section 4 has been committed;”.

Amendment of section 6

**5**. The principal Act is amended in section 6 by adding immediately after subsection (4) the following:

“(5) Notwithstanding the provisions of any written law to the contrary, an offence under this section shall be tried in the High Court.”.

Addition of section 8A

**6**. The principal Act is amended by adding immediately after section 8 the following:

“Attempt to commit offence

**8A**. Any person who attempts to commit an offence under this Part shall, on conviction, be liable to a fine

of not less than one million shillings but not exceeding five million shillings or imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding one year, or to both.".

Amendment of section 9

**7**. The principal Act is amended in section 9 by adding immediately after subsection (5) the following:

"(6) Any person who contravenes the provisions of this section commits an offence.".

Repeal and replacement of section 10

**8**. The principal Act is amended by repealing section 10 and replacing it with the following:

"Reporting of offences

**10**.-(1) A person who possesses information about any person committing an offence of trafficking in persons shall immediately report the offence to the police officer or any person in the security services within the locality.

(2) Any person who contravenes subsection (1) commits an offence.

(3) Where the information under subsection (1) is reported to a person other than a police officer, such person shall convey the information to the nearest police station.".

Amendment of section 12

**9.** The principal Act is amended in section 12 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Where an arrest under this Act is carried out by an officer from another security service, such officer shall immediately hand over the arrested person to the nearest police station.".

Amendment of section 26

**10**. The principal Act is amended in section 26, by-

(a) designating the content of section 26 as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

"(2) The sale proceeds of any property confiscated or forfeited under this Act may, subject to approval of the Minister responsible for finance, be deposited in the Fund.".

Amendment of section 30

**11**. The principal Act is amended in section 30 by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) The Anti-Trafficking Committee shall be supported by a Secretariat which shall consist of such number of persons appointed by the Minister after consultation with the Minister responsible for public service.".

Amendment of section 31

**12**. The principal Act is amended in section 31-

(a) in subsection (1), by-

(i) adding immediately after paragraph (l) the following:

"(m) a law officer from the National Prosecutions Service not below the designation of an assistant director;"; and

(ii) renaming paragraphs (m) and (n) as paragraphs (n) and (o) respectively; and

(b) by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) A member of the Committee shall, unless his appointment is otherwise terminated, hold office for three years and may be eligible for re-appointment for one further term.".

Addition of section 34A

**13.** The principal Act is amended by adding immediately after section 34 the following:

"General penalty

**34A**. Any person who commits an offence under this Act for which no specific penalty is prescribed shall, on conviction, be liable to a fine of not less than one million shillings but not exceeding ten million shillings or imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years, or to both.".

## PART III
## AMENDMENT OF THE DRUG CONTROL AND ENFORCEMENT ACT, (CAP. 95)

Construction Cap. 95

**14**. This Part shall be read as one with the Drug Control and Enforcement Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**15**. The principal Act is amended in section 2 by adding in the appropriate alphabetical order the following definition:

"“substance with drug related effect” means a substance with addictive properties presenting a risk of abuse as a drug and may pose a threat to public health;”.

Amendment of section 4

**16**. The principal Act is amended in section 4 by deleting subsections (5) and (6) and substituting for them the following:

“(5) For purposes of controlling drug, drug abuse and trafficking in drugs, diversion of precursor chemicals and controlled pharmaceuticals, any other authority vested with powers to issue permit or licence to deal or engage in drug, precursor chemicals or substances with drug related effects, shall notify the Authority before issuing import or export permit, licence or certificate.

(6) The Authority may make rules for better implementation of its functions under this Act.”.

Amendment of section 14

**17.** The principal Act is amended in section 14 by inserting the words “Without prejudice to the drugs, psychotropic substances or precursor chemicals prohibited under any other written laws,” immediately before the words “The list” appearing at the beginning of subsection (1).

Amendment of section 15

**18**. The principal Act is amended in section 15(3) by deleting the word “fifty” appearing in paragraph (iii) and substituting for it the words “one hundred”.

Amendment of section 15A

**19**. The principal Act is amended in section 15A, by-

(a) inserting the words “of not less than” immediately after the word “term” appearing in subsection (1); and

(b) deleting the word “fifty” appearing in subsection (2)(c) and substituting for it the words “one hundred”.

Amendment of section 17

**20**. The principal Act is amended in section 17(1) by inserting the words “commits an offence and” between the

words "substance" and "shall".

## PART IV
## AMENDMENT OF THE EMPLOYMENT AND LABOUR RELATIONS ACT,
## (CAP. 366)

Construction Cap. 366

**21**. This Part shall be read as one with the Employment and Labour Relations Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**22**. The principal Act is amended in section 2(1), by-

(a) deleting the word "or" appearing at the end of paragraph (iii);

(b) deleting the fulstop appearing at the end of paragraph (iv) and substituting for it a semicolon and the word "or"; and

(c) adding immediately after paragraph (iv) the following:

"(v) the Immigration Services Department.".

## PART V
## AMENDMENT OF THE GRAZING LAND AND ANIMAL FEED RESOURCES ACT,
## (CAP. 180)

Construction Cap. 180

**23**. This Part shall be read as one with the Grazing Land and Animal Feed Resources Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 6

**24**. The principal Act is amended in section 6(3) by inserting the words "management and development of grazing land control," between the words "for the" and "manufacture" appearing in paragraph (e).

Amendment of section 7

**25**. The principal Act is amended in section 7(2), by-

(a) adding the words "range management," immediately after the words "degree in" appearing in paragraph (a); and

(b) deleting the words "animal range" appearing in paragraph (b) and substituting for them the words "range management".

## PART VI
## AMENDMENT OF THE IMMIGRATION ACT, (CAP. 54)

Construction Cap. 54

**26**. This Part shall be read as one with the Immigration Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 3

**27.** The principal Act is amended in section 3 by adding in the appropriate alphabetical order the following definition:

"Ministry" means the Ministry responsible for matters relating to immigration;".

Amendment of section 4

**28**. The principal Act is amended in section 4, by-

(a) deleting the words "responsible for Home Affairs" appearing in subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) The Department established under subsection (1) shall be a Force within the Ministry and in that capacity-

(a) it shall be governed in a manner and style similar to other forces within the Ministry; and

(b) it shall have all the rights and privileges enjoyed by other forces within the Ministry.

(4) The Minister may make regulations prescribing the rights and privileges which may be enjoyed by immigration officers of the Department.".

## PART VII
## AMENDMENT OF THE MEAT INDUSTRY ACT, (CAP. 421)

Construction Cap. 421

**29**. This Part shall be read as one with the Meat Industry Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of section 10A

**30**. The principal Act is amended by adding immediately after section 10 the following:

"Delegation of functions

**10A**.-(1) The Board may, upon recommendation by the Registrar and after consultation with the Minister,

delegate some of its functions to a local government authority.

(2) The functions delegated under subsection (1) shall be performed under the supervision of the Registrar.".

Addition of sections 13A and 13B

**31**. The principal Act is amended by adding immediately after section 13 the following:

"Establishment of zones

**13A**.-(1) The Board may, upon recommendation by the Registrar and after consultation with the Minister, establish meat industry zones as it may deem necessary for better carrying out and implementation of the functions of the Board.

(2) The zones established shall be headed by the zonal officer in-charge under the supervision of the Registrar.

(3) The zonal officer in-charge shall be appointed from among livestock or food science professionals with proven experience in the meat industry.

Appointment of inspectors and graders

**13B**.-(1) The Minister may, by order published in the *Gazette*, appoint meat inspectors, meat graders and livestock graders from amongst livestock or food science professionals in the public service who shall perform functions within specified areas.

(2) The tenure, powers, duties and functions of meat inspectors, meat graders and livestock graders shall be prescribed in the regulations.

(3) Without prejudice to subsection (1), any person employed by the Board as a livestock or food science professional shall be deemed to be a meat inspector from the date of employment.".

Amendment of section 16

**32**. The principal Act is amended in section 16(4)(a) by adding immediately after subparagraph (iv) the following:

"(v) other meat industry stakeholders;".

Amendment of section 17

**33**. The principal Act is amended in section 17, by-

(a) deleting the words "of livestock producer, trader or livestock market operator" appearing in subsection (1) and substituting for them the words "as a meat industry stakeholder";

(b) deleting the words "livestock producer, or trader or livestock market operator after complying with the conditions prescribed by the Board" appearing in subsection (2) and substituting for them the words "meat industry stakeholder after complying with the conditions prescribed in the regulations"; and

(c) deleting the words "by the Board" appearing in subsection (3) and substituting for them the words "in the regulations".

Amendment of section 33A

**34**. The principal Act is amended in section 33A(2) by inserting the word "not" between the words "but" and "exceeding".

## PART VIII
## AMENDMENT OF THE POLICE FORCE, TANZANIA IMMIGRATION SERVICES DEPARTMENT AND PRISONS SERVICE COMMISSION ACT, (CAP. 241)

Construction Cap. 241

**35**. This Part shall be read as one with the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prisons Service Commission Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 19A

**36**. The principal Act is amended in section 19A by adding the words "the Commissioner General of Immigration" immediately after the word "Prisons" appearing in subsection (1).

## PART IX
## AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND ACT, (CAP. 371)

Construction Cap. 371

**37**. This Part shall be read as one with the Public Service Social Security Fund Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 40

**38**. The principal Act is amended in section 40(3) by

adding the words "the Commissioner General of Immigration" immediately after the word "Prisons" appearing in paragraph (c)

## PART X
## AMENDMENT OF THE TANZANIA WILDLIFE RESEARCH INSTITUTE ACT,
## (CAP. 260)

Construction
Cap. 260

**39**. This Part shall be read as one with the Tanzania Wildlife Research Institute Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 3

**40**. The principal Act is amended in section 3, by-

(a) deleting the definition of the term "Director of Game"; and

(b) deleting the definition of the term "wildlife" and substituting for it the following:

""wildlife" has the meaning ascribed to it under the Wildlife Conservation Act;"; Cap. 283

(c) adding in the appropriate alphabetical order the following definitions:

""CITES" means the Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora of 1973 and includes any appendices thereto and any resolutions of the Conferences of the Parties;

"Director" means the Director of Wildlife appointed under section 7 of the Wildlife Conservation Act;"; Cap. 283

"research" means a systematic study conducted in order to develop, verify and disseminate appropriate technologies for the benefit of stakeholders in the wildlife industry;".

Amendment of section 4

**41**. The principal Act is amended in section 4(1) by adding the phrase "or in its acronym "TAWIRI" which shall be the leading institute responsible for wildlife research" immediately after the word "Institute".

Amendment of section 5

**42**. The principal Act is amended in section 5(1), by-

(a) adding immediately after paragraph (k) the following:

"(l) to provide scientific advice for wildlife protected under CITES;

(m) subject to consultation with the Minister, to establish and manage forensic laboratories and collect forensic data on wildlife genetic resources;
(n) to conduct wildlife census and monitoring of wildlife population in Mainland Tanzania; and"; and
(b) renaming paragraph (l) as paragraph (o).

Amendment of section 10

**43**. The principal Act is amended in section 10, by-
(a) adding the words "data and sample" immediately after the word "information" appearing in subsection (1); and
(b) deleting subsection (2) and substituting for it the following:
"(2) Any person who contravenes or fails to comply with subsection (1) commits an offence and shall, upon conviction, be liable to a fine of not less than five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings.".

Amendment of section 11

**44**. The principal Act is amended in section 11, by-
(a) adding the words "data and sample" immediately after the word "information" wherever it appears in subsections (1) and (2);
(b) deleting the words "not exceeding fifteen thousand shillings" appearing in subsection (2) and substituting for them the phrase "of not less than five hundred thousand shillings but not exceeding two million shillings"; and
(c) adding immediately subsection (2) the following:
"(3) In addition to the penalty under subsection (2) and subject to the procedures prescribed in the regulations, any permit issued to a person convicted under this section may be withdrawn.".

Addition of sections 11A and 11B

**45**. The principal Act is amended by adding immediately after section 11 the following:

"Intellectual property on invention

**11A.**-(1) Any rights to an invention or discovery in wildlife research shall-
(a) in the case of research conducted by the Institute, be owned by the

Institute; and

(b) in the case of research conducted by the Institute and another person, be co-owned by the researcher and the Institute.

(2) Any person who intends to use an invention or discovery under subsection (1) shall seek written permission from the researcher and the Institute.

Restriction to publish

**11B.** Any person who conducts wildlife research in Mainland Tanzania shall not publish or cause to be published the results of such research unless the person has obtained approval of the Institute.".

Amendment of section 13

**46**. The principal Act is amended in section 13(2), by-

(a) by adding immediately after paragraph (d) the following:

"(e) prescribing for registration of local and foreign wildlife researchers and the mode of application, refusal and cancellation of registration;

(f) for coordinating wildlife research projects and allied scientific research carried in Mainland Tanzania;

(g) prescribing for the use of wildlife research data and information;

(h) regarding the ownership of intellectual property rights including wildlife research data and information and research discovery;

(i) prescribing conditions for export of wildlife specimens or samples;

(j) prescribing research fees and charges;

(k) for conducting physical and chemical wildlife immobilization;

(l) prescribing procedures regarding engagement of research associates;

(m) prescribing procedures for publication of wildlife research findings; and";

(b) renaming paragraph (e) as paragraph (n).

Addition of section 13A

**47**. The principal Act is amended by adding immediately after section 13 the following:

"Appeals

**13A**. Any person who is aggrieved by the decision of the Institute when implementing any provision of this Act may, within thirty days upon receipt of such decision, appeal to the Minister.".

Repeal and replacement of section 14

**48**. The principal Act is amended by repealing section 14 and replacing it with the following:

"Appointment, functions and powers of Director General

**14**.-(1) There shall be a Director General of the Institute appointed by the President on the advice of the Minister from amongst persons who possess relevant qualifications and competence to manage efficiently and effectively the affairs of the Institute.

(2) A person shall be eligible for appointment as a Director General if that person is a citizen of Tanzania with high level intergrity and possesses-

(a) a doctorate degree in wildlife or related sciences from a recognized university; and
(b) proven knowledge and experience of at least ten years in matters relating to wildlife research and development; and
(c) at least seven years experience in a managerial position of any research related institute.

(3) The Director General shall be the Chief Executive Officer of the Institute and shall be responsible for-

(a) day to day operations and affairs of the Institute;
(b) mobilisation and management of funds, properties and business of the Institute;
(c) administration, organisation and management of staff of

the Institute and discipline of the employees other than management staff of the Institute; and

(d) coordination and implementation of policies and programmes of the Institute.”.

Amendment of section 21

**49**. The principal Act is amended in section 21, by-

(a) adding immediately after paragraph (c) the following:

“(d) such sums or contributions as the Institute may receive from the Tanzania Wildlife Protection Fund;”; and

(b) renaming paragraph (d) as paragraph (e).

## OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend Nine laws namely; Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432, the Drug Control and Enforcement Act, Cap. 95, the Employment and Labour Relations Act, Cap. 366, the Grazing Land and Animal Feed Resources Act, Cap. 180, the Immigration Act, Cap. 54, the Meat Industry Act, Cap. 421, the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prisons Service Commission Act, Cap. 241, the Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371 and the Tanzania Wildlife Research Institute Act, Cap. 260.

This Bill is divided into Ten Parts as follows:

Part I of the Bill contains Preliminary Provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432, whereas in section 3 the definitions of certain terms have been deleted and therewith substituted with new definitions and other definitions have been amended with the aim of ensuring that the terms used are correctly defined in order to avoid any ambiguity. Section 6 is amended in order to require offences of severe trafficking in persons to be tried in the High Court. A new section 8A is proposed to be added in order to introduce a provision to prohibit attempts to commit offences under the Act. The amendment aims at ensuring that even attempts to commit offences of trafficking are penalised.

Section 9 is proposed to be amended in order to establish an offence for disclosing private information of victims of trafficking. The amendment aims at discouraging unlawful disclosure of information and ensuring that the private life and identity of victims of trafficking is protected. Section 10 is amended in order to allow information about offences of trafficking in persons to be reported by any person instead of the victim only. The amendment aims at imposing a duty on any person who obtains information on trafficking to report the same to the relevant authorities. Section 12 is amended in order to impose on any person who arrests a suspect of trafficking a duty of handing over the arrested person to the nearby police station.

Sections 26 of the Act is amended in order to enable the proceeds from properties confiscated or forfeited under the Act to be deposited in the Anti-

Trafficking Fund. Section 30 is amended by removing the limit in the number of the persons who may be appointed to serve in the Secretariat. The aim of the amendment is to enable the Minister to determine and appoint sufficient persons depending on the needs arising and extent of the duties and functions of the Secretariat. Section 31 is amended by adding to the Anti-Trafficking Committee a member from the National Prosecutions Service and specifying the tenure of office for members of the Committee. A new section 34A is proposed to be amended in order to introduce a general penalty in respect of offences for which a specific penalty is not prescribed. The aim of the amendment is to ensure that penalties are prescribed for all offences under the Act.

Part III of the Bill proposes to amend the Drug Control and Enforcement Act, Cap. 95. Section 2 is amended in order to provide the definition of the term "substance with drug related effect" which has been used in several provisions in the Act but is currently not defined. Section 4 is proposed to be amended so as to require other authorities empowered to issue permits or licences to deal in drugs to notify the Authority instead of consulting the Authority before issuing such permit or licence. The aim is to reduce unnecessary bureaucratic procedures and enable better implementation of the functions of the Authority in regulating drugs. Section 14 is proposed to be amended so as to recognise include drugs that are prohibited under any other written laws. The amendment aims at ensuring that all narcotic drugs, psychotropic substances or precursor chemicals are regulated.

Sections 15 and 15A are proposed to be amended with the view of increasing the limit of the weight of cannabis or khat in respect of offences triable by the High Court or District Court respectively. The aim of the amendment is to reduce backlog of cases in the District Courts awaiting to be tried by the High Court. Section 17 is amended in order to criminalise the possession or use of a small quantity of narcotic drug or psychotropic substance. Currently the Act prohibits such possession or use but does not make it an offence.

Part IV of the Bill proposes to amend the Employment and Labour Relations Act, Cap. 366, whereas section 2 relating to application of the Act is amended in order to exclude the Immigration Services Department from the scope of the Act. These amendments are a result of recognition of the Immigration Services Department as a Force.

Part Vof the Bill proposes to amend the Grazing Land and Animal Feed Resources Act, Cap. 180, whereby section 6 is amended so as to enable the Director to issue guidelines for the development and management of various matters concerning grazing land and animal feeds. Section 7(3) is amended in order to provide for the correct academic qualification for appointment as an animal feed inspector or a grazing land inspector.

Part VI of the Bill proposes to amend the Immigration Act, Cap. 54. Section 3 is amended so as to add the definition of the term "Ministry" which has been used in several provisions of the Act but is currently not defined. Section 4 is amended in order to recognise the Immigration Department as a Force within the Ministry and to enable the Minister to make regulations providing for the rights and privileges of immigration officers similar to other forces within the Ministry. However, it is proposed to retain the concept "Immigration Department" in the Act instead of changing it to "Immigration Force" so as to maintain the diplomatic image of the Department in the international sphere.

Part VII of the Bill proposes to amend the Meat Industry Act, Cap. 421. A new section 10A is proposed to be added so as to empower the Board to delegate some of its functions to a local government authority. The aim of the amendment is to ensure that the Board's functions are implemented even at the local government level. New sections 13A and 13B are added so as to make provision for establishment of zones and appointment of inspectors. The proposed establishment of meat industry zones is intended to ensure better implementation of the functions of the Board. Further, the proposed section 13B aims to empower the Minister to appoint meat inspectors from amongst livestock or food science professionals to perform functions in their specified areas.

Section 16 is amended so as to include in the powers of the Registrar the duty to keep and maintain a register of other meat industry stakeholders not mentioned in that provision. Similarly, section 17 is amended so as to require all meat industry stakeholders to be registered by the Board before carrying on business in the meat industry. The aim of these amendments is to ensure that all business activities in the meat industry are regulated by the Board and all stakeholders are registered.

Part VIII of the Bill proposes to amend the Police Force, Tanzania Immigration Services Department and Prisons Service Commission Act, Cap. 241, whereby section 19A is amended by including the Commissioner General of Immigration within the provisions of that section. The aim of the amendment is to provide for the terminal benefits to which the Commissioner General is entitled.

Part IX of the Bill proposes to amend the Public Service Social Security Fund Act, Cap. 371, whereby section 40 is amended by including the Commissioner General of Immigration within the provisions of that section. The amendment aims at ensuring that the Commissioner General of Immigration receives similar benefits entitled to the heads of other forces within the Ministry of Home Affairs.

Part X of the Bill proposes to amend the Tanzania Wildlife Research Institute Act, Cap. 260, whereas section 3 is amended so as to add the definition of

various terms used in the Act. Section 4 is amended so as to recognize TAWIRI as the leading Institute in wildlife research. The aim of the amendment is to ensure that any research in wildlife is conducted under the regulation and supervision of TAWIRI. Section 5 is proposed to be amended so as to widen the scope of the Institute's functions to include, among other things, providing scientific advice for endangered wildlife and conducting wildlife census.

Sections 10 and 11 are proposed to be amended so as to enhance the penalty for commission of offences under those provisions. The aim of the amendment is to ensure that the penalty provided by the Act deters contravention of the provisions of the law. It is further proposed to add new sections 11A and 11B to make provisions for intellectual property on inventions in wildlife research and restriction to publish research findings. The aim of the proposed sections is to ensure that all rights relating to inventions or discoveries in wildlife research conducted in Mainland Tanzania are protected and any findings are published upon approval by TAWIRI.

Section 13 is proposed to be amended so as to widen the scope of the areas for which the Minister may make regulations in order to include other areas which may need to further be expounded by regulations. A new section 13A is proposed to be introduced so as to allow appeals to be made to the Minister by persons aggrieved by any decision of the Institute. Section 14 is amended so as to provide for the qualifications for a person to be appointed as the Director General of the Institute and the functions to be performed by him. Section 21 is amended so as to recognize the contributions from the Tanzania Wildlife Protection Fund to be among the sources of the funds of the Institute.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria Tisa zifuatazo: Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95, Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366, Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sura ya 180, Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54, Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421, Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha Masharti ya Utangulizi ambayo ni Jina la Muswada na tamko kuhusu marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, ambapo katika kifungu cha 3 tafsiri ya baadhi ya misamiati inapendekezwa kufutwa na badala yake kuweka tafsiri mpya na tafsiri za misamiati mingine zinapendekezwa kuboreshwa kwa lengo la kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika matumizi ya misamiati hiyo. Kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kuweka masharti kwa kesi zinazohusisha makosa makubwa ya usafirishaji wa binadamu kusikilizwa katika Mahakama Kuu. Kifungu kipya cha 8A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yatakayozuia majaribio ya kutenda makosa ya usafirishaji wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa majaribio ya kutenda makosa chini ya Sheria hii yanawekewa adhabu.

Kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha kosa la kutoa taarifa binafsi za wahanga wa usafirishaji wa binadamu. Marekebisho haya yanalenga kuzuia utoaji wa taarifa za wahanga kinyume na sheria na kuhakikisha kuwa maisha binafsi na utambulisho wa wahanga unalindwa. Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kuwezesha taarifa kuhusu makosa ya usafirishaji wa binadamu kutolewa na mtu yeyote badala ya mhanga pekee. Marekebisho haya yana lengo la kutoa kwa kila mtu jukumu la kutoa taarifa za utendaji wa makosa kwa mamlaka husika. Kifungu cha 12 kinarekebishwa ili kumpa mtu yeyote anayemkamata mshukiwa wa usafirishaji wa binadamu jukumu la kumfikisha mtu huyo katika kituo cha polisi kilicho karibu.

Kifungu cha 26 kinarekebishwa ili kuwezesha mapato yanayotokana na mali zilizokamatwa au kutaifishwa katika utendaji wa makosa chini ya Sheria hii kuwekwa katika Mfuko wa Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu. Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa idadi ya watu wanaoweza kuteuliwa kuhudumu katika Sekretarieti ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu. Marekebisho haya yanalenga kumuwezesha Waziri kuamua na kuteua idadi ya watu watakaohudumu katika Sekretarieti kulingana na wajibu na majukumu ya Sekretarieti. Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuongeza mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Kamati ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu na kuainisha muda wa kushika madaraka kwa wajumbe wa Kamati hiyo. Kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahsusi haijaainishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa makosa yote chini ya Sheria yanawekewa adhabu.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95. Kifungu cha 2

kinarekebishwa ili kuweka tafsiri ya msamiati "*substance with drug related effect*" ambao umetumika katika masharti mbalimbali lakini haujapewa tafsiri katika Sheria. Lengo ni kuondoa uwezekano wa kutafsiriwa vinginevyo wakati wa utekelezaji wa Sheria. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuvitaka vyombo vingine vyovyote vyenye mamlaka ya kutoa vibali au leseni katika shughuli ya dawa kuitaarifu Mamlaka kabla ya kutoa vibali au leseni. Marekebisho haya yana lengo la kuondoa ukiritimba katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka katika kudhibiti dawa za kulevya. Kifungu cha 14 kinarekebishwa ili kujumuisha katika masharti yake dawa ambazo zimezuiliwa chini ya sheria nyingine yoyote. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa dawa zote za kulevya zinadhibitiwa.

Vifungu vya 15 na 15A vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza uzito wa bangi na mirungi kwenye makosa yanayosikilizwa katika Mahakama Kuu au Mahakama za Wilaya. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza mrundikano wa kesi Mahakama za Wilaya zinazosubiri kupelekwa Mahakama Kuu kwa ajili ya kusikilizwa. Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kufanya kuwa kosa la jinai kitendo cha kukutwa na au kutumia kiwango kidogo cha dawa za kulevya. Kwa sasa, Sheria inazuia kitendo hicho bila kutamka kuwa ni kosa la jinai.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, Sura ya 366, ambapo kifungu cha 2 kinachohusiana na matumizi ya Sheria kinarekebishwa ili kuiondoa Idara ya Uhamiaji katika wigo wa Sheria hiyo. Marekebisho haya yanatokana na hatua ya Idara ya Uhamiaji kutambulika kama Jeshi.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sura ya 180, ambapo kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kumuwezesha Mkurugenzi kutoa miongozo kwa ajili ya ukuaji na usimamizi wa masuala mbalimbali yanayohusu nyanda za malisho na vyakula vya wanyama. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuweka sifa sahihi za kitaaluma za mtu kuteuliwa kama mkaguzi wa vyakula vya wanyama au wa nyanda za malisho.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54, ambapo kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa lengo la kuongeza tafsiri ya neno "Wizara" ambalo limetumika katika masharti mbalimbali ya Sheria lakini halijatafsiriwa kwa sasa. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi na kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni za kuainisha haki na stahili mbalimbali kwa maafisa uhamiaji kama za majeshi mengine chini ya Wizara. Aidha, inapendekezwa kubaki na dhana ya "Idara" katika Sheria badala ya kubadili jina

kuwa "Jeshi la Uhamiaji" ili kuendeleza taswira ya kidiplomasia ya Idara katika jumuiya ya kimataifa.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421. Kifungu kipya cha 10A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Bodi ya Nyama kukasimu utekelezaji wa baadhi ya majukumu yake kwa mamlaka za serikali za mitaa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa majukumu ya Bodi yanatekelezwa hata katika ngazi za serikali za mitaa. Vifungu vipya vvya 13A na 13B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uanzishaji wa kanda na uteuzi wa wakaguzi. Uanzishaji wa kanda za tasnia ya nyama unaopendekezwa unalenga kuhakikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Bodi.

Aidha, kifungu cha 13B kinachopendekezwa kinalenga kumpa Waziri mamlaka ya kuteua wakaguzi wa nyama kutoka miongoni mwa wataalamu wa mifugo na sayansi ya chakula watakaotekeleza majukumu katika maeneo yao husika. Kifungu cha 16 kinarekebishwa ili kujumuisha miongoni mwa majukumu ya Msajili, jukumu la kutunza rejesta ya wadau wengine wa tasnia ya nyama ambao hawajatajwa katika kifungu hicho. Vilevile kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuwataka wadau wote wa nyama kusajiliwa na Bodi kabla ya kufanya shughuli yoyote ya kibiashara katika tasnia ya nyama. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa shughuli zote za kibiashara katika tasnia ya nyama zinasimamiwa na Bodi na wadau wote wanasajiliwa.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241, ambapo kifungu cha 19A kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha mafao anayostahili kulipwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371, ambapo kifungu cha 40 kinarekebishwa kwa kumjumuisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji katika masharti ya kifungu hicho. Marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha kuwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anapokea stahili sawa na wakuu wa majeshi mengine yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260, ambapo kifungu cha 3 kinafanyiwa marekebisho ili kuongeza tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria. Kifungu cha 4 kinarekebishwa ili kuitambua TAWIRI kama taasisi kiongozi katika masuala ya utafiti wa wanyamapori. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa utafiti wowote kwenye wanyamapori unafanywa kwa usimamizi wa TAWIRI. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua

wigo wa majukumu ya TAWIRI kwa kujumuisha, miongoni mwa mambo mengine, utoaji wa ushauri wa kisayansi kuhusu wanyamapori walio katika hatari ya kupotea na kufanya sensa ya wanyamapori.

Vifungu vya 10 na 11 vinarekebishwa kwa kuongeza adhabu iliyoainishwa kwa vitendo vya ukiukaji wa masharti ya vifungu hivyo. Marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa adhabu inayowekwa inazuia vitendo vya uvunjifu wa sheria. Aidha, vifungu vipya vya 11A na 11B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu hakimiliki katika ugunduzi katika tafiti za wanyamapori na zuio la uchapishaji wa tafiti. Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa haki zote zinazotokana na ugunduzi katika tafiti za wanyamapori zinalindwa na tafiti za wanyamapori zinachapishwa baada tu ya kupata idhini ya TAWIRI.

Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza kanuni ili kujumuisha maeneo ambayo yanaweza kuhitaji kufafanuliwa zaidi katika Kanuni. Kifungu kipya cha 13A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka utaratibu wa rufaa kwa mtu asiyeridhika na maamuzi ya Taasisi. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha sifa za mtu kuteuliwa kama Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI pamoja na majukumu yake. Kifungu cha 21 cha Sheria kinarekebishwa ili kutambua fedha na michango inayotoka katika Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato ya TAWIRI.

Dodoma,
18 Agosti, 2021

ADELARDUS L. KILANGI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. PROF. ADELARDUS L. KILANGI, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)(NO. 5) ACT, 2021"**

*(Made under S.O. 99 (10))*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Act, 2021" is amended as follows:

**A:** In Clause 31-

(a) in the proposed section 13(A) (1), by deleting the words "meat industry zones" and substituting for them the words " zonal offices";

(b) in the proposed section 13(A) (2), by deleting the word " zones" and substituting for it the word "zonal offices"; and

(c) in the proposed section 13(B), by inserting the word "industry" between the words "meat" and "inspectors" wherever they appear.

**B:** In Clause 43 (b) by deleting the phrase "five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings" appearing in the proposed subsection (2) and substituting for it the phrase "two million shillings but not exceeding five million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding two years".

**C:** In Clause 44-

(a) in paragraph (b) by deleting the phrase "five hundred thousand shillings but not exceeding one million shillings" and substituting for it the phrase "two million shillings but not exceeding seven million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding three years"; and

(b) in paragraph (c) by deleting the word "withdrawn" appearing in the proposed subsection (3) and substituting for it the word "revoked".

Dodoma, **ALK**
.........................., 2021 *AG*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuwasilisha vizuri kabisa kwa umakini mkubwa yale yaliyojiri upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ili atupitishe yale yaliyojiri kwa upande wa Kamati ya Bunge. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. Karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naomba Taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) ya Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act (No. 5) of 2021)*. Ambao ulisomwa kwa Mara ya Kwanza tarehe 31 Agosti, 2021 wakati wa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi la Mbili kwa kuzingatia masharti ya Kanuni 93 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilijadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kuwashukuru wadau wetu ambao ni Taasisi ya *Tangible Initiative for Local Development (TIFLD)* na Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Law Society)* kwa maoni yao yenye tija ambayo yameiwezesha Kamati kupambanua masuala ya msingi

katika kuchambua na kushauri ipasavyo kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) ya Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Act*, 2021*)* unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria 9 kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizi. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu ni kama ilivyobainishwa kwenye Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa Muswada na nitaanza maudhui ya jumla. Kamati imefanya uchambuzi kwa kupitia sehemu 10 za Muswada huu wenye jumla ya Sheria 9 ambazo zinajumla ya Ibara 49 za marekebisho kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii ya kuchambua Muswada ilizingatia desturi ya Kibunge duniani inayotambua dhima ya Kamati katika Miswada ya Sheria kwa kuwa Muswada huu unagusa sekta zaidi ya moja. Kamati iliongeza umakini na kuzingatia maoni ya wataalam na wabobezi wa masuala ya Kibunge ili kufanya uchambuzi unaotosheleza kuwezesha uamuzi bora wa Kibunge.

Mheshimiwa Spika, mfano wa maoni ya kitaalamu kuhusu utaratibu ni maelezo ya mtaalamu wa Bunge la Uingereza ambaye alisema, nayanukuu *"The function of Committee on a Bill is to consider the Bill clause by clause and if it wishes, word by word and to modify it to reflect the Committee's legislative intentions"* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri hiyo isiyo rasmi tunaweza kusema kuwa kazi ya Kamati katika Muswada ni kuangalia kwa kufikiria Ibara kwa Ibara na kama itapenda, neno kwa neno na kuthibitisha maandishi yaliyomo katika Muswada au kuyarekebisha ili kuakisi dhamira ya Kamati katika utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, mtaalamu mwingine ambaye maoni yake kwenye chapisho lake yalizingatiwa ni Profesa Griffith wa Chuo Kikuu cha London Uingereza ambaye mtaalamu huyo alisema, naomba ninukuu *“The purpose of going through the text of a Bill is to make amendments, that will render the Bill more generally acceptable”* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kutafsiri hayo tunaweza kusema kuwa madhumuni ya kupitia maandishi kwenye Muswada na kuyatafakari ni kufanya marekebisho yatakayoweza kuwa na misingi ya jumla inayokubalika. Maoni hayo ya Wataalamu na Waandishi yanathibitisha utaratibu uliotumiwa na Kamati katika uchambuzi wa jumla. Kamati ilibaini kuwa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria 9 yaliyobainishwa kwenye jumla ya Ibara 49 za Muswada, ambapo uchambuzi wa Kamati ulibaini masuala 9 ya majadiliano kwa muktadha wa jicho la uwakilishi wa wananchi ambapo masuala hayo ni kama yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Moja, Ibara ya 4 inayopendekeza marekebisho ya tafsiri katika Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu Sura ya 432. Ambayo inajumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, Uhamiaji, Ustawi wa Jamii, Kazi na Ajira, Serikali ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu katika dhana ya huduma za usalama *(Security Service)*.

Mheshimiwa Spika, Pili, Ibara ya 5 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432 ambapo inaweka masharti ya kesi zinazohusu usafirishaji haramu wa binadamu kusikilizwa na Mahakama Kuu. Tatu, Ibara ya 6 inayopendekeza nyongeza ya Kifungu kipya cha 8A katika Sheria hiyo hiyo ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, ambayo inaweka adhabu dhidi ya kujaribu kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu ambapo awali hazikuwepo.

Mheshimiwa Spika, Nne, ni Ibara ya 16 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 4 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambayo inaweka masharti kwa vyombo vyenye mamlaka ya kutoa vibali au leseni katika shughuli za dawa, kutakiwa kuitaarifu Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya tofauti na ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ya Tano ni Ibara 28 ambayo inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 kwa kuitambua Idara ya Uhamiaji kama Jeshi tofauti na ilivyo sasa, kwa kuiwekea utaratibu wa Kijeshi bila kubadilisha jina.

Mheshimiwa Spika, Sita ni Ibara ya 31 ambayo inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 13 cha Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421. Kwa kuanzisha vifungu vipya vya 13A na 13B vyenye kuanzisha Kanda za Viwanda vya Nyama nchini na kuweka msingi wa kutoa miongozo kwa ajili ya ukuaji na usimamizi wa masuala yanayohusu nyanda za malisho na vyakula vya wanyama.

Mheshimiwa Spika, Saba ni Ibara ya 36 ambayo inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 19A cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, kwa kujumuisha mafao anayostahili kulipwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, sambamba na utaratibu unaotumika kwa mafao ya IGP na Kamishna Generali wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, Nane ni Ibara ya 41 ambayo inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260, kwa kuongeza tafsiri ya misamiati mipya ikiwepo kutambua kifupisho cha *TAWIRI* kuwa ni Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania na hivyo kuipa mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa tafiti za tasnia ya wanyamapori nchini.

Mheshimiwa Spika, Tisa ni Ibara ya 49 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 21 cha

Sheria hiyo ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Sura ya 260, inayoongeza vyanzo vya mapato ya *TAWIRI* kuwa ni pamoja na michango kutoka kwenye Mfuko wa Udhibiti wa Wanyamapori Tanzania *(Tanzania World life Protection Fund)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuridhia ufafanuzi wa mtoa hoja kuhusu masuala hayo. Hata hivyo, kuhusu suala la kubadili hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi kwa kuiwekea utaratibu wa Kijeshi, Kamati ilibaini kuwa ni suala mahsusi lenye kuhitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa mtoa hoja, kwa msingi wa hoja zinazobainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maudhui ya jumla ya Muswada. Kama nilivyoeleza hapo juu, Kamati iliridhia maudhui yote ya mapendekezo ya marekebisho ya Muswada huu, lakini pia kwa kuzingatia msingi wa hoja zifuatazo: -

(a) Ibara ya 4 inayopendekeza marekebisho ya tafsiri ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, inajumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, Uhamiaji, Ustawi wa Jamii, Kazi na Ajira, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu katika dhana ya huduma za usalama *(security service).* Kamati ilibaini kuwa ujumuishaji wa taasisi hizo unatokana na ukweli kuw udhibiti wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ni jukumu lenye kujumuisha wadau wengi kutoka taasisi shirikishi za Serikali kutokanana uhalisia wa jambo lenyewe. Aidha, taasisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Afisa wa Ustawi wa Jamii tayari wanatambuliwa kwenye Kifungu cha 3 cha Sheria hiyo.

(b) Ibara ya 5 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 6 cha Sheria hiyo ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, ambayo inaweka masharti ya kesi zinazohusu usafirishaji haramu wa binadamu kusikilizwa na Mahakama Kuu. Kamati ilibaini marekebisho yamezingatia

ukweli kuwa, unyeti wa kesi hizo unahitaji kusikilizwa na Mahakama Kuu kwa mujibu wa sheria.

(c) Ibara ya 6 inayopendekeza nyongeza ya Kifungu kipya cha 8A katika Sheria hiyo hiyo ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, Sura ya 432, ambayo inaweka adhabu dhidi ya kujaribu kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu ambapo awali hazikuwepo. Kamati ilibaini kuwa pendekezo hilo ni kwa lengo la kuongeza udhibiti wa makosa hayo ambayo ni hatari kwa afya na usalama wa taifa na wananchi wake.

(d) Ibara ya 16 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 4 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95, ambayo inaweka masharti kwa vyombo vyenye mamlaka ya kutoa vibali au leseni katika shughuli za dawa kutakiwa kuitaarifu Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya tofuti na ilivyo kwa sasa. Kamati ilibaini kuwa pendekezo hilo linakusudia kuongeza udhibiti kwa vyombo hivyo ili visitumike vibali au leseni za shughuli za dawa kupitisha baadhi ya dawa zenye sifa za kuwa dawa za kulevya.

(e) Ibara ya 19 inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 15A cha Sheria hiyo ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95, ambayo imeweka ukomo wa adhabu ya chini kwa mtu atakayekamatwa na dawa za kulevya pamoja na kuweka ukomo wa uzito wa bangi au mirungi kwa lengo la kutofautisha kesi zitakazosikilizwa katika Mahakama Kuu na kesi zile zitakazosikilizwa katika Mahakama za Wilaya au za Hakimu Mkazi. Kamati ilibaini kuwa, pendekezo hili litapunguza mlundikano wa majalada ya kesi kwenye Mahakama Kuu ambazo zinaweza kushughulikiwa katika Mahakama za Wilaya au za Hakimu Mkazi.

(f) Ibara ya 31 inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 13 cha Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421, ambapo pamoja na mambo mengine muhimu, inaweka msingi wa kutoa miongozo kwa ajili ya ukuaji na usimamizi wa masuala yanayohusu nyanda za malisho na vyakula vya

wanyama. Kamati ilibaini kuwa marekebisho hayo yataimarisha usimamizi wa nyanda za malisho na vyakula vya wanyama kwa ustawi wa tasnia hiyo.

(g) Ibara ya 41 inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260, ambayo inatambua kifupisho cha *TAWIRI* na kumaanisha kuwa ni Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, ambapo Kamati ilibaini nia ya marekebisho hayo ni kwa ajili ya kutambua kifupisho hicho kwa mujibu wa sheria na hivyo kuipa taasisi hiyo mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa utafiti za tasnia ya wanyapori nchini.

(h) Ibara ya 43 inayorekebisha Kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura ya 260, inayoongeza adhabau ya faini kutoka 10,000 hadi 50,000 kwenda 500,000 hadi 1,000,000 kwa kosa la kutotoa taarifa za utafiti kwa Taasisi ya Utafiti. Kamati ilibaini kuwa, Sheria hii ilitungwa mwaka 1980, na kwa kipindi hicho adhabu ya shilingi 10,000 ilikuwa inaendana na wakati huo. Hivyo kwa wakati huu ambapo ni takriban miaka 41 tangu kutungwa kwa sheria hiyo, maoni ya Kamati ni kuwa upo ulazima na umuhimu wa kuhuisha viwango vya adhabu kulingana na wakati wa sasa na thamani ya pesa.

Aidha, adhabu hiyo imewekwa kwa lengo la kuongeza udhibiti wa tafiti zisizotakiwa dhidi ya wanyamapori wetu, hali ambayo isipodhibitiwa kwa adhabu inaweza kuathiri taswira ya raslimali hiyo.

(i) Ibara ya 49 inabainisha vyanzo vya Mapato ya *TAWIRI* kuwa ni pamoja na michango kutoka kwenye Mfuko wa Udhibiti wa Wanyapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Protection Fund),* ambapo Kamati ilibaini kuwa, pendekezo hilo lina lengo la kutumia sehemu ya michango inayotokana na kazi ya tasnia hiyo kuchangia gharama za uendeshaji wa Taasisi hiyo kwa nia ya kupunguza utegemezi na kuongeza ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa yafuatayo ni Maoni ambayo ya Uchambuzi wa Kamati Kuhusu Suala la Kubadili Hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi katika Ibara ya 28(3) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kikao cha majadiliano baina ya Kamati na Serikali kilichofanyika tarehe 4 Septemba, 2021, Kamati ilibaini Ibara ya 28(3) ya Muswada unaotajwa hapo juu inapendekeza kubadili hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi lenye hadhi sawa na majeshi mengine ya nchi, na hivyo idara hiyo itawaliwe na uendeshaji wa kijeshi kama ilivyo kwa majeshi mengine; na kwa mantiki ya uboreshaji wa motisha za watumishi wa idara hiyo. Kamati ilikubaliana na nia njema ya Serikali kuhusu mapendekezo ya kuboresha haki na maslahi ya watumishi hao wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa suala hili uliibua maoni ya Kamati ambayo yalijikita kwenye athari tatu zifuatazo:-

(a) Hadhi ya kijeshi kwa Idara ya Uhamiaji katika mahusiano ya kimataifa;

(b) Idara ya Uhamiaji kutotajwa kwenye orodha ya tafsiri ya mwanajeshi kwa mujibu wa Ibara ya 147(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(c) Iwapo matakwa ya kisheria yalizingatiwa katika utekelezaji wa maamuzi hayo ndani ya mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia msingi wa hoja hizo, Kamati ilimshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajibu hoja hizo kwa maandishi kuhusu maudhui yaliyobainishwa kwenye Ibara ya 28(3) ya Muswada kwa lengo la kuiwezesha Kamati kubaini kama yalizingatia hatua zote za kiserikali ikiwemo kibali cha Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, mapendekezo

ya Ibara ya 28(3) ya Muswada ni maamuzi ya Serikali na kuwa yalizingatia hatua zote kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati iliridhia mapendekezo ya Serikali kuhusu Ibara ya 28(3) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo sasa ni maoni na ushauri wa kamati kwa ufupi kabisa. Kama nilivyoeleza katika sehemu ya maudhui na uchambuzi, kwamba Kamati inakubaliana na nia njema ya mependekezo ya marekebisho katika Muswada huu, kwa kuwa yanakusudia kuondoa mapufungu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Hata hivyo, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kubadili hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi ambayi ni *Special Issue;* pamoja na melezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mbele ya Kamati kuwa hatua zote za kiserikali zilizingatiwa katika kufikia maamuzi ya Ibara ya 28(3) ya Muswada huu kuhusu kubadili hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi, busara za Kamati zimeona ni vyema Bunge lako Tukufu libaini maoni ya Kamati kuhusu mazingira ya suala hilo kwa kuzingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ustawi wa Taifa letu na kwa faida ya vizazi vilivyopo na vizazi vijavyo. Hivyo, kwa muktadha huo, maoni ya Kamati kuhusu suala hili ni kama ifuatavyo:-

(i). Serikali ione umuhimu wa kufanyia marekebisho Ibara ya 147(4) ya Katiba ya Nchi kwa lengo la kujumuisha Idara ya Uhamihaji pamoja na majeshi mengine ambayo hayatambuliki katika Ibara hii kuwa moja ya majeshi ya nchi kwa mujibu wa Katiba;

(ii). Pamoja na Ibara ya 151 ya Katiba kutoa tafsiri pana ya neno *'Jeshi',* bado kuna umuhimu wa Idara ya Uhamihaji pamoja na majeshi mengine yatakayoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 151 ya Katiba kujumuishwa na kutambuliwa katika Ibara ya 147(4) ya Katiba kwa lengo la kulinda maslahi ya wanajeshi wa majeshi hayo kwa mujibu wa Katiba ya nchi;

(iii). Serikali iweke mfumo mzuri na ulio wazi kisheria wa kushughulikia masuala ya ndani ya nchi yenye kuhusisha mataifa mengine kwa lengo la kulinda taswira ya nchi katika mahusiano ya kidiplomasia na mataifa mengine; na

(iv). Serikali ione umuhimu wa kutumia mfumo wa Hati Idhini ya Rais iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali, kama kiongozi mkuu namba moja wa Sekta ya Utumishi wa Umma na Serikali kwa taasisi zote nchini, ambaye pia ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, ili hati hiyo iwe mwongozo katika hatua zote za kubadili hadhi au muundo wa taasisi na vyombo vyote vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vilivyoanzishwa kwa misingi ya Katiba, kabla ya hatua ya utungaji wa sheria yenye kunzisha au kubadili hadhi au muundo wa taasisi na vyombo hivyo vyenye hadhi ya kikatiba kwa lengo la kulinda misingi ya utawala wa katiba kama sheria mama, kwa maslai mapana ya nchi na kwa ustawi wa vizazi vilivyopo kwasasa na vizazi vitakavyofuata.

Mheshimiwa Spika, kihusu maoni na ushauri wa kimaandishi Kamati ilibaini baadhi ya ibara zenye kuhitaji maoni ya Kamati kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi wakati wa utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya 4(b) inayojumuisha maneno *'forced marriage'* au *'forced begging'* kuwa moja ya biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu. Maoni ya Kamati ni kuwa, pamoja na uwepo wa uwezekano wa mtu kutumia mazingira hayo kufanya biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu lakini Serikali ione umuhimu wa kuandaa mwongozo wa kanuni kuhusu kubainisha mazingira hayo kwa lengo la kuepusha matumizi mabaya ya tafsiri hizo dhidi ya baadhi ya jamii, ambazo uamuzi wa kuoa au kuolewa bado unafanywa na wazazi. Au kwenye jamii ambazo vitendo vya ombaomba ni sehemu ya maisha ya kila siku kwa baadhi ya wanajamii. Msisitizo wa Kamati upo kwenye uangalifu wa utekelezaji wa tafsiri hizo ili kuepusha kuingilia maisha ya kila siku ya wanajamii, ambayo si kosa linalokusudiwa na Bunge kwa mujibu wa marekebisho haya.

(b) Ibara ya 44(c) inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 11, kwamba pamoja na adhabu inayotolewa chini ya Kifungu kidogo cha 2, mtu aliyehukumiwa anaweza kunyang'anywa kibali cha utafiti *(withdrawn)*. Kamati inashauri Ibara hiyo ifanyiwe marekebisho ili mtu akishahukumiwa, kibali chake cha utafiti kifutwe. Hivyo neno *withdrawn* libadilishwe na kuandikwa neno *revoked.*

Mheshimiwa Spika, naomba ni hitimishe taarifa hii kwa mara nyingine tena kwa kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili iweze kuufanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Profesa Adelardus Lubango Kilangi bila kumsahau Ndugu Onorius Njole Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (*CPD*) kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wadau wetu wote waliotoa maoni yao katika Kamati kwa ajili ya kuboresha Muswada huu. Hakika, Kamati ilifaidika kwa kiasi kikubwa sana na maoni hayo.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa ambayo wamefanya ya kuchambua Muswada huu. Naomba na majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa Muswada huu na utaratibu wa shughuli za Kamati. Nawashukuru pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald S. Magili na wanasheria wa Bunge, Ndugu Matamus Fungo na Ndugu Evelyne Shibandiko.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nawashukuru sana Katibu wa Kamati ya Katiba na Sheria Ndugu Stanslaus Kagisa pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Yohana Mwakibibi waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na utaratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yote hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuukubali, kuujadili na kuupitisha Muswada huu kwa utekelezaji bora zaidi wa sheria hizo na kwa manufaa mapana ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 2) WA MWAKA 2021 (*THE WRITTEN LAWS MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, (NO. 2) 2021)* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu ya Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2021 **(*The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, No.2 of 2021)***.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2021 **(*The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, (No. 2)2021)* ulisomwa** Bungeni Mara ya kwanza tarehe 12 Februari, 2021 wakati wa Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Pili wa Bunge wa Bunge la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge** uliuleta

Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maudhui na umuhimu wa Muswada huo Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya **Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.** Hivyo, Jumla ya Taasisi Saba zisizokuwa za Kiserikali (CSOs) ziliwakilishwa na jumla ya Watendaji Arobaini ambao walifika mbele ya Kamati tarehe 19 Agosti, 2021 kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhusu Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa na Muswada huu. Majina ya taasisi hizo yamebainishwa katika taarifa hii.

### 1.1 Hatua ya kupokea Maoni ya Wadau

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyotangulia kubainisha hapo juu, Kamati ilipima na kubaini umuhimu wa maoni ya Wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu, na hivyo, kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,** na kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, taasisi Kumi zisizo za kiserikali zilitumiwa barua za Mialiko ambapo Jumla ya Watendaji Arobaini (40) kutoka taasisi sita(6) zilizothibitisha kushiriki, walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha maoni yao. Majina ya Taasisi hizo ni kama yalivyobainishwa kwenye taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wadau wetu wote kwa ushiriki wao pamoja na maoni yao yenye tija ambayo yameiwezesha Kamati kupambanua masuala ya msingi katika kuchambua na kushauri ipasavyo kuhusu maeneo mbalimbali yenye kuhitaji maboresho kwenye Muswada huu.**

## 2.0 YATOKANAYO NA UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Sheria zinazopendekezwa Kufanyiwa Marekebisho pamoja na maudhui ya jumla kwa kila Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mtoa Hoja alieleza Kamati Kuwa, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali

(Na. 2) wa Mwaka 2021 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Mbili (12) kwa lengo la kurahisisha utekelezaji madhubuti wa Sheria hizo na kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu pamoja na maudhui ya jumla kwa kila Sheria ni kama ilivyobainishwa kwenye taarifa hii.

2.2 **Masuala Mahsusi Ya Kiuchambuzi Yaliyobainika**

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuliwezesha Bunge lako Tukufu kubaini maeneo ya kisheria yenye hoja mahsusi kwa ajili ya kushauri ipasavyo, Kamati ilichambua na Kujadili jumla ya Ibara 83 zilizo kwenye Muswada huu na kubaini **Jumla ya masuala sita (6) kwenye Sheria sita (6) kati ya 12** zinazorekebishwa katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano ya kina baina ya Serikali na Kamati, suala la Sita (6) ambalo awali lilihusu kuondoa Ukomo wa Makatibu Wakuu kuendelea kutekeleza majukumu ya Bodi pale ambapo Bodi hizo zinakuwa hazipo, yaliyopendekezwa katika **Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation Act, Cap.1*), Sehemu hiyo imeondolewa na hivyo suala hilo halitokuwa sehemu ya hoja za Kamati kwa mujibu wa taarifa hii.**

**Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwasilishe Masuala Mahsusi Matano (5)** ambayo ni vyema Bunge likayapima ili yazingatiwe wakati wa kupitisha Muswada huu. Masuala hayo ni:-

a) Kamati za Maadili za Mawakili za Mikoa zinazopendekezwa kuanzishwa kwenye **Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (*The Advocates Act, Cap.341*),** zimepewa mamlaka sawa na Kamati ya Taifa (*National Advocates Committee) katika utoaji wa adhabu kwa Mawakili ikiwemo adhabu ya kumwondoa Wakili kwenye rejesta ya Mawakili. Hivyo, sheria imetengeneza mazingira ya* matumizi mabaya ya mamlaka

kwa Kamati za Mikoa hali ambayo inaweza kuathiri ajira za Mawakili;

b) Marekebisho yanyopendekezwa katika **Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108** (*The Birth and Deaths Registration Act, Cap.108*); hayajabainisha nani atapewa kipaumbele zaidi kwa wanafamilia wanaotakiwa kuchukua cheti cha Kifo cha Marehemu. Na hivyo, kuacha ombwe la kisheria kuhusu nani atapewa kipaumbele cha kuchukua hicho cheti kati ya mwenza ,au watoto au ndugu wengine wa marehemu **na kama ni mtoto je ni mtoto wa ndani ya ndoa au nje ya ndoa au wa kulea,** hali ambayo inaweza kusababisha mitafaruku kwenye familia wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

c) Adhabu zinazopendekezwa kwenye **Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 (*The Business Names (Registration) Act, Cap 213*);** hazijawekewa kiwango cha chini. Hali hiyo, kwanza inaweza ikasababisha utoaji wa adhabu tofauti kwa watu wawili au zaidi waliofanya kosa linalofanana lakini pia mazingira hayo ya kisheria yanaweza kuchochea vitendo vya rushwa kwa watoa haki.

**d) Mheshimiwa Spika**, marekebisho yanayopendekezwa **katika Sheria ya Mahakama za Hakimu, Sura ya 11** yanahusu kuruhusu Mawakili wa kujitegemea na wale wa Serikali kuwawakilisha wateja wao kwenye Mahakama za Mwanzo ambazo zinasimamiwa na Mahakimu Wakazi wenye shahada. Aidha, marekebisho haya pia yanapendekeza kuwandoa wazee wanaotoa ushauri katika Mahakama za mwanzo *(Assessors)* kwasababu za uwepo wa Mahakimu wenye shahada ya Sheria pamoja na uwepo wa uwakilishi wa Mawakili.

**Mheshimiwa Spika, kutokana na maudhui hayo, Kamati ilibaini mambo mawili ya mjadala kuhusiana na marekebisho hayo. Mambo hayo ni:-**

a) Uanzishwaji wa mfumo wa utoaji haki wenye kuruhusu haki ya uwakilishi wa Mawakili katika mahakama za Mwanzo.

Hatua hiyo inapongezwa kwakuwa imezingatia ushauri wa Kamati wa muda mrefu kuhusu upatikanaji wa haki ya uwakilishi katika Mahakama za Mwanzo. Hivyo, maoni ya Kamati ni kuwa, utekelezaji wa marekebisho hayo utasogeza karibu huduma za utoaji haki kwa wananchi wengi zaidi katika ngazi za Vijiji, kata na tarafa zenye huduma za mahakama za mwanzo, hali ambayo itarahisisha utoaji haki nchini; na

e) Pendekezo la kuwandoa wazee wanaotoa ushauri katika Mahakama za mwanzo *(Assessors)* kwasababu za uwepo wa Mahakimu wenye shahada ya Sheria pamoja na uwepo wa uwakilishi wa Mawakili, liliibua mjadala wa kina na hivyo kuhitaji kufanyiwa marekebisho**.**

**Aidha, Kamati ilibaini uwepo wa ombwe la kisheria katika mfumo uliopo kwasasa ambao unaruhusu Wazee hao kuendelea kuwepo mahakamani hata pale wanapokuwa hawahitajiki kwa kuzingatia aina ya shauri llililopo mahakamani, ni eneo ambalo lilihitaji kuboreshwa ili kuanzisha mfumo rasmi utakaohakikisha ulazima wa uwepo wa Wazee hao kwenye mashauri yanayohitaji ushauri wao**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kukosa maoni ya wadau wenye kupinga pendekezo hili la Serikali la kuwaondoa wazee washauri katika Mahakama za Mwanzo, uchambuzi wa Kamati pamoja na majadiliano baina ya Kamati na Serikali yalibaini dosari kuwa, mfumo unaopendekezwa na marekebisho haya, haukubainisha mfumo wa kuwarejesha Wazee washauri wa Mahakama pale ambapo kunakuwepo shauri mbele ya mahakama lenye kuhitaji ushauri wao. Hivyo, Kamati ilishauri marekebisho yafuatayo: -

(i) Sheria ibainishe mfumo mpya wa kisheria na kiuratibu utakaoendelea kuwatumia Wazee washauri wa Mahakama kwa kuzingatia ukweli kuwa, kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu wazee hao walikuwa bado ni wa muhimu kwa usuluhishi wa migorogoro hususan inayohusu mirathi na ndoa yenye kutokana na misingi ya Mila, desturi na imani za dini

na kwa kuzingatia uelewa wa Wananchi wetu walio wengi ambao hawana uelewa wa kutosha kuhusu mifumo ya kisheria na taratibu zake; na

(ii) Serikali iandae utaratibu wa kuwalipa haki zao Wazee washauri wa Mahakama ambao watakoma utumishi wao kutokana na kuanza utekelezaji wa marekebisho ya Sheria hii.

f) Waziri amepewa mamlaka mapana katika kupendekeza makosa mengine yenye kuendana na makosa yanayotajwa chini ya **Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 (*The Companies Act, Cap 212,*** kupitia Kanuni atakazotunga***.*** Marekebisho hayo yanampa Mamlaka Waziri yasiyomhusu, hatua ambayo ikiruhusiwa inaweza kutumiwa vibaya katika kuwanyima baadhi ya watu haki za msingi za kujitafutia kipato halali kupitia biashara za Makampuni***.***

**Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, Bunge lako linayo dhima kuhakikisha sheria zinazotungwa zisitoe mwanya wa kuathiri ustawi wa Jamii kwa kutoa Mamlaka mapana kwa Mawaziri ya kubuni makosa bila ukomo na pasipokubainisha misingi ya makosa hayo.**

## 3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika sehemu ya Maudhui na uchambuzi wa Muswada, Kamati inakubaliana na mependekezo ya marekebisho katika Muswada huu, kwa kuwa yana lengo la kuondoa mapufungu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo..

Hata hivyo, wakati wa uchambuzi, Kamati imebaini **Jumla ya masuala ya msingi Kumi na Moja (11) na Jumla ya dosari tano (5) za kiuandishi na Kiuchapaji,** ambapo Kamati ilishauri ipasavyo na wakati wa Kikao cha pamoja na Serikali cha tarehe 23 Agosti, 2021, Serikali iliridhia ushauri wa Kamati na hivyo kuzingatia marekebisho hayo kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho, ambalo ni sehemu ya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo ya awali, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

3.1 **Masuala Mahsusi *(Special Issues)***

**a) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act, Cap.341);**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

(i) Katika ibara ya 7 inayopendekeza marekebisho ya kuongeza kifungu kipya cha 4A katika Sheria inayoanzisha Kamati ya Maadili ya Mawakili ya Mkoa kamati inashauri neno "*Ethics*" liondolewe katika kamati hizo, au neno "*Ethics*" liongezwe katika Kamati ya Taifa kwa lengo kuakisi jina linalotumika na Kamati ya Taifa lilandane na Kamati za Mikoa;

(ii) Mtumishi wa Umma atakayeteuliwa kuwa Katibu wa kamati za Mawakili za Mikoa awe na taaluma ya Sheria ili aweze kuelewa masuala yanayojadiliwa na Kamati ya Mawakili;

(iii)Utaratibu wa kumpata Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati inapotokea hawapo ufafanuliwe vizuri ili kuziba ombwe la kisheria wakati wa utekelezaji wa marekebisho hayo;

(iv)Kamati za Mawakili za Mikoa zisiwe na uwezo wa kutoa adhabu ya kumtoa Wakili katika rejesta ya Mawakili, badala yake Kamati hizo zibakie na Jukumu la kupendekeza adhabu kwenye Kamati ya Mawakili ya Taifa ili kudhibiti matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kuathiri ajira za Mawakili; na

(v) Ibara ya 4A(5) iainishie utaratibu utakaotumiwa na Katibu wa Kamati ya Mawakili ya Mkoa kuwasilisha malalamiko kwa Jaji Mfawidhi wa Mkoa ili kuepuka mlolongo wa malalamiko na kuchelewesha haki kwa mtuhumiwa.

**b) Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 (The Birth and Deaths Registration Act, Cap.108);**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

Katika Ibara ya 10 inayopendekeza marekebisho ya kifungu cha 17 cha Sheria, kufuta maneno "if any" na badala yake kuongeza maneno *"if for any reasons the spouse or child are incapable of collecting the death certificate"* ili kubainisha nani atapewa kipaumbele zaidi kwa wanafamilia wanaotakiwa kuchukua cheti cha Kifo cha marehemu na hivyo, kuondoa ombwe la kisheria kuhusu nani atapewa kipaumbele cha kuchukua hicho cheti kati ya mwenza au watoto au ndugu wengine wa marehemu kwa lengo la kubainisha mfumo wa kumdhibiti mtu asiyetakiwa kuchukua cheti hicho .

**c) Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213,**
**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

Katika Ibara 18 inayopendekeza marekebisho ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213, adhabu ya faini iliyopendekezwa kwa makosa ya jumla iwekewe kiwango cha faini cha chini *(minimum fine)* ili kuepusha mazingira ya *utoaji* wa adhabu tofauti kwa watu wawili au zaidi waliofanya kosa linalofanana lakini pia kuondoa mazingira ya kisheria yanayoweza kuchochea vitendo vya rushwa kwa watoa haki;

**d) Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 (*The Companies Act, Cap. 212*);**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

(i) Katika Ibara ya 30 inayopendekeza marekebisho ya kifungu cha 3 cha Sheria, katika kifungu kidogo cha (5) kufuta maneno "*associated with instances of or"* ili kuwakinga wale

ambao watahusishwa kuhusika na biashara ya utakatishaji fedha, kufadhili ugaidi, biashara ya usafirishaji wa binadamu, usafirishaji wa madawa ya kulevya ingawa hajahukumiwa Mahakamani ili waweza kufungua kampuni; na

(ii) Maneno "*or any other related offences as may be prescribed by the Minister*" ya ondolwe kwenye Muswada ama makosa ambayo Waziri atayataja yatamkwe kwenye Sheria ili *kuhakikisha sheria haitoi Mamlaka mapana kwa Waziri, ya kubuni makosa bila ukomo au pasipokubainisha misingi ya kuzingatiwa kwenye sheria mama inayotungwa na Bunge.*

**e) Sheria ya Mahakama za Hakimu, Sura ya 11**
**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

Ibara ya 54 ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha mfumo mpya wa kisheria utakaoendelea kuwatumia Wazee washauri wa Mahakama pale watakapohitaji, kwa kuzingatia ukweli kuwa, kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu Wazee hao walikuwa bado ni wa muhimu katika usuluhishi wa migorogoro ya kijamii hususan inayohusu mirathi na ndoa yenye kutokana na misingi ya Mila, desturi na imani za dini na kwa kuzingatia uelewa wa Wananchi wetu walio wengi ambao hawana uelewa wa kutosha kuhusu mifumo ya kisheria na taratibu zake.

**f) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 (*The Environmental Management Act, Cap.191*);**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Kamati inashauri Bunge liliridhie marekebisho yafuatayo:-

Katika Ibara ya 42 inayopendekeza kuongeza kifungu kipya cha 194 katika kipengele kidogo (5), jukumu la kuwasilisha taarifa kila robo ya mwaka kuhusu makosa yaliyofifilishwa kwa Msajili wa Baraza la Rufani la Mazingira (*Enviromental Appeal Tribunal*) ni kutoa jukumu ambalo halipo kisheria, na badala yake jukumu hilo apewe Mkurugenzi Mkuu wa Baranza la

mazingira ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Masuala yote ya Mazingira.Maoni ya Kamati ni kuwa, Msajili aliyetamkwa kwenye Sheria ni Msajili wa Baraza la Rufani la Mazingira (*Enviromental Appeal Tribunal*) ambaye anateuliwa na Jaji Mkuu kwa kazi maalum ya kulihudumia baraza la Rufani la na siyo Mtendaji wa baraza la Mazingira wa kudumu, hivyo, anaweza asiwe na taarifa sahihi kama ilivyo kwa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC kuhusu makosa yote yaliyofifilishwa. Hali hiyo ikuruhusiwa, inaweza kuathiri utekelezaji wa marekebisho haya.

3.2 **Dosari za kiuchapaji**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kubaini masuala ya msingi yenye kuhitaji maboresho ya Bunge lako Tukufu, pia ilibaini baadhi ya dosari za kiuchapati na kiuandishi kwenye Jumla ya Sheria Tatu ambazo ni:- Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 (*The Land Disputes Courts Act, Cap.216*) kwenye Ibara ya 51, Sheria ya Mahakama za Hakimu, Sura ya 11(*The Magistrates' Courts Act, Cap. 11*)kwenye ibara ya 55, Sheria ya Utalii, Sura ya 65 (*The Tourism Act Cap.65*) kwenye ibara ya 65 na Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326 (*The Trade and Service Marks Act, Cap.326*)kwenye ibara ya 81.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilizingatia marekebisho hayo kwa kuufanyia Marekebisho Muswada huu kwa kila Sehemu na ibara zote zilizobainika kuwa na dosari au changamoto za utekelezaji, kama yanavyoonekana kwenye **Jedwali la Marekebisho** ambalo ni sehemu ya taarifa hii.

3.3 **Maoni na Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri wa Kamati uliotolewa hapo juu kuhusu masuala ya mahsusi ya kiuchambuzi yaliyobainika katika Muswada huu, pia kupitia mjadiliano ya Wadau pamoja na Serikali, Kamati iliweza kubaini masuala ya kuzingatiwa na Serikali wakati wa kutekeleza Sheria hizi, kama ifuatavyo:-

a) Serikali ihakikishe inawashirikisha wadau wanohusika na Sheria inayokusudiwa kufanyiwa marekebisho au kutungwa

kwa lengo la kuwasilisha Bungeni Miswada ya Sheria yenye mawazo jumuishi na hivyo kuondoa malalamiko ya Wadau kuhusu kutoshirikishwa wakati wa michakato ya maandalizi ya Miswada ya Serikali na hivyo kuepusha ukinzani usiyo kuwa walazima wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo;

b) Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, ishirikiane na Mahakama katika kuhakikisha kuwa, Kanuni zitakazoundwa kuhusu utekelezaji wa Shughuli za Mahakama za Mwanzo zitoe muongozo rasmi kuhusu namna bora ya kusuluhisha migogoro ya mirathi na ndoa kwa wananchi wengi wenye kusimamiwa na mila na desturi pamoja na imani zao za dini pasipokuathiri misingi za imani zao ambayo inatokana na Vitabu vitakatifu wanavyoviamini;

c) Serikali ihakikishe inawalipa haki zao Wazee washauri wa Mahakama ambao watakoma utumishi wao kutokana na kuanza utekelezaji wa marekebisho ya **Sheria ya Mahakama za Hakimu, suara ya 11**;

d) Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, ihakikishe inaweka utaratibu Mzuri kikanuni katika kudhibiti mfumo wa uchukuaji cheti cha Kifo cha Marehemu ili kuhakikisha cheti hicho kisiangukie kwenye mikono ya mtu ambaye ni hatari kwa ustawi wa familia na wategemezi wa marehemu. Aidha, utekelezaji wa utaratibu huo uzingatie na kuheshimu historia ya maisha, mila, desturi, na imani ya Marehemu na familia yake kwa ujumla wake;

e) Vyeti vya Mawakili wa Kujitegemea na Waendesha Mashtaka vifanyiwe maboresho kwa kuondoa masharti yalivyo kwasasa yanayowazuia kusimamia kesi kwenye Mahakama za Mwanzo ili kuwezesha utekelezaji wa marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu**;** na

f) Serikali ihakikishe kuwa, viwango vya adhabu na Tozo vinavyopendekezwa kwenye Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni, viwe ni viwango vyenye uhalisia wa hali halisi ya Wananchi wetu na vizingatie mazingira ya utekelezaji wake. Hatua hiyo iambatane pia na utoaji wa

Mamlaka stahiki kwa Mawaziri na Vyombo vingine, yenye kuzingatia mipaka iliyowekwa Kisheria kwa ajili ya kuzingatia misingi ya utawala bora katika mgawanyo wa mamlaka miongoni mwa mihimili ya Serikali. Maoni ya Kamati ni kuwa, endapo misingi hiyo haitozingatiwa inaweza kuweka mazingira ya kuligombanisha Bunge na Wananchi wake na pia, uzingatiaji huo utaepusha ukinzani usiokuwa wa lazima wakati wa uchambuzi na utekelezaji wa Sheria hizo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili iweze kuufanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Prof. Aderladus Lubango Kilangi, Mb, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof.Palamagamba Mwaluko Kabudi (Mb bila kumsahau Ndugu Onorius Njole Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru Wadau wetu wote waliofika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao kwaajili ya uboreshaji wa Muswada huo. Hakika, Kamati ilifaidika sana na maoni yao ambao kwa kiasi kikubwa yaliwajengea uelewa zaidi Wajumbe katika kuchambua Muswada huu na kushauri ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kuufanyia kazi Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD) pamoja na taarifa yote hii inayowasilisha maoni ya Kamati. Majina ya Wajumbe hao ni:

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uchambuzi wa Muswada huu na uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald S.Magili, na Wanasheria wa Bunge, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Thomas Shawa na Ndg. Rehema Lazarus Kipera.

Kipekee kabisa nawashukuru sana Katibu wa Kamati ya Katiba na Sheria Ndg. Stanslaus Kagisa pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg.Yohana Mwakibibi waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yote hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuukubali, kuujadili na kuupitisha Muswada huu kwa utekelezaji bora zaidi wa sheria hizo na kwa manufaa mapana ya Taifa letu.**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Najma Murtaza Giga, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
1 SEPTEMBA, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga, tunakushukuru sana kwa kupitia maoni ya Kamati vizuri kabisa na kwa ufasaha mkubwa. Sasa tunakwenda katika uchangiaji Waheshimiwa, enhee sasa ngoja ni-*sanitize* kwanza kidogo. Naona sasa tunaingia kwenye hatua nyingine kabisa, Waheshimiwa Wabunge mimi niki-*sanitize* na ninyi mnafanya vivyo hivyo, maana enzi hizi ni enzi za *sanitizer*.

Ahsante tunaanza na Mheshimiwa Agnesta L. Kaiza, atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza, mchokoza mada.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze

kuchangia machache. Kabla sijakwenda katika Muswada naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa jinsi ambavyo ametusimamia kwa weledi na hata tukaweza kufanikisha kudadavua na kuweka sawa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba kwa weledi huu wa mwana mama unatuma ujumbe moja kwa moja kwamba wanawake tukiaminiwa na kukabidhiwa majukumu makubwa na mazito tuna uwezo wa kuyasimamia, kuyafanya na tukaleta matokeo chanya ambayo hayakutarajiwa.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja sasa katika mchango wangu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 inapendekeza katika Kifungu kidogo cha 4 cha Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 kuitambua Idara hii ya Uhamiaji kuwa ni Jeshi kamili bila kubadilisha jina. Natambua nia njema kabisa ya Serikali juu ya jambo hili, lakini niseme kwamba yapo mambo kadha wa kadha ambayo sisi kama Bunge tunapaswa kuyatafakari kabla hatujapitisha Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, suala la majeshi ni suala la Kikatiba. Ninaposema suala la Kikatiba ina maana tunapokuwa tunapitisha Sheria hii hatuna budi kuhakikisha kwamba Sheria hii haiendi kukinzana na Katiba. Kuanzisha au kufuta, kufuta au kuanzisha Jeshi jipya au kulipa hadhi, jambo hili linapaswa kuangaliwa kwa kina kwa maana ya Katiba yetu ya Nchi kwa sababu bila hivyo tunaweza kujikuta tuna-*contradict* Sheria pamoja na Katiba ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitambui Idara ya Uhamiaji kuwa ni miongoni mwa Majeshi katika nchi yetu. Sasa tunapokuwa tunaletewa Muswada kama huu wa kuweza kuipa hadhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimeishaikamata, na Waheshimiwa Wabunge...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** ...kama wanazo katika vishkwambi vyao, unaposema Katiba lazima u-*refer* Katiba wapi na nini, halafu mtu taarifa utakuja baadaye kidogo, ili twende pamoja.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ibara ya 147 Kifungu kidogo cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitambui kabisa...

**SPIKA:** Twende polepole, na dakika zako zinalindwa kabisaa. 147 aah kidogo ili twende pamoja, ehee nimeshafika 147.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, Kifungu kidogo cha 4.

**SPIKA:** Endelea kwa kuisoma.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, sina Katiba, iko wapi Katiba.

**SPIKA:** 147(4) si ndiyo.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo

**SPIKA:** Kwa madhumuni ya Ibara hii mwanajeshi maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Polisi, Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa. Mmmhm.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naweza kuendelea,

**SPIKA:** Mmmhm.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Yupo Msekwa au yupo humu humu ndani? Endelea Mheshimiwa na taarifa yako.

**T A A R I F A**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kama tutaridhia na kuifanya Idara ya Uhamiaji kuwa na hadhi ya Jeshi hatukiuki Katiba kwa sababu Ibara anayoisoma haisomwi peke yake, unaweza kuisoma na Ibara nyingine 2. Kwanza Ibara ya 147(2) inasema; Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza kwa mujibu wa Sheria kuunda na kuweka Tanzania Majeshi ya aina mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukisoma Ibara 151 ya Katiba yetu ambayo ni Ibara ya tafsiri inasema hivi; Jeshi maana yake ni lolote kati ya Majeshi ya Ulinzi na ni pamoja na Jeshi lolote jingine lililoundwa na Katiba hii au kwa Mujibu wa Sheria na linalotawaliwa kwa amri ya Jeshi.

Kwa hiyo Katiba hii Ibara hiyo imetaja lakini haisomwi peke yake maana majeshi haya yaliyotajwa kwenye Katiba lakini na lolote litaloundwa kwa mujibu wa Sheria ya Nchi yetu inayotungwa na Bunge hili. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Agnesta leo unapigwa asubuhi asubuhi tu. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kama kawaida.

**SPIKA:** Jipange vizuri. Dakika zake mmemlindia enhee.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, kwanza niseme kwamba Taarifa hiyo binafsi siipokei kwa sababu *the way* ninavyoendelea kuchangia nitamjibu Mheshimiwa Mbunge ni nani haswa na jambo gani linapaswa kufanyika ili tuweze kupitisha sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema suala zima la kijeshi ni la kikatiba. Sasa unaposema tunakwenda kupandisha Idara ya Uhamiaji kuipa hadhi ya kuwa jeshi kamili wakati katika Ibara 147 haiitambui *which means* yupo mtu...

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Unajua tuna pande mbili na Msekwa, sasa ni vizuri kusema ni nani, sasa nimekuona Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ibara ya 47 kipengele anachosema Mheshimiwa...

**SPIKA:** Taratibu, umesema Ibara ya 47?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Twendeni taratibu, endelea.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, angetakiwa arudi nyuma kidogo asome kifungu kidogo cha (1) na (2) ambacho kinasema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria...

**SPIKA:** Umesema Ibara ya 47 au ngapi?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Ibara ya 47(2) ambayo inasema Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza kwa mujibu wa sheria...

**SPIKA:** Ibara ya 47(2) inasema bila kuathiri masharti...

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Ni Ibara ya 147(2).

**SPIKA:** Ibara ya 147?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Ndiyo.

**SPIKA:** *Okay!* Ile aliyoisoma Mheshimiwa?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Ndiyo, yeye ameruka kifungu anatakiwa arudi juu kidogo, yeye amekwenda chini, arudi kifungu cha (2).

**SPIKA:** Alishapewa taarifa hiyo tayari.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, alipewa Ibara ya 151.

**SPIKA:** Alipewa na hiyo.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Haya sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta, sasa endelea tu maana hiyo…

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nikuombe ulinde muda wangu maana hizi Taarifa zimekuwa nyingi sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unaelimishwa tu usiwe na wasiwasi. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, aliyetoka kunipa taarifa amekiri kwamba Idara ya Uhamiaji haijatajwa katika Ibara hii ambayo nimeitaja *which means* ili tuweze kuipandisha hadhi Idara ya Uhamiaji kuwa jeshi kamili, yapo ya kufuata, yapo ya kuzingatia, ndiyo hayo ambayo nakwenda kuyaelezea.

**TAARIFA**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Eeeee!

**SPIKA:** Unapewa taarifa Mheshimiwa Agnesta.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi ndugu yangu Mheshimiwa Agnesta kwamba Bunge hili linaweza kuyarekebisha hayo kupitia Ibara ya 98(1) ambayo inasema: "Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii kwa kufuata Kanuni zifuatazo:- (a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii (isipokuwa yale yanayohusika na aya ya (b) ya ibara hii ndogo) au masharti yoyote ya Sheria yoyote iliyotajwa katika Orodha ya Kwanza kwenye Nyongeza ya Pili utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe tu hofu kwamba hili jambo linawezekana kwetu wenyewe baada ya sheria kupita na sisi tukaweza kuwaingiza haya majeshi yatakayoongezeka...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika ...kwa mujibu wa Ibara ya 51 waweze kujumuika katika Ibara ya 147. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haiwezekani kumpa taarifa mtoa taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sasa kuna taarifa anapotosha. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Subiri! Inatakiwa kwanza niendelee na Mheshimiwa Agnesta kwanza ndiye aliyepewa taarifa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa niliyonayo ambayo nampa Mwenyekiti wangu naomba niendelee kuchangia hoja yangu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nimesema na narudia kusema kwamba natambua nia njema ya Serikali juu ya jambo hili lakini...

**T A A R I F A**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta unapewa taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Agnesta kwa kurejea Taarifa ya Kamati inayosema yafuatayo, naomba ninukuu, yasionekane ni maneno yangu.

**SPIKA:** Pale wamekosea.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. HALIMA J. NDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati inasema yafuatayo...

**SPIKA:** Kamati walikosea Mheshimiwa Halima. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba niruhusu...

**SPIKA:** Ni makosa ya uchapaji tu. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nitoe taarifa yangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa...

**SPIKA:** Ni makosa ya uchapaji Mheshimiwa Halima, nimeshakupa mwongozo, kwa hiyo, hiyo achana nayo. Mheshimiwa Agnesta endelea.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaaa. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, kaa. Mheshimiwa Agnesta endelea. *(Makofi/Kicheko)*

Nimesikia vizuri, si niko hapa, wewe tulia. Mheshimiwa Agnesta endelea. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea na nimeipokea Taarifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende moja kwa moja katika mchango wangu. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katiba yetu inamtambua kama Amiri Jeshi Mkuu na Katiba inasema Amiri Jeshi Mkuu pale anapoona kwamba kuna hali ya hatari, dharura juu ya jambo fulani la kijeshi ataleta au atatoa kitu kinachoitwa hati idhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uki-*refer* kwenye Taarifa yetu ya Kamati imeongelewa vizuri hati hii kwamba hati idhini kutoka kwa Amiri Jeshi Mkuu ilipaswa kuja kwetu ili ikapate kuwa mwongozo wa Bunge...

**SPIKA:** Nitajie kifungu cha Katiba kinachozungumzia hati idhini, kifungu namba ngapi? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kengele ya kwanza hiyo bado una muda.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ili kuukomboa wakati naomba niendelee kuchangia...

**SPIKA:** Mambo ya Kikatiba hayana kuokoa wakati, likishakuwa la Kikatiba lazima tuwe na uhakika. *(/Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee *please...*

**SPIKA:** Haya, hiyo umeifuta. Endelea basi.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, sijaifuta kwa sababu kutokusema iko sehemu gani haimaanishi kwamba sijui na ndiyo maana nimeiongelea kwa sababu najua ipo. Sasa niseme tu ni wazi kwamba tunahitaji hiki kitu kinachoitwa hati idhini kutoka kwa Amiri Jeshi Mkuu.

**SPIKA:** Lakini umeshindwa kutuambia iko wapi.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nitakuambia kabla sijakaa. Naomba niendelee…

**SPIKA:** Haya mambo yanataka ujipange. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Sawa.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati ya Katiba na Sheria wakati tunajadiliana pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tulihoji ndiyo maana hata hawa wenzangu wanaonipa Taarifa najua mioyoni mwao ninachokisema ndicho wanachokiamini, tulisema na tulimuuliza kwamba tunahitaji kupata ile hati idhini ili iweze kutuongoza lakini…

**SPIKA:** Hiyo kitu yako umeshindwa kutuongoza ni wapi? Unapiga *blah blah theory* hapa, hatutaki *theory,* mradi una-*refer* jambo ambalo ni la Kikatiba unapaswa kutuambia wapi.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, basi naomba niendelee katika jambo lingine.

**SPIKA:** Eeh! Hapo sawa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, lakini naona hilo limepokelewa na limesikika.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tunajadili suala zima la kupandisha Idara ya Uhamiaji kwenda kuwa jeshi kamili lazima tujiulize mambo makuu mawili. Serikali inapaswa kujiuliza kwanza mahusiano yetu ya kimataifa na wenzetu

kule wanatuonaje tunapokuwa tumeibadili Idara ya Uhamiaji kuwa jeshi kamili, tunakuwa tunatengeneza taswira gani kwa watalii na wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, najaribu ku-*imagine* mtalii au mwekezaji anakuja au kule Ubalozini labda anatafuta *documents* au amekuja hapa Tanzania anakutana na Uhamiaji wako *full ...*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta, sasa wewe unataka wakute raia wamekaa kienyeji? Mheshimiwa Simbachawene tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, pengine ili tusikupotezee muda tusichangie wengi nitumie nafasi hii kumuelewesha kwamba tutaonekanaje tukiifanya Idara ya Uhamiaji kuwa jeshi, nimueleze tu, Uingereza Uhamiaji ni jeshi na linaitwa *UK Border Force,* wanatumia silaha na iko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Marekani, India na Australia Uhamiaji ni jeshi. Kwa hiyo, watatuonaje, watatuona tunafanana na wao na tunajitahidi sana kuwa kama wao. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Agnesta hajapitapita huko. Mheshimiwa endelea kuchangia. *(Kicheko)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nimesikia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri lakini ningepewa nafasi ya kuuliza pia na mimi ningeuliza, tulisubiri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ooh, bahati mbaya kengele ya pili imeshalia.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, *this is not fair.*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshalia, tunaendelea na uchangiaji...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja ni-*wind up. (Makofi)*

**SPIKA:** Tukifika mbele kule kwenye vifungu na nini nitakupa tu nafasi, endelea kujiandaa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika...

**SPIKA:** Mwongozo kuhusu nini Mheshimiwa Halima?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea mapema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mapema leo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amesoma taarifa ya Kamati. Katika maelezo yake pamoja na mambo mengine naomba nimnukuu alisema nini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima nilishakupa Mwongozo katika hilo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba unisikilize.

**SPIKA:** Nilishatoa mwongozo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hukutoa mwongozo...

**SPIKA:** Kwa hiyo, kunitaka nitoe mwongozo wa pili itakuwa tunachelewa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ile ilikuwa taarifa.

**SPIKA:** Subiri basi niendelee kutafakari, unajua mwongozo unaweza ukatolewa jibu hapo hapo au baadaye.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sijasoma bado.

**SPIKA:** Ngoja niendelee kutafakari kwanza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba ni-*wind-up point* yangu.

**SPIKA:** Mchangiaji wetu wa pili ni Mheshimiwa Abdullah Mwinyi na atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Nondo. Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, tafadhali, ndiye unayefuata kuchangia.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, kidogo nimeshtuka kwa sababu nilikuwa sijajipanga kuchangia lakini kwa sababu umeninyanyua nitasema mawili matatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ripoti yake nzuri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uwasilishaji wake mzuri sana. Kwa kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati hii sitaweza kukosa mawili, matatu ya kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegusia sheria 9, napenda tu kugusia maneno mawili, matatu katika sheria zifuatazo. Ya kwanza ni Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432; Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95; Sheria ya Utumishi wa Jeshi

la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sura ya 241; na mwisho napenda tu kugusia Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, Sura 260. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *The Anti-Trafficking in Persons Act*, Sura 432 kwa kweli ni sheria ya msingi sana. Ulinzi na usalama ni jukumu letu sote Tanzania nzima sio tu jukumu la vyombo vya ulinzi na usalama pekee.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko katika Sura 432 yamegusia masuala mbalimbali na kuwapa mamlaka wananchi kadhaa kuweza kudhibiti biashara hii haramu. Napenda kuzungumzia kifungu cha 9 kinachozungumzia kuhusu *whistle-blowers,* wale ambao wanaona uharamia unatokea na wakaripoti ili kuhakikisha kwamba uharamia ule unadhibitiwa. Pia kifungu cha 12 nacho kinathibitisha tena kwa ziada *private citizens arrest,* wananchi tukiona kuna matatizo yanatokea, tumepewa mamlaka ya kuhamasishana na kuhakikisha ule uharamia wa namna hiyo hauendelei. Kwa kweli, sisi kama Kamati tumeridhia na ni masuala mazuri kabisa yameletwa kwa ajili ya kuyarekebisha.

Mheshimiwa Spika, Sura inayofuata ya 95, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, napenda tu kugusia jambo moja la msingi. Kipengele kipya cha 15 na 15A kinazungumzia masuala ya mirungi na bangi na kuweka mipaka na uzito wa kosa hilo kulingana na uzito wa mihadarati yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili, kwa kweli nimekubaliana na *proposal* ya Serikali lakini nitoe tahadhari. Suala la mirungi japokuwa nchini kwetu ni haramu lakini tunapakana na nchi za ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na nyingi za *SADC* ambazo suala la mirungi lenyewe si haramu. Sasa udhibiti wake utakuwa una matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile sisi tuko ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya pale zinarushwa ndege kama zile ndege za minofu za pale Mwanza zinaruka kutoka Nairobi

zimejaa mirungi kupeleka Ulaya hali kadhalika Uganda. Sasa hili suala katika *territory* yetu ndani ya Tanzania ni haramu na lina *penalty* kubwa lakini wenzetu wanaotuzunguka wote wamelihalalisha. Sasa ama tulitazame kwa ujumla wetu wote, tuwashawishi wenzetu liwe haramu kote au tuliwekee misingi fulani fulani ambayo inaweza ikaruhusu hii biashara ikaendelea la udhibiti wake utakuwa una matatizo makubwa. Haikuwa maudhui ya mabadiliko ya sheria hii lakini hilo ni angalizo kwa Serikali, tulitazame siku zijazo kwa sababu udhibiti wake utakuwa una matatizo ilhali wote wanaotuzunguka mirungi kwao ni halali isipokuwa sisi hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, suala la Uhamiaji ambalo limezungumziwa kwa ari kubwa mpaka sasa hivi, sheria na Katiba vinaguswa katika masuala haya. Kiukweli vipengele vimesomwa hapa kwa pupa sana bila kuwaruhusu watu kujenga hoja halafu tukazitumia zile hoja ili kuelekezana vizuri.

Mheshimiwa Spika, ibara sahihi ya kwanza kwa kuanzia ni Ibara ya Katiba ya 147(2), naomba nipewe wasaa kidogo niitafute katika kishkwambi hapa, niipate kuisoma vizuri nitiririke vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kama huioni tukusomee.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, Ibara 147(2) inasema: “Majeshi ya Ulinzi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza, kwa mujibu wa sheria, kuunda na kuweka Tanzania majeshi ya aina mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania”.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 147(4) inasema: “Kwa madhumuni ya ibara hii, “mwanajeshi” maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa”.

Mheshimiwa Spika, hii katiba ni ya mwaka 1977, kipindi hicho wakati hii Katiba inakuwa *formulated* haya ndiyo yalikuwa majeshi. Mwaka 1977 haya ndiyo yalikuwa majeshi lakini walitazamia kabisa kwamba siku za usoni kwa sababu mbalimbali nyingine kunawezekana kuwe na sababu ya kufanya tuwe na majeshi ya ziada. Ndiyo maana Ibara ya 147(2) inasema, kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 151 inazungumzia maana ya jeshi. Jeshi maana yake nini? Maana ya jeshi, ni lolote kati ya majeshi ya ulinzi na ni pamoja na jeshi lolote lingine lililoundwa na Katiba hii au kwa mujibu wa sheria na iliyotawaliwa na Amiri Jeshi Mkuu au kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Naomba kuishia hapa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo nilishakutaja, hayupo? Hayupo, si ndio?

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Ok, endelea.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba nijielekeze sana kwenye haya mabadiliko ambayo yanapendekezwa katika Sheria, Sura ya 432 katika marekebisho ya sheria, ambayo inazungumzia kuzuia usafirishaji wa binadamu. Katika Kifungu cha 3 tafsiri za baadhi ya misamiati inapendekezwa kufutwa na badala yake kuweka tafsiri mpya na tafsiri za misamiati mingine zinazopendekezwa, ili kuboresha kwa lengo la kuondoa mikanganyiko.

Mheshimiwa Spika, sisi ni Waafrika na jamii zetu sisi tunasema kwamba, ziko kwenye *extended families.* Sasa

katika haya maboresho ya misamiati naona kuna maneno badala ya lile unyonyaji *(exploitation)* kuna maneno mengine yamewekwa kwa mfano, wanasema:-

(a)*keeping a person in a state of slavery;*

(b) *subjecting a person to practices similar to slavery;*

(c) *involuntary servitude;...*

(f) *forced labour;...*

(h) *forced marriage; or*

(i) *forced begging.*

Mheshimiwa Spika, sasa jamii zetu zinategemeana sana, kuna watoto wa mjomba, kuna watoto wa shangazi ambao wanahamia kwa shangazi, wanahamia kwa mjomba, wanahamia kwa jirani. Hawa unategemea wanapokaa kwenye hizi familia zetu wawe kama sehemu ya familia, kwa maana ya kushiriki katika shughuli zote za kifamilia; iwe shughuli za uzalishaji, mashambani, biashara na kadhalika. Hatuna mfumo wa kuandikishiana mikataba tukiamini kwamba, kwa sababu ni sehemu ya familia, huyu mtoto ama kijana anapaswa kushiriki katika hizi shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa wasiwasi wangu, sheria hii itasababisha migogoro ndani ya familia kwa maana mtoto wa mjomba ambaye amekaa miaka mitatu kwa shangazi ametumikishwa anadai, sio kutumikishwa, ameshiriki katika shughuli za uzalishaji pale akadai kwamba, yeye ni muathirika wa hizi shughuli za usafirishaji wa binadamu kwa maana kwamba, amenyonywa.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia kwa mapana yake naona tuna changamoto sana hasa kwa huu mtindo wa familia zetu kuagiza watumishi wa ndani, mayaya. Kwa sababu, sheria hii inazungumzia sio tu namna alivyochukuliwa

kule, lakini namna ambavyo anashiriki katika shughuli za uzalishaji mali, lakini bila ya kuangalia stahiki za mfanyakazi. Stahiki za mfanyakazi tunazijua kuna kima cha chini cha mshahara, tunajua bima, tunajua *pension,* lakini tunajua aina ya familia zetu, watumishi wetu na jinsi gani hawa mayaya wanaishi katika hizi familia. Sasa tusije tukapitisha sheria ambayo inaenda kusababisha migogoro ndani ya familia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi nina bahati mwaka...

**SPIKA:** Hebu rudia tena, inasemaje? Inasemaje hii kitu maana...

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, huu msamiati mpya katika hii Sura ya 432 unazungumzia suala la *forced labour, involuntary servitude,* lakini kuna Kifungu (b) wanasema, *subjecting a person to practices similar to slavery.* Ukiangalia katika tafsiri unaweza ukasema kwamba, mtu ambaye halipwi mshahara wa mwezi, kwa mfano, inaonekana kwamba, huyu mtu anatumikishwa na inaweza ikatafsiriwa kwamba, huyu mtu ni mtumwa.

Mheshimiwa Spika, katika familia zetu sisi kuna vijana ama ndugu ama marafiki ambao wanakuja mjini kutafuta fursa kwa ndugu, ama wengine kwa sababu maisha yamewashinda wanakuja kukaa kwa ndugu zao. Sasa hawa wanapokaa na kama umesoma Kitabu cha Bulicheka wanazungumzia kabisa mgeni siku ya kwanza umfanyie nini, siku ya pili, siku ya tatu mpe jembe aende akalime. Sasa isije ikawa siku ya tatu anapewa jembe aende akalime, akaja jirani na kwa sababu, sheria hii inatusababisha kwamba, mtu yeyote anaweza akapeleka taarifa, mtu yeyote yule, anaweza akaenda na wako wengi mjini, anaweza akasema kwamba, unachokifanya hicho ni utumikishwaji na ni kinyume cha sheria na ukapelekwa mahakamani ukashitakiwa.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu kinaweza kikaparaganyisha familia nyingi tusipokuwa waangalifu. Sasa

*comfort* yangu nataka tuone ni kwa jinsi gani sheria hii ime-*take into context* mazingira yetu halisi ya kiafrika.

**SPIKA:** Ahsante. tukifika kipengele hicho nitakupa nafasi, Mwanasheria Mkuu atakufafanulia.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nina bahati 2007 wakati kuna *Global Forum Against Trafficking* pale Vienna nami pia nilishiriki. Moja ya vitu ambavyo vilituwekesha mpaka usiku mkubwa ni tafsiri.

Mheshimiwa Spika, kuna Taifa moja ambalo siwezi kulitaja kwa jina, lenyewe lilikataa kabisa kupitisha ile *protocol* kwa sababu ya neno moja tu, *sexual tourism;* wanakwambia kwamba, wao *in their context* hilo neno halipo na kwenye sheria zao halipo. Sasa sisi tunavyoleta maneno kama ya *involuntary servitude* ama *forced labor* wakati *TANU* ama CCM ilikuwa na msemo kwamba, watu wasiwe nzige, kwa maana unapoenda kwa familia lazima uwe unachangia, unashiriki katika shughuli za uzalishaji. Katika mazingira kama hayo katika *context* yetu, sheria hii inazungumzia vipi?

Mheshimiwa Spika, nachelea kusema kwamba...

**SPIKA:** Umeeleweka, litapata ufafanuzi baadaye na nitakupa nafasi nimesema ya kuchangia, *unless* una lingine. Kama ni hilo...

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hili suala la *forced marriage* na *forced begging...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya ni ya pili.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote. Pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *CPD* na Wizara ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo machache sana. La kwanza labda ni-*clarify* hii *issue* ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Ibara hii inayozungumzwa ya 147(4), mimi sijui hata kwa nini watu wanajadili kwa sababu, sisi tunazungumza habari ya majeshi. Ibara hii Waheshimiwa wanazungumza hapa ni *definition* ya mwanajeshi ambayo ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, nadhani hii iishie hapa, lakini kwa wanaotaka kujifunza zaidi wasome Ibara ya 151, *definition* ya neno Askari, wataelewa zaidi likitumika kuhusiana na jeshi. Naomba ninukuu:

"...likitumika kuhusiana na jeshi lolote, maana yake ni pamoja na askari yeyote ambaye kwa mujibu wa amri ya jeshi hilo ni mtu anayewajibika kinidhamu."

Mheshimiwa Spika, hizi ni *terminologies.* Unajua watu wasifikiri kila kitu kilichoko kwenye Katiba unaweza ukasema *is unconstitutional* na nitakupa tu mfano huko mbele ili Wanasheria waweke hii sawasawa. Huwezi kusema sheria hii *is unconstitutional* kwa sababu haina rangi ya Katiba, tunafahamu hii rangi ya Katiba, si ndio?

Mheshimiwa Spika, huwezi ukasema sheria hii *is unconstitutional* kwa sababu haina *page numbers* pamoja na kwamba, Katiba ina *page numbers.* Kwa hiyo, hili tumezungumza habari ya jeshi, sasa watuambie kama ile ibara inazungumzia jeshi ama mwanajeshi? Sasa sisi hatuzungumzi habari ya *definition* ya mwanajeshi, hatuzungumzi. Hilo moja.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mwinyi pale, sasa naogopa kusema Wakili Msomi Mwinyi. Alichosema ni kwamba...

**SPIKA:** Unaruhusiwa Mheshimiwa.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, sawa, kumbe naruhusiwa, nashukuru.

**SPIKA:** Kabisa. Nimeshaelimishwa kwamba, ni wasomi. *(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ni kweli, unajua hizi ni lugha za Mawakili, ukim-*address* wakili mwenzako *is a sign of respect,* ilikuwa haina haja ya kusema kwamba, sisi tuna nanihii zaidi, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo tulichokuwa tunakisema kifungu wanachosema Waheshimiwa Wabunge ni mfano tu kwamba, mwanajeshi atoke kwa makundi haya, kwa mfano tu, lakini kama nilivyosema haizungumzii majeshi inamzungumzia mtu mmoja. *Definition* ya mtu anayeitwa mwanajeshi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajadiliana kwenye Kamati tuliona suala alilokuwa analizungumzia Mheshimiwa Londo. Hata sisi tunachokisema kwa sababu, sheria hii ni kweli imeongeza hiyo *forced marriage* na imeongeza kitu kinaitwa *forced begging* ambayo kwa tafsiri ya Kiswahili maana yake ni ndoa za lazima kwa maana ya *forced marriage* na kumlazimisha mtu kuishi kwa ombaomba.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati, tuliishauri Serikali ku-*define* baadaye haya maneno ili yasilete mkanganyiko wa tafsiri na sheria nyingine kwa sababu, tunajua jamii nyingi za Watanzania baadhi ya ndoa hizi bado ni *arranged* kati ya wazazi na lakini ikitafsiriwa vizuri tu baadaye kwenye kanuni haitaleta mkanganyiko huo. Kwa hiyo, hata sisi tuliona, lakini kwa kuwa hii sheria haiku-*define* basi maoni ya Kamati tumeomba Serikali baadaye iondoe huo mkanganyiko kwa

sababu tunajua Sheria ya Ndoa inazungumzia aina ya ndoa hizo ambazo jamii zetu nyingi sana wakiwemo wa Kiteto kuna hiyo tafsiri ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, pia tulikuwa tumeomba, huku kulazimishwa mtu kuwa ombaomba inaweza pia ikawa na tafsiri pana ya kisheria. Kwa hivyo, tuliomba pia, baadaye Serikali iweke kwa namna ambayo kwa sababu, unajua kimsingi mtoto akiwa mtaani leo ana wazazi, akikutwa na hali ile sasa ya ombaomba maana yake ni kwamba, wazazi wameshindwa kutimiza hiyo *obligation*. Sasa tukasema baadaye pia, Serikali ifafanue kwenye kanuni ili isiwe kila mtoto anayekutwa mtaani ionekane basi wazazi wake wana-*fall* kwenye hii *trafficking,* kwa sababu, wakati mwingine familia zetu ni tofauti tofauti, viwango vya hali ya kimaisha ya Watanzania wote haifanani. Kwa hivyo tulisema na Kamati iliona hilo na kuiomba Serikali kulifafanua kwenye *regulations* ili iondoe utata huo na kwa kuwa hii sheria hai-*define* haya maneno itawekwa vizuri sana kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine tulichoona kwenye Kamati, ni kwamba, pengine bado kwenye sheria nyingi nyingi utakutana na hili neno *department.* Tumeona kwenye *amendments* zile bado inasema kwamba, pamoja na mabadiliko haya litaendelea kutumika neno hilo, kwa mujibu wa Kifungu kile cha 3 kwamba, nanii itaendelea kutumika kama idara.

Mheshimiwa Spika, inasema:

*"The Department established under subsection (1) shall be a Force within the Ministry and in that capacity".*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kuwa sasa *intention* ni kufanya jeshi liwe *independent.* Kwa hiyo, kuna haja sasa kuangalia baadaye hizi sheria nyingine ili isitokee *confusion* ya *word department* na jeshi kwa sababu, *department* ni *small unit.* Bado lugha ile ya kizamani wakati bado ilikuwa ni *department* ndani ya jeshi ili iwe *in order,* usitokee tena mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo tuliliona pia hilo kama Kamati, tukashauri kwamba, kwa kuwa, bado sheria nyingi *including* sheria hii ambayo inakuwa *amended* ya *Police Force...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ooh, ahsante sana. Naambiwa ni kengele ya pili.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, sawa, baada ya kusema haya, naungana na Kamati na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward. Katika mchango wako ulipata tabu kidogo kum-*address accordingly* Wakili Abdallah Mwinyi kama Msomi; hatuja-*rule out* kuitana hivyo hata kidogo, msije mkasema Spika alishafanya kitu hicho, hapana. Yale yalikuwa ni maoni yangu tu na ilikuwa ni *advice,* ndio maana nilianza kwa kusema hivi ni lini mtaacha? Kwa sababu, ni jambo ambalo ukilitazama tu unajua kwamba, iko siku vizazi vijavyo watakuja kuacha hicho kitu, kwa sababu, si imeandikwa wajikwezao wataviliwa.

Ni lugha fulani katika Kiswahili, ina *connotation* ya kujikweza, kwa hiyo, ndugu zetu wa Kagera si tunawaita *nshomire nshomire*, sasa na nyie mkiitana *nshomire*, ila kwa Kiswahili msomi, haina shida sana, lakini kwa vyovyote yaani ukiitazama tu iko siku, Waingereza wao *it is easy* kwa sababu, utamaduni wao, *culture* yao iko katika *classes, Sir, Learned Brother,* wana hizo *categories*, lakini sisi Waswahili tunajaribu sana ku..., na hasa sisi ambao tulikulia katika ujamaa, ndio shida yetu hii, lakini hatuwakatazi kabisa kuitana mtakavyo. Si ninyi tu, hata wengine, hata siku ile sikusema tu Wanasheria nilitaja na kada nyingine, nafikiri mlinisikia siku ile kwa hiyo, halina shida kabisa, tuendelee tu tukiwa huru.

Baada ya jana kwamba, tumepitisha sheria ndugu zetu wa zimamoto kuwa jeshi, sikutarajia leo tungeweza kuwa na mjadala huu na hasa baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, ambayo ndio inahusika hasa na majeshi, kutupatia ushauri ambao tuliupata jana, tutakuwa hatueleweki kama jana tuliamua vile halafu leo tena tunaanzisha mjadala ambao haupo. Kwenye Katiba hapa kabisa ukiisoma vizuri 147(2) ndio hasa inayohusika kwa sababu, inahusika na kuunda na ndio kipengele kinachotaja habari ya kuunda na hapa tunaunda kwa hiyo, tuko *in order.*

Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi chana.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali kwa ajili ya kutuletea Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali katika wakati huu muafaka, hasa nikitilia mkazo kwenye hii Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu pamoja na hii Sheria ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, sheria hizi zimekuja kwa wakati muafaka kwa sababu ni sehemu kubwa kabisa ya utekelezaji wa dhana ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mama yetu Samia Suluhu Hassan ya kuifungua ncbi yetu na kukuza uchumi. Unapofungua nchi na kukuza uchumi lazima kuzingatia kuweka sheria ambazo kwanza zinarahisisha uhusiano wa kimataifa; lakini pili zinawalinda hata Watanzania wenyewe dhidi ya mambo ambayo yanaweza yakajitokeza katika mchakato huo wa kufungua nchi, yakawaathiri Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Sheria hii ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, ambapo ile Ibara ya 4 inayorekebisha kile Kifungu cha 3 na kutoa yale makosa ambayo yanakatazwa chini ya sheria hii, ikiwa ni pamoja na haya ambayo mzungumzaji mmojawapo aliyetangulia aliyazungumza, juu ya mambo ya *forced marriage* na kadhalika. Katika hasa hili la *forced marriage* naomba tu

nilipongeze Bunge lako Tukufu kwamba, pengine ndio tunaingia katika historia kwa sababu, mwezi wa Tatu mwaka huu Mahakama ya Uhalifu wa Kivita *(ICC)* katika ile kesi ya Dominick Ogweni wa Uganda ilitoa mojawapo ya sehemu ya hukumu yake ilitamka wazi kwamba, *forced marriage,* yaani hizi ndoa za kulazimisha ni *crime against humanity,* ni uhalifu dhidi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, suala hili halikuanzia pale. Kulikuwa na mtanange mkubwa sana wa kisheria na kikesi Siera Leone, halikwisha kwa sababu Mahakama zilikuwa zikitofautiana tofautiana, likaenda Cambodia, baadaye *ICC* ndiyo wakatoa hukumu hiyo mwezi Machi mwaka huu. Natarajia kwamba baada ya hukumu hiyo, nchi sasa zitarekebisha sheria zake kuendana na tamko hili la Mahakama hii kubwa la dunia. Kwa hiyo, angalau Tanzania tumekuwa moja kati ya nchi za kwanza kufanya hivyo kurekebisha sheria yetu hii na ninaamini idara na sekta nyingine pia zitaangalia sheria zao ili ikiwezekana ziendane na maamuzi haya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, labda kabla sijaendelea, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge ambaye alikuwa na wasiwasi juu ya hii *definition* ya mambo ya *slave* kwamba pengine inaweza ikatuathiri kwenye mazingira yetu. *A slave,* yaani mtumwa sifa ya kwanza ni kwamba anakuwa ni *property* (mali) ya yule ambaye anammiliki. Ili awe mali yake, ni lazima yule awe amelipiwa, amepatikana kwa thamani, kwa *consideration.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vigumu sana hizi *extended family* zetu kwamba mtoto wa shangazi amekuja kukaa kwangu, hata kama kwangu kuna kazi nyingi kuliko zile za kule kwao, kuangukia kwenye tafsiri ya mtumwa, siyo jambo ambalo ni rahisi kabisa. Kwa sababu ili uwe mtumwa lazima uwe mali ya yule ambaye anakumiliki; na kuwa mali ni lazima uwe ulilipiwa fedha au bei na uwe unatumika kwa faida ya yule anayekutumia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya suala la Sheria ya Uhamiaji, la kwanza ni vizuri tukakubaliana kwamba Idara ya Uhamiaji

ina majukumu ya kidiplomasia na ina majukumu ya kiusalama na mengine ya kiulinzi; na sheria nyingine zote zinatambua majukumu haya ya Idara ya Uhamiaji na zinaipa majukumu hayo. Sheria inawapa mamlaka ya kukamata *powers of arrest* mamlaka ya kuchunguza, ambayo hayo yote ni mamlaka ambayo yanafanywa na chombo ambacho ni cha kiusalama na cha kiulinzi.

Mheshimiwa Spika, hata ile Tume ya Utumishi ambayo inaangalia maslahi yao, inaangalia maslahi ya Polisi, inaangalia maslahi ya Magereza lakini wao wanaingia ndani ya Tume ile, lakini hawana hadhi kama wenzao. Hili linaleta mkanganyiko. Kwa hiyo, marekebisho hayo ni muhimu yanapofanywa ili sasa kuwawezesha kufanya kazi zao kwa mamlaka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeingia kwenye miradi mikubwa ambayo inatufanya tuingie zaidi kwenye mahusiano ya Kimataifa. Hata mradi wa bomba la mafuta *for that matter* ni mradi ambao unatufanya masuala ya Kimataifa yawe ni ya kila siku na hata *Royal Tour* ambayo ipo kwenye mchakato wa kutengenezwa, sasa hivi litaifungua nchi hii suala la kuingia na kutoka wageni litakuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, nilazima tuwe na Idara ambayo ina mamlaka ya kisheria ya kuwapa hata imani wale wanaoingia na kutoka kwamba wapo kwenye mikono salama.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi, nimalizie tu kwanza kwa kukubaliana na tafsiri ambazo wamezizungumza wenzangu juu ya suala hili la Katiba linalozungumziwa. Alivyozungumza Mheshimiwa Mwinyi na Mheshimiwa Olelekaita nakubaliana nao, labda tu niwekee tu msumari wa mwisho kwenye huu mjadala kwamba hii Ibara ya 147 ambayo tumeizungumza sana iko wazi kabisa kwamba kwa madhumuni ya ibara hii; siyo kwa madhumuni ya Katiba hii, ila kwa madhumuni ya ibara hii, ndiyo ikatoa *definition* ya mwanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya Katiba hii, ni ibara ya 151 ambayo inatoa *definition* ya jeshi ambayo

nadhani wote tunakubaliana kwamba ni hata jeshi lililoundwa na sheria nyingine yoyote. Jeshi lingine lolote lililoundwa kwa sheria nyingine yoyote. Kwa hiyo, kwa vile hatuzungumzii suala la Ibara ya 147 peke yake, tunazungumzia Katiba hii, tafsiri sahihi ni ile iliyopo kwenye Ibara ya 151. Kwa hiyo, hatukatai kwamba Ibara 147 Ibara ndogo ya (4) ni ibara halali ya Katiba hii na inayotoa tafsiri, lakini kwa madhumuni ya kazi tunayoifanya leo, kwa vile inahusu Katiba yetu nzima na sheria nyingine, tafsiri inayo-*prevail* ni ile Ibara ya 151 ambayo inatoa tafsiri inayohusika na Katiba nzima, siyo ile ya 147 ambayo inahusika na ibara moja tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tadayo, Agnesta na rafiki zake wao lengo lao ionekane Katiba hii ina upungufu, sasa ipatikane mpya. Ndiko wanako-*drive* tu, wala hawana lolote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, tafadhali.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza nampongeza Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa kutuletea haya maboresho, naunga mkono hoja. Naenda ukurasa wa tano wa Muswada, pale kwenye tafsiri; na ninaanza na ile tafsiri ya neno *"forced begging."* Hii iko kwenye Kifungu cha 4 cha Muswada ambapo imeongeza Tafsiri ya maneno mbalimbali, lakini nitajikita kidogo pale kwenye *"forced begging."* Naunga mkono *forced begging*. Kuna *begging* na *forced begging*.

Mheshimiwa Spika, *forced begging* ni pale ambapo mtu analazimishwa kwenda kuomba. Nimewahi kusimamia baadhi ya kesi na nitaitaja mojawapo; kuna mama mmoja alikuwa anakusanya watoto walemavu, anasema

anakwenda kuwasaidia. Anawachukua vijijini, mikoani. Mbaya zaidi alikuwa anawachukua kwenda kwenye nchi nyingine kutoka kwenye nchi yetu. Naihifadhi hiyo nchi kwa ajili ya usalama. Katika ile nchi nyingine, wale watoto takribani 10 na kitu, walikuwa wanachukuliwa na taxi asubuhi, wanashushwa kwenye vituo mbalimbali wawe *beggars*. *That is forces beggars under eighteen*. Jioni anahesabia kila mtoto amepata shilingi ngapi katika omba omba. Alikuwa anapata takribani kwa siku shilingi 300,000/= ya Tanzania. Sasa naafiki kabisa kuongeza maneno tunapozuia usafirishaji haramu wa watu, neno *"forces begging"* liwepo. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, kwa sababu nimesema kuna watu wametumika kwenye ku-*force beggars,* kwenye kifungu cha 10 ambacho kinarekebisha Kifungu cha 26, sheria hiyo hiyo, *trafficking in person,* yenyewe inasema *the sale proceeds of any property,* Kifungu cha 10 (2) itakuwa *confiscated or forfeited under this Act* na *subject to approval of the Minister responsible* itakwenda *to be deposited* kwenye *fund.* Sasa kama kuna mali imepatikana, itataifishwa. Nilikuwa nauliza: Je, fedha zinazopatikana kotokana na *trafficking in human* na zenyewe zimo hapa, tunaziweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwa haraka sana kutokana na muda, hii *Immigration Act* inakuwa ni *point* yangu ya mwisho kumalizia. Naomba pale Kifungu cha 30, 10A A*mendment of the Meat Industry Act*, inasema *"recommendation by the Registrar and after consultation with the Minister delegate some of the function to a Local Government Authority*." Sasa nilikuwa naomba neno *registrar* lipewe tafsiri, maana tuna Ma-*Registrar* wa aina nyingi. Baada ya hapo, kifungu hiki kinasema: *"The Board may upon recommendation by the Registrar and after consultation with the Minister delegate some of the functions to the Local Government Authority."* Naafiki, baadhi ya shughuli watazipa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, hata nikasema tukiafiki hii, lazima *Local Government Authority Act* (Na. 8) na (Na. 7) pia

tukaangalia namna ya kuziboresha ili ziweze kupokea hiyo mamlaka ya Waziri. Maana kule inatambua Waziri wa TAMISEMI, lakini hapa atakuwa Waziri *responsible* for masuala ya *meat.*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine naungana kabisa na Mwanasheria Mkuu, Kifungu cha 44, hii ni Sheria ya *Amendment of Tanzania Wildlife Research Institute* Kifungu cha 44 (c) ambapo pale wamesema: *"to a person convicted under this Act may be withdrawn."* Inazungumzia masuala ya *permit* inaweza kuwa *withdrawn.* Badala ya neno *"withdrawn",* naomba litumike neno *revoked.* Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu alisema nadhani wakati anawasilisha, hilo jambo limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nakwenda kwenye *Amendment of Immigration Act* kwamba Uhamiaji sasa inakuwa jeshi. Kwanza naunga mkono hoja, ni sawa kabisa uhamiaji kuwa jeshi. Kwanza tumechelewa kusema uhamiaji kuwa Jeshi, ilipaswa tufanye maamuzi haya muda mrefu. Idara hii ya uhamiaji inasaidia katika mipaka masuala mbalimbali. Katika mipaka yetu lazima tujiridhishe watu wanaoingia ndani ya nchi kuangalia alama za vidole *(finger print),* kuna masuala ya *Visa* na ndiyo maana kuna baadhi ya maeneo mtu akiomba *Visa,* tunamwambia *Visa* yako itakuwa ni *referred,* hadi tukaangalie kama wewe ni mtu salama, huna makosa ya jinai, *you are not a criminal.* Kwa hiyo, haya yote yanafanyika na masuala ya Uhamiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitendo cha kusema Uhamiaji iwe jeshi, ninaafiki. Vile vile Uhamiaji wanashughulika na mambo ya *passport.* Kupitia *Passport* tusipokuwa salama, nchi yetu inaweza ikatumika kufanya ubadhirifu. Tanzania kuna maneno hatujui jinsi ya kuyatumia, tunayasikia tu kwa wenzetu. Kuna maneno kama *terrorist*, Ugaidi kuna maneno kama Boko haramu, hatuyajui sisi ni kisiwa cha amani; kuna maneno kama *Al-Qaida* hatuyajui, ni kisiwa cha amani; tunapoona amani Tanzania ipo, tusione vyaelea, vimeundwa na wanaoundwa ni pamoja na Uhamiaji. Kwa hiyo, kitendo

cha kusema leo kwamba Uhamiaji iwe jeshi, naunga mkono, ninaafiki na kwa kweli kwa namna moja au nyingine naweza nikasema kwanza tumechelewa ilipaswa ije kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza kwa mujibu wa Sheria; na hii leo ndiyo tumeletewa sheria, kuunda na kuweka Tanzania majeshi ya aina mbalimbali; na leo tumeona Jeshi la Uhamiaji sasa itakuwa ni *force and not department,* kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Uhamiaji tuna nchi; boda ya kwetu na nchi moja ni kilometa takribani 900. Hiyo ni boda tu. Kilometa 900 kwenye barabara ni sawa sawa na kutoka Dar es Salaam - Iringa mpaka Makambako, hiyo ni boda tu. Sasa maeneo haya wanaweza wakaingia wahalifu. Kwa hiyo, hawa watu wa *Immigration* kwenye boda wanasaidia sana kuhakikisha wanaoingia ni salama na wanaoingia ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muafaka kabisa iwe jeshi, wapewe bajeti ya kutosha na vile vile kama inavyoelezwa, *"the department established under subsection (1) shall be a force within the Ministry and in the capacity, it shall be governed in the manner and style similar to other force within the Ministry.* Vile vile lazima wapewe *rights* na *privilege* kutokana na utaratibu wa jeshi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana. Mheshimiwa Zungu, halafu Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Siku ya Ijumaa inayokuja panapo majaliwa, Kamati ya Ulinzi na Usalama itakuletea Azimio la Kupambana na Ugaidi na *protocals* ambazo Tanzania imeridhia, sasa Bunge lako itabidi likubali kuridhia ili sasa nasi tuwe katika *signatory* wa Bara ya *AU* pamoja na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, katika *commitment za States* zipo 12; (b) inasema: *"prevent the entry into the training of terrorist groups on their territories." Response* ya kwanza ya nchi ya ku-*prevent* wahamiaji haramu, ku-*prevent* wakimbizi haramu, wanaotembea na silaha ni uhamiaji. Ndio wa kwanza, hakuna popote pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, chombo hiki cha Uhamiaji sasa hivi ninavyosema, kipo kwenye *theatre for operation,* kwenye vita Msumbiji kinapambana na magaidi wa Msumbiji, chombo hiki ambacho kinasimamiwa na *Jenerali* wetu makini kabisa *General* Anna Makakala. Sasa watu na amani hii mnayoiona Tanzania ni sababu ya vyombo hivi ambavyo vinafanya kazi.  Nchi yoyote lazima iwe na msemo, nasi Tanzania tunasema, *"Uniting and Straightening Tanzania by providing appropriate tools required to intercept obstruct malicious activities within our borders by arming our enforcers." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Marekani kuna *Transport Security Agency,* wale wote ni watu wa Uhamiaji. Sasa inawezekana wengine hawajui. Ukienda Dubai, zamani walikuwa wanavaa *uniform,* sasa hawavai *uniform,* lakini vitu wanavyo chini ya meza. Akiingia mhalifu, wanapambana naye. Vile vile, kwa mara ya kwanza katika Taifa letu, Amiri Jeshi Mkuu ndiye aliyemteua Kamishna *General* wa Uhamiaji na ndiye aliyemwapisha na kumvisha nyota hadharani cheo chake kwa kuonesha sasa hawa ni Jeshi. Kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, tumechelewa kuleta hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ni chombo muhimu katika vyombo vyote vya jeshi. *Response* ya kwanza kwenye mipaka

ni wao, hakuna chombo chochote kingine. Tunapotaka kuweka vigezo kutoku-*strengthen* amani ya nchi yetu kwa kutumia Katiba *we are wrong somewhere.* Tunapovamiwa kwenye mipaka, tunapovamiwa nchini, hakuna Katiba itakwenda kusimamisha hayo mapigano ya hao wanaokuja kuleta Tanzania, bali ni vyombo hivi ambavyo vipo chini ya Amiri Jeshi Mkuu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wenzangu waelewe umuhimu wa vyombo hivi, wana uwezo wa kijeshi kupambana na uhalifu wowote *malicious* yote *ya attack* ambayo itataka kuja hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana tena sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Muda wangu ulikuwa mdogo, lakini nilitaka niguse hapa hapa kuwasaidia wenzetu waelewe umuhimu wa chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Simbachawene, halafu nitakuita mtoa hoja uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana sana kwa kunipa nafasi; na kwa kuwa iliyokuwa Idara na ambayo sasa Bunge lako linakaa kwa ajili ya kutunga kuifanya iwe jeshi kamili, ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na ndiyo *practice* inaonesha kwa nchi wanafanya hivyo.

Mheshiumiwa Spika, niseme ukweli, hata kwa hali ilivyo sasa, ukimwangalia Kamishna Jenerali na wale Askari wote na wamevaa vyeo, tayari wana sura ya kijeshi na wanashiriki katika vikao vya Kamati mbalimbali za Ulinzi na Usalama sambamba na vyombo vingine vya kijeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini leo hii tunataka kutunga sheria hii? Unaposema jeshi, maana yake ni nidhamu.

Tunataka chombo hiki sasa kiwe na nidhamu, kifanye kazi kwa amri. Chombo kinachokuwa kinafanya kazi kama Jeshi kinakuwa chini ya Amiri Jeshi Mkuu. Kwa ilivyokuwa, kilikuwa ni kama hakipo chini ya Amiri Jeshi Mkuu, lakini kinafanya kazi na Amiri Jeshi Mkuu. Sasa tunarasimisha kwa sababu kila kitu kipo sawa sawa. Tayari tunakiona kama Jeshi na tayari wanavaa sare ya kijeshi na wana vyeo vya kijeshi, kasoro tu kulikuwa kuna upungufu wa kukifanya kuwa jeshi kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo hapa kuna mjadala kwamba kwa kufanya Idara hii kuwa jeshi tunavunja Katiba, la hasha! Nadhani wanaofikiri hivyo wameji-*misdirect* kwenye Kifungu cha 147 (4) ambacho kimetoa tafsiri ya mwanajeshi. Kilipotoa tafsiri ya mwanajeshi kikasema, maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la kujenga Taifa. Wao wakadhani majeshi yalifungwa hapa, hakutakiwi Tanzania kuundwa jeshi lingine. Hapa ilikuwa ni tafsiri ya mwanajeshi kwa maana ya majeshi yaliyokuwepo wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuanzisha leo jeshi: Je, tunavunja Katiba? Kibali hicho tunakipata wapi? Tunakipata kwenye Ibara ya 147 (1) na ya (2). ya (1) inasema: *"ni marufuku kwa mtu yeyote au shirika lolote au kikundi chochote cha watu, isipokuwa Serikali kuunda au kuweka Tanzania Jeshi la aina yoyote."* Kwa hiyo, ni Serikali ndiyo inayoweka Jeshi la aina yoyote iliyokuja na Muswada hapa Bungeni ni Serikali na Mkuu wa Serikali ni Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende ya pili ya 147(2) inasema hivi Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza kwa mujibu wa sheria kuunda na kuweka Tanzania majeshi ya aina mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania hapo ndiyo ina *qualify* zaidi kwamba sasa kumbe Serikali ina uwezo wa kuweka majeshi haikuishia kwenye ile kwamba baada ya yale tuliyoelezwa kwenye 147(4) basi iishie pale pale hapana bali yanaweza kuwekwa kwa mujibu wa sheria. Sheria inatungwa na nani? na Bunge

151 inasema kuhusu tafsiri sasa ukienda 151 inasema Jeshi maana yake nini? Jeshi maana yake ni lolote kati ya majeshi ya Ulinzi na ni pamoja na Jeshi lolote jingine lililoundwa na katiba hii au kwa mujibu wa sheria na linalotawaliwa kwa amri ya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amri ya Jeshi inatolewa na nani? Na Amiri Jeshi Mkuu. Jeshi lolote maana yake kati ya haya yaliyowekwa kwenye Ibara ya 147(4) na lingine lolote litakalokuja kwa mujibu wa kutungwa sheria bungeni. Kwa hiyo, nadhani kwa wanasheria wazuri nadhani wanafahamu na wameelewa sasa tukibakia hapa tunataka kuleta utata utakuwa ni utata. Lakini nadhani tumeelewana na hata wenzetu waliotoka kwenye kamati kule nadhani wameelewahapa tulikuwa tunanogesha mjadala lakini kimsingi katiba ni maandishi lakini yanahitaji pia tafsiri ya mtu aliyesomea kutafsiri sheria,

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa mchango wako mzuri sana huo na si wote wanajua neno Amri ya Jeshi wale mliopita Jeshini mnajua neno imezuiliwa. Raia hawezi kujua imezuiliwa maana yake nini Mheshimiwa mtoa hoja tafadhali hitimisha hoja yako sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Adelardus Kilangi *Professor* tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 Mwaka 2021. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliotoa maoni yao katika michango yao mbalimbali tumepokea maoni kutoka kwa Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mheshimiwa Abdallah Mwinyi, Mheshimiwa Denis Longe, Mheshimiwa Edward Kisau, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Dkt Pindi Chana, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Simbachawene ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, katika michango hiyo mambo makuu yaliyojitokeza ni kama matatu hivi na nitachukua nafasi hii kuyatolea ufafanuzi. Jambo la kwanza ni suala la kuitambua Idara ya Uhamiaji kuwa Jeshi ambayo imeibuliwa katika mchango wa Mheshimiwa Agnesta lakini Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia na katika mchango wake alijikita katika Ibara ya 147(4) ambayo inagusa neno mwanajeshi.

Mheshimiwa Spika, hii imeshaelezwa na Wabunge wengine waliochangia wakisema kwamba ibara hiyo inagusa au inazungumzia neno mwanajeshi na siyo jeshi na kwamba kama tunahitaji kupata ibara mahususi inayohusiana na jeshi au kuanzisha jeshi ni Ibara ya 147(2) lakini pia Ibara 151 ya katiba. Sitazirudia kuzisoma kwa sababu zimesomwa mara kadhaa ibara hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka nisema neno moja kwamba kunapoibuliwa hoja au wasiwasi kwamba katiba imevunjwa au inaelekea kuvunjwa ni vema yakatolewa maelezo ya kina ili wasiwasi huo usiwepo na ufafanuzi huo uingie katika kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Ibara 147(4) ni lazima isomwe pamoja na Ibara ya 147(3) naomba niisome hiyo fasili ya (3) itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa isipokuwa tu atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya katiba hii. Kwa hiyo hiyo ndiyo inatangulia sasa ibara ndogo ya (4) inasema kwa madhumuni ya ibara hii mwanajeshi maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake ni nini hapa neno mwanajeshi lililotumika katika Ibara ya 147(4) linaendana na kilichotamkwa katika fasili ya tatu kwamba itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa. Kwa hiyo, neno mwanajeshi hapa limetumika katika muktadha ule wa kuzuia kujiunga na

chama chochote cha siasa na kwa hiyo ndiyo maana inatumika tu kwenye ibara hii.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme zaidi kuhusu hapo hadi mwaka 1992 ibara ndogo ya (3) na ibara ndogo ya (4) hazikuwepo kwenye katiba hizi zimeingizwa wakati wa kujadili sheria ya marekebisho ya katiba iliyofanyika mwaka 1992 na yale marekebisho yalikuwa na sababu mahsusi lakini ili kuthibitisha hilo nadhani ni vema tukarudi katika majadiliano ndani ya Bunge tarehe 30 na tarehe zilizofuata za mwezi Aprili mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja alikuwa ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais na alikuwa anaeleza au anawasilisha Muswada wa Sheria ya mabadiliko ya nane katika katiba ya nchi ya mwaka 1992 katika ukurasa wa 118 wa *Hansard* unaoakisi majadiliano ya tarehe 30 Aprili, 1992 mtoa hoja alisema lengo la kufanya mabadiliko katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuuondoa mfumo wa chama kimoja cha siasa na kuanza mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika ukurasa wa 121 katika majadiliano ya tarehe 30 hiyo hiyo Aprili 1992 kipengele cha (vii) anasema pendekezo hii ni baadhi ya masuala ambayo yatafanyiwa marekebisho katika katiba na yanayopendekezwa na sheria hiyo ni pendekezo kuhusu wanajeshi, vyombo vya ulinzi na usalama na watumishi wengine wa ngazi za juu wa umma kujiunga na vyama vya siasa. kwa hiyo huo ndiyo muktadha wa hayo mabadiliko tunayokuja kuyaona yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, akihitimisha hoja yake ambayo ilichukua siku kadhaa hii ilikuwa ni tarehe 7 Mei 1992 ambayo iko katika ukurasa wa 659 wa *Hansard* mtoa hoja anasema Wabunge wengine ambao kwa kweli walikuwa wengi zaidi walipendekeza kwamba wanajeshi wasihusishwe kabisa na masuala ya siasa.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kuwaarifu ndugu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Muswada huu wakati wa kusoma mara ya pili Serikali itapendekeza badiliko la ziada kwenye Ibara ya 147 katika hiyo ibara ya 147 kama mtakavyoona mimi kwangu iko kwenye ukurasa wa 73 huo ni wa mtoa hoja tutaongeza kifungu kingine kidogo baada ya kifungu cha pili cha katiba ambacho kitasema kuwa wanajeshi wasiingie katika vyama vyovyote vya siasa.

Mheshimiwa Spika, yalipokuja hayo marekebisho kwenye sheria yenyewe ukienda Ibara ya 36 ya Muswada wa sheria ya mabadiliko ya (8) ya Katiba ya nchi ambayo ilikuja kuwa Sheria namba (4) ya mwaka 1992 ibara ya 36 ndiyo inabeba hivyo vifungu viwili vilivyoongezwa katika Katiba. Ibara ya 36 ilivyosomeka wakati huo ilisema Ibara ya 147 ya katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza baada ya ibara ndogo ya pili, ibara ndogo zifuatazo: Kwanza ni ibara ndogo ya (3) na inasema hivi itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya (5) ya Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine ndiyo hicho kidogo cha (4) kinachosema kwa madhumuni ya ibara hii mwanajeshi maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, ninarudia kusema kwamba Ibara ya 147(4) inahusika tu na kile kilichosemwa katika ibara ya 147 (3) na haihusiani hata kidogo na suala la kuanzisha Jeshi au Majeshi ibara sahihi ni 147(2) na 151. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mchangiaji pia alieleza kwamba ili kuanzisha Jeshi unahitaji hati ya Rais ya kuanzisha Jeshi na akawa anarejea natumaini anataka kurejea Ibara ya 33 ya Katiba ambayo anasema Mheshimiwa Rais ni Amiri Jeshi Mkuu na ni kweli 33(2) inasema Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu lakini hiyo haisemi kwamba anapokuwa na sifa hizo tatu kunapotakiwa kuanzishwa Jeshi ni lazima atoe hati haijaandikwa mahali

popote pale. Kwa sababu tunayo tayari ibara ya 147(2) imejitosheleza katika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika hoja nyingine ambayo ilikuwa inahusu suala la kwamba baadhi ya mihadarati inayozuiwa Tanzania inaruhusiwa katika nchi nyingine ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na pengine nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mwinyi. Sasa nadhani hatuwezi tukatunga sheria kwa ajili ya nchi nyingine lakini litabaki ni suala la mashirikiano na mashauriano katika nyanja za Kimataifa na kuona kama linaweza kuwa ni mojawapo ya masuala ambayo nchi hizi zinaweza zikalichukulia msimamo wa pamoja. Lakini kwa ujumla Serikali imelichukua jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ambayo nafikiri ni vema kuitolea ufafanuzi inahusu tafsiri ya neno *exploitation* kwenye ile sheria ya *anti-trafficking in persons* unajua Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameeleza wasiwasi wao katika baadhi ya maneno yaliyotafsiriwa hapo na hasa kama tulivyosema neno *exploitation* ambalo chini yake ziko tafsiri au mazingira mbalimbali ambayo yanaweza kuhesabiwa kama ni *exploitation*. Lakini yaliyozungumzwa zaidi ni hili la *servitude* kwamba linaweza likaendana likapingana pengine na mazingira tuliyonayo. Lakini nilitaka kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hoja hiyo kwamba ili *servitude* ihesabike kuwa ni *exploitation* lazima iwe *involuntary* na tafsiri hiyo ipo katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kulikuwa na wasiwasi juu ya *forced labor* na hasa katika mazingira hayo hayo pia ya kwetu ya kiafrika lakini basi nimuondoe wasiwasi kwa sababu maelezo yametolewa kwamba hii haitajumuisha mazingira ambapo yanahusisha watoto wanaoishi na ndugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mwisho kabisa kuna neno *forced marriage* hili nalo Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi lakini ninapenda kuwatoa wasiwasi huo kwa sababu unapolizungumzia neno *forced marriage* linapaswa kusomwa kwa muktadha wa kifungu cha 4(1)(b)

pamoja na (c) cha sheria kama ilivyosasa lakini nafikiri ni vema nikasoma sasa hivyo vifungu nilivyovitaja ili nieleze ni muktadha gani unaozungumziwa hapa unapozungumzia juu ya *forced marriage* ambayo ni mojawapo ya makosa ya *trafficking in persons*.

Mheshimiwa Spika, sasa kifungu hiki kinasema *a person commits an offence of trafficking in persons if that person...* tunakuja *(b) Introduces or matches the persons to a foreign nation for marriage for the purpose of acquiring, buying, offering, selling or trading the person in order that person be engaged in prostitution phonography, sexual exploitation, forced labor, slavery, involuntary servitude or date bondage.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, neno *forced marriage* muktadha wa kwanza ndiyo huo ambao nimeusema hii itaitwa *forced marriage if a person introduces or matches a person to a foreign nation for marriage and or those other things* ambazo nimevieleza.

Mheshimiwa Spika, lakini (c) inasema *offers or contracts marriage real or simulated for the purpose of acquiring, buying, offering, selling or trading a person in order that person be engaged in prostitution, phonography sexual exploitation forced labor or slavery involuntary servitude or date bondage.*

Kwa hiyo mazingira mengine ambapo kutakuwa na f*orced marriage* ndiyo hayo ambayo yameelezwa katika kifungu kidogo hicho. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwasi neno *forced marriage* litatafsirika kwamba muktadha wa hivyo vifungu nilivyovisoma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii lakini pia kutoa ufafanuzi katika maeneo mbalimbali ambapo Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi na baada ya majumuisho haya naomba tena kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru tena Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi wako wa undani zaidi kuhusiana na mjadala uliotokea kabla ya hapa, katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI- KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima!

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2021)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujielekeze katika Muswada wetu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021*(The written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2021.* Ukurasa wa Nne.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Mheshimiwa *AG* mtoa hoja tunaomba taarifa.

**TAARIFA**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5), wa mwaka *2021 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021]* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous*

*Amendments) (No. 5), Bill, 2021]* kama ulivyorekebishwa na katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa taarifa hiyo muhimu. Sasa kama ilivyo ada naomba niwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2021.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. Napenda nitumie nafasi hii kukushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, timu yote iliyohusika na Muswada huu kutoka Serikalini lakini pia Kamati yetu ya Katiba na Sheria, Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wadau mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo tumeutendea haki Muswada huu, umepitiwa kwa uhakika kabisa, kila mahali pameangaliwa vizuri kwa umakini mkubwa, lakini kabla hatujamaliza hatua hii sasa nimuite Katibu ili akamilishe mchakato wetu kwa kusoma mara ya tatu. *(Makofi)*

**NDG. MOSSY LUKUVI-KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Tisa (9) kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Law updated with some challenges observed in its implementation).*

*(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii sasa kilichobakia ni kuupeleka Muswada huu mbele ya Mheshimiwa Rais kwa ajili ya baraka zake na hilo litakapotokea tutakuja kuwajulisha rasmi kwamba sasa umekuwa Sheria kamili ya Nchi. Kwa hiyo, safari yake inaendelea lakini kwa maana ya Bunge tumeshamaliza hatua zote tatu muhimu katika kushughulikia Muswada wowote wa Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tarehe 8 Septemba, Saa Nne asubuhi kutakuwa na semina kwa Wabunge wote pale Msekwa kuhusu huduma zinazotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa na itaendeshwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF).* Kwa hiyo, wale waliokuwa na maswali na nini basi kesho tukutane pale Saa Nne ili mambo yaweze kuwekwa sawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zetu zilizopangwa leo zimekamilika zote, ninawashukuru sana kwa hilo, basi nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Nane kamili mchana.

*(Saa 11.50 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Septemba, 2021 Saa Nane Mchana)*